ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Nne - Tarehe 4 Agosti 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika: (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 - Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleao

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: *Audhubillah minashaitwan Rajim Bismillah Rahman Rahim.*

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine katika kikao hiki kinachoendelea cha Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tukiwa wazima na wenye afya njema. Itakumbukwa kuwa mwanzoni mwa kikao hiki niliwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/2014, ambayo yaliidhinishwa na Baraza hili Tukufu. Nawashukuru nyote Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena namshukuru sana Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima na imara kwa nchi yetu na imani yake kwangu binafsi**.** Nawashukuru pia, wasaidizi wake wakuu, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi,

Makamu wa Pili wa Rais kwa msaada na miongozo yao kwangu binafsi na kwa Ofisi yangu. Kwa ujumla shukurani zangu kwako wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kutuongoza hapa Barazani hadi leo hii tunakaribia kuhitimisha kikao hiki muhimu cha Baraza kilichopitia, kushauri na kuidhinisha Mapendekezo ya bajeti za wizara mbali mbali za Serikali yetu ya Mapinduzi. Kupitia kwako naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa kupitia Mapendekezo haya, kuyatolea maelekezo na hatimae kuridhia yawasilishwe mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, aidha**,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wote wa Ofisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, unaoongozwa na Ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Ndugu. Amina Kh. Shaaban, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Juma A. Hafidh, Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa michango na ushirikiano wao wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo haya ya utangulizi na shukurani, naomba nianze kwa kuwakumbusha wajumbe wa Baraza lako Tukufu majukumu ya Ofisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango na Maendeleo. Kimsingi majukumu ya Ofisi hii yamejikita katika maeneo mawili makuu:

i) Mipango ya kitaifa (ikiwemo usimamizi wa Mipango ya Maendeleo ya Uchumi); na
ii) Fedha (masuala ya kitaifa na kisekta).

Utendaji wa Ofisi hii kwa ujumla unasimamiwa na Katibu Mkuu na masuala ya Uchumi na Mipango ya Kitaifa yanasimamiwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2012/13 NA MALENGO YA MWAKA 2013/14

Mhe. Naibu Spika**,** utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii unaongozwa na Katiba ya nchi, Sheria za Kodi, Sheria za Fedha, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Sheria ya Tume ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010, DIRA ya Maendeleo ya 2020, MKUZA II pamoja na maelekezo mbali mbali ya Tume ya Mipango, Baraza la Mapinduzi na miongozo ya Baraza la Wawakilishi.

MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kusimamia mapato ya nchi kwa ujumla, ambayo maelezo yake nimeshayatoa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali, Ofisi hii pia inawajibu wa kukusanya mapato ndani ya Idara zake na baadae kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2012/13, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 4,049.42 milioni kutoka vyanzo mbali mbali vya ndani. Mpaka kufikia Juni 30, 2013, Ofisi iliweza kukusanya jumla ya TZS 3,921.90 milioni, sawa na asilimia 96.9 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 131,500.0 milioni, ambapo TZS 37,249.00 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 38,352.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo TZS 8,325.0 milioni kama ni mchango wa Serikali na TZS 30,027.0 milioni ikiwa ni misaada na mikopo kutoka nje. Mfuko Mkuu wa Serikali ulikadiriwa kutumia TZS 54,900.00 milioni. Bajeti hii imeongezeka baada ya kufanya uhaulishaji kwa ajili ya ununuzi wa meli ya Serikali. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi imeweza kutumia jumla ya TZS 37,249.00 milioni sawa na asilimia 100 kwa kazi za kawaida na TZS 8,897.84 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika kuelezea utekelezaji wa fedha kwa mwaka uliopita. Kiambatisho Nam. IV kinaonesha mchango wa Serikali katika matumizi ya Programu na miradi ya maendeleo Ki-Idara ambapo jumla ya TZS 4,202.13 milioni sawa na asilimia 50 zilitumika. Kiambatisho Nam. V kinaonesha fedha zilizopatikana kama mchango wa Serikali kimradi. Matumizi ya TZS

54,900.00 milioni yalifanyika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka 2012/13. Viambatisho Nam. VI na VII vinaonyesha mgawanyo wa rasilimali kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2013/14.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza muhtasari wa mapato na matumizi sasa naomba nieleze mapitio ya utekelezaji wa mipango na bajeti ki–Idara na taasisi na kuelezea malengo ya mwaka 2013/14.

UTEKELEZAJI 2012/2013 NA MAKADIRIO 2013/2014 KI-IDARA NA TAASISI

TUME YA MIPANGO

Mhe.Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeanzisha Tume ya Mipango kuwa ndio chombo cha juu kabisa kwa ajili ya kupanga Maendeleo yetu ya Kiuchumi na kijamii. Tume hii imeundwa upya kufuatia kutungwa kwa Sheria mpya Namba 3 ya mwaka 2012. Sekretarieti ya Tume hii ya Mipango inaundwa na Idara tatu na Taasisi moja inayojitegemea katika kusimamia masuala ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Idara na taasisi hizo ni, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini, Idara ya Ukuzaji Uchumi, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa Idara zinazounda Sekretarieti ya Tume ya Mipango ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA MASKINI

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kuangalia Mipango ya Kitaifa kwa ujumla na jinsi Sekta mbali mbali zinavyotekeleza masuala mbali mbali ambayo yanasaidia katika kupunguza umasikini. Kwa mwaka 2012/2013, Idara iliidhinishiwa jumla ya TZS 225.90 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 2,318.2 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2013, Idara ilishapatiwa jumla ya TZS 225.90 milioni kwa kazi kawaida sawa na asilimia 100 na TZS 1,382.6 milioni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 59.6 ya makadirio. Fedha hizi zilitumika katika kutekeleza yafuatayo:

i) Kuchapisha nakala 300 za vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo 2012/2013 na vitabu 500 vya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014;

ii) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013 wenye programu 22 na Miradi 81 ya maendeleo Unguja na Pemba, ambapo changamoto mbali mbali zilijitokeza zikiwemo, fedha za Miradi kuhaulishwa na kutumika kinyume na shughuli zilizokusudiwa. Changamoto hizi zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi unaostahiki ili kuleta ufanisi wa utekelezaji;

iii) Kufanya mapitio ya Sekta ya Fedha katika maeneo ya huduma za kibenki, huduma ndogo ndogo za kifedha, shughuli za Bima, Soko la mitaji, shughuli za mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kazi ya mapitio inatarajiwa kukamilika katika robo ya kwanza ya mwaka 2013/14;

iv) Kutayarisha ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa MKUZA II, 2012/13 inayotarajiwa kukamilika robo ya kwanza ya 2013/14;

v) Utayarishaji wa kuandaa kanuni za Sheria ya Tume ya Mipango;

vi) Kuandaa Vikao viwili vya Tume ya Mipango.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya TZS 688.20 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 4,419.80 milioni kwa kazi za maendeleo. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni:

i) Kukusanya na kuandaa taarifa za Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 na kuandaa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015;

ii) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014 wenye programu 35 na miradi 75 ya maendeleo Unguja na Pemba;

iii) Kuandaa kikao na Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali kwa ajili ya matayarisho ya bajeti ya maendeleo ya mwaka 2014/15;

iv) Kuandaa vikao vinne vya Tume ya Mipango na sita vya kamati Tendaji ya Tume;

v) Kuandaa Mafunzo kwa Maafisa Mipango 40 wa wizara 16 za Serikali kuu, Serikali za mitaa na Taasisi juu ya uchambuzi wa Sera *Policy Analysis*;

vi) Kuandaa maonesho ya maadhimisho ya wiki ya Umasikini;

vii) Kufanya Uchambuzi wa Hali ya Umasikini kwa vijiji vitano (5) na kuandaa taswira ya Umasikini *Poverty Profile* kwa kuzingatia Ripoti ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya;

viii) Kutoa mafunzo kwa watendaji 35 juu ya Uandaaji wa Mipango;

ix) Kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini yenye kuleta matokeo kwa watendaji wa vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini vya wizara za Serikali;

x) Kutayarisha mfumo wa ufuatiliaji *ICT* wa Upatikanaji na uwekaji wa Taarifa;

xi) Kuandaa taarifa za maendeleo ya watu Zanzibar na utekelezaji wa Malengo ya Milenia.

xii) Kufanya tathmini ya mahitaji ya vifaa, mafunzo na muundo wa Taasisi ndani ya Tume ya Mipango na Idara za Mipango, Sera na Utafiti pamoja na kuandaa mpango kazi ili kuimarisha utendaji wa taasisi hizi;

xiii) Kuratibu vikao vya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania.

IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe.Naibu Spika, jukumu kuu la Idara hii ni kuangalia mwenendo mzima wa ukuaji Uchumi wa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/13, idara ilipangiwa kutumia TZS 288.018 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 150.00 milioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Juni 2013, Idara iliweza kutumia jumla ya TZS 288.018 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka. Aidha, TZS 22.8 milioni zilitumika kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 15 ya makadirio. Katika kutumia fedha hio, Idara imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kufuatilia Mwenendo wa Uchumi kwa kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Benki Kuu ya Tanzania Tawi la Zanzibar;

ii) Kutathmini na kushauri juu ya mwenendo wa Mfumko wa bei kila mwezi;

iii) Utunzaji wa Taarifa za Takwimu za Kifedha za Serikali kwa kuwekewa "*Database*" litakaloendelea kufanyiwa mapitio kila Takwimu mpya zinapotolewa;

iv) Kufanya mapitio ya mfumo wa utabiri wa Uchumi na wa mapato kwa kila takwimu mpya zinapotolewa kwa ajili ya kutabiri mwenendo wa viashiria vya Uchumi na Mapato;

v) Kupendekeza marekebisho ya sheria za kodi kupitia kitengo cha sera za kodi kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wakiwemo Sekta binafsi;

vi) Kuanzisha Kitengo kinachoshughulikia Miradi itakayoekezwa kwa mashirikiano ya Serikali na Sekta binafsi *(Public Private Partnership);*

vii) Kufanya mafunzo ya awali ya modeli ya programu ya kifedha kwa wafanyakazi;

viii) Kujenga uwezo wa Idara kwa kuwapatia wafanyakazi sita (6) mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya pili na wafanyakazi sita (6) mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi ndani na nje ya nchi;

ix) Kuandaa na kuutumia mfumo mpya wa taarifa unaohusiana na idadi za bidhaa katika kufanya uchambuzi na kutoa taarifa sahihi za mwenendo wa bei za bidhaa nchini;

x) Kuiwakilisha Serikali katika vikao vya kitaalamu vya Kikanda ikiwa ni pamoja na vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mashirikiano na nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya na Mashirikiano ya Jumuia ya Utatu,

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya TZS 426.69 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 150.00 milioni kwa kazi za maendeleo kwa kutekeleza mambo yafutayo:

i) Kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ili kujua mchango na ukuaji wa kila sekta katika Pato laTaifa;

ii) Kupitia na kuchambua taarifa za hali ya mfumko wa bei na kufuatilia mwenendo wake kwa kila mwezi ili kutoa mapendekezo ya hatua za muda mfupi na mrefu za kudhibiti mfumko wa bei nchini;

iii) Kuimarisha kitengo cha kutunza Taarifa zaTakwimu za kifedha za serikali kwa kuendelea kuliongezea *Database* Moduli mpya kila zinapopatikana taarifa;

iv) Kuandaa tafiti mbili za kiuchumi katika maeneo ya mchango wa wajasiriamali wadogo na wa kati katika Uchumi na utafiti juu ya Maendeleo ya viwanda Zanzibar;

v) Kuimarisha kitengo cha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na sekta Binafsi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi, kukamilisha Sera, mapitio ya sheria na muongozo juu ya Mashirikiano hayo;

vi) Kufanya mapitio na kuendeleza mfumo wa utabiri wa uchumi na wa mapato kila takwimu mpya zinapotolewa ili kurahisisha kufanya makadirio ya viashiria vya uchumi;

vii) Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha sera ya kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wa kodi;

viii) Kuanza kutumia programu ya kifedha kwa kufanya utabiri wa uchumi wa kila robo mwaka;

ix) Kuendelea kuiwakilisha Serikali katika mikutano, majadiliano na kufuatilia masuala yanayohusu ushirikiano wa kikanda.

IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe.Naibu Spika, kwa ujumla idara hii ina jukumu la kuangalia maendeleo ya Watendakazi na hali ya Ukuaji wa Idadi ya Watu. Kwa mwaka 2012/2013, Idara ilipangiwa kutumia TZS 188.47 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 190.00 milioni kwa kazi za maendeleo kama mchango wa Serikali. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka, Idara ilifanikiwa kupata jumla ya TZS 188.47 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 100 ya makadirio na TZS 176.11 milioni ni mchango wa Serikali kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 92.7 ya makadirio. Matumizi ya fedha hizi yalielekezwa katika maeneo yafuatayo:

i) Kuandaa utafiti mdogo juu ya umakini wa mafunzo ya amali katika ajira;

ii) Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa za utafiti wa Hali ya Utumishi Unguja na Pemba;

iii) Kuandaa mikutano miwili (2) ya wadau wa masuala ya idadi ya watu Zanzibar kwa robo tatu za mwaka 2012/2013;

iv) Kutayarisha na kuiwasilisha kwa wadau taarifa ya mwaka 2012 juu ya masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo Zanzibar yenye ujumbe wa “Vijana na Ajira**”;**

v) Kutoa mafunzo kwa Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na maafisa Mipango wapatao 35 juu ya kuoanisha viashiria vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na bajeti;

vi) Kwa usaidizi wa mtaalamu wa ndani, Idara imefanya tathmini, mapitio na majaribio ya daftari la shehia na matokeo yake yameshajadiliwa katika mikutano miwili ya wadau;

vii) Kufanya tathmini juu ya utekelezaji wa program ya Uhai, Hifadhi, Maendeleo ya Mama na Mtoto katika ngazi ya Shehia na wilaya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya TZS 149.104 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 342.00 milioni kwa kazi za maendeleo ili kutekeleza yafuatayo:

i) Kufanya uratibu juu ya masuala ya idadi ya watu, watendakazi na ustawi wa mama na mtoto katika ngazi mbalimbali;

ii) Kukamilisha utafiti wa umakini wa mafunzo ya amali katika ajira na taarifa zake kuziwasilisha kwa wadau Unguja na Pemba;

iii) Kuendelea na hatua za utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini kwa kukamilisha ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na uandikaji ripoti;

iv) Kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili ripoti juu ya Hali na Ustawi wa wastaafu Zanzibar 2012/2013;

v) Kufanya mapitio ya vipaumbele juu ya mahitaji ya wataalamu nchini kutokana na Matokeo ya Utafiti wa Hali ya Utumishi;

vi) Kuchapisha daftari la shehia lililofanyiwa mapitio na kutoa mafunzo kwa masheha na wasaidizi wao juu ya matumizi yake;

vii) Kutayarisha ripoti ya mwaka 2013/14 juu ya masuala ya idadi ya watu Zanzibar, pamoja na kuandaa mikutano ya kila robo mwaka juu ya masuala ya idadi ya watu;

viii) Kushiriki katika maandalizi na kilele cha maadhimisho ya siku ya idadi ya watu duniani ya mwaka 2014;

ix) Kutayarisha ripoti juu ya masuala ya idadi ya watu na athari zake kijamii na kiuchumi kwa madhumuni ya kuwasilishwa kwenye kikao cha Tume ya Mipango;

x) Kutafsiri na kuchapisha Ripoti ya tathmini juu ya takwimu za kijamii;

xi) Kuandaa mikutano miwili ya Kamati ya Wataalamu juu ya programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto;

xii) Kutathmini utekelezaji wa program ya hifadhi ya mama na mtoto katika ngazi ya sekta, wilaya na shehia;

xiii) Kufanya tathmini juu ya sababu zinazopelekea kuongezeka kwa matukio ya vifo vinavyotokana na uzazi pamoja na mapungufu katika masuala ya lishe na usafi wa mazingira kwenye ngazi za Shehia.

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** jukumu kubwa la Ofisi hii ni kukusanya na kuzichambua takwimu za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka wa fedha 2012/13 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu SMZ ilipangiwa jumla ya TZS 1,262 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na TZS 2,900 milioni kwa utekelezaji wa kazi za miradi ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika**,** Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2013, jumla ya TZS 1,262 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ziliweza kupatikana kwa kutekeleza kazi za kawaida na TZS 1,164 milioni sawa na asilimia 40 ya makadirio zilipatikana kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliweza kufanya yafuatayo:

i) Kukusanya Takwimu za Kijamii na Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2012 na kutoa Ripoti yake, iliyobainisha ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2012;

ii) Kukamilisha matayarisho yote na kusimamia kwa upande wa Zanzibar Sensa ya Watu na Makazi ya Tanzania, iliyofanyika tarehe 26 Agosti, 2012;

iii) Kufanya tafiti katika sekta ya uzalishaji na viwanda, utalii, uwekezaji, na utumiaji wa huduma ya maji Zanzibar ambapo utafiti wa uzalishaji wa viwanda,utalii na uwekezaji ripoti zake bado ambapo utafiti wa utumiaji wa huduma ya maji Zanzibar ripoti yake imekamilika na kuonesha matumizi, mtandao na upatikanaji wa maji nchini;

iv) Kukamilisha na kuwasilisha kwa wadau taarifa za tafiti nne (4) juu ya Viashiria vya UKIMWI, Malaria, Sensa ya Kilimo na ile ya Mifugo za mwaka wa 2011/12;

v) Kuwapatia mafunzo katika ngazi ya Shahada ya uzamili *Masters Degree* jumla ya maafisa Takwimu (7), mmoja (1) katika fani ya

TEHAMA na Takwimu, Ofisa mmoja (1) katika Stashahada ya Uzamili *Post Graduate Diploma*, mmoja (1) katika fani ya Uchambuzi wa Umasikini, *Poverty Analysis*, maafisa sita (6) katika ngazi ya Shahada ya kwanza katika fani ya Takwimu na Uchumi, na maofisa wawili (2) Stashahada katika fani ya takwimu na rasilimali watu;

vi) Kuwapatia jumla ya maofisa kumi na moja (11) mafunzo ya muda mfupi katika fani za Uhasibu, Uongozi wa miradi ya maendeleo, Ukaguzi na Tathmini *Monitoring & Evaluation*, Rasilimali watu *HR*, na masuala ya Takwimu *Statistical packages*.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2013/2014, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaombewa jumla ya TZS 1,550 milioni ikiwemo ruzuku ya TZS 1,300 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na jumla ya TZS 250.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mmoja wa Maendeleo. Ofisi inatarajia kupokea jumla ya TZS 3,933.0 milioni kama mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania *TSMP* kwa upande wa Zanzibar, na TZS 36.0 milioni zinatarajiwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania ikiwa ni mchango wake kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu za Faharisi ya Bei *Consumer Price Index* na takwimu za

Pato la Taifa kwa robo mwaka. Mambo yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

i) Kufanya Utafiti wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2013 na kutoa taarifa yake ikiwa ni pamoja na taarifa ya makadirio ya ukuaji uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2013;

ii) Kutekeleza Mpango wa Sensa na Utafiti kwa kufanya tafiti zikiwemo za Sekta Isiyo Rasmi *Zanzibar Informal Sector Survey*, Utafiti wa Hali ya Nguvu Kazi *Zanzibar Integrated Labour Force Survey*, Utafiti wa Viashirio vya Kiuchumi na Kijamii Tanzania Panel Survey, Utafiti wa Sekta ya Biashara, Usafiri na Ujenzi *Integrated Survey on Trade, Transport and Communication*;

iii) Kuendelea na Uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Watu na Makaazi na kutoa taarifa zake;

iv) Kutekeleza Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania ikiwa ni pamoja na kuanza kazi za usanifu na uchoraji wa ramani za jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar;

v) Kuendeleza na kukuza taaluma za kitakwimu hapa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo maofisa takwimu, kuendesha semina na mikutano ya watoaji na watumiaji wa takwimu, kuimarisha mifumo ya utoaji na uhifadhi wa takwimu kwa kutumia mitandao ya *"Tanzania Socio-Economic Database*" (*TSED*) na *"National Data Archives"* (*NADA*), na kutoa miongozo ya ukusanyaji, uchambuzi na uwekaji wa takwimu rasmi miongoni mwa Idara na Taasisi za Serikali.

MASUALA YA FEDHA

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema, Ofisi yangu inasimamia Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia Tume ya Mipango. Ofisi pia inasimamia masuala ya Fedha Serikalini. Idara zinazosimamia masuala ya fedha ni Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Bajeti, Idara ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma, na Idara ya Fedha za Nje.

Baada ya kukamilisha maelezo yanayohusu masuala ya Uchumi na Mipango, naomba sasa nieleze masuala ya Fedha.

IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara hii ndio inayosimamia masuala ya fedha nchini ikiwemo utunzaji wa mapato, udhibiti wa matumizi pamoja na kuwaendeleza Wahasibu na Wakaguzi. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/13,

B1. IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ndio inayosimamia masuala ya fedha nchini ikiwemo utunzaji wa mapato, udhibiti wa matumizi pamoja na kuwaendeleza Wahasibu na Wakaguzi. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/13, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 2,371.163 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 40.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Juni 2012/13, Idara ilipatiwa jumla ya TZS 2,371.163 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio kwa kazi za kawaida na jumla ya TZS 38.0 milioni sawa asilimia 95 kwa kazi za Maendeleo. Mambo yaliyotekelezwa kwa mwaka huo ni:

i) Kusimamia mapato na kuendelea kuimarisha udhibiti na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
ii) Kukamilisha ufungaji wa hesabu za mwaka 2011/12 na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
iii) Kuratibu vikao kumi na moja (11) vya kila mwezi vya Kamati za Ukomo wa matumizi;
iv) Kulipa kwa wakati TZS 132,660.00 milioni kwa ajili ya mishahara Serikalini, TZS 100,020.00 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 31,270.00 milioni zikiwa ni mchango wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo;
v) Kupokea TZS 21,000.00 milioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya TZS 21,400 milioni kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni kodi ya wafanyakazi wa Muungano wanaofanya kazi Zanzibar;
vi) Kulipa TZS 8,649.02 milioni mafao ya pencheni na TZS 6,968.74 milioni kiinua mgongo kwa wastaafu 747;
vii) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani wapatao 50;
viii) Kuchapisha vitabu 15,900 vya Risiti za Serikali;
ix) Kusimamia na kuendeleza mfumo wa pamoja wa Usimamizi wa fedha (*Integrated Financial Management System - IFMS);*
x) Kusimamia deni la Taifa na kuhudhuria vikao vya Wataalam wa Kamati ya Madeni huko Tanzania Bara; na
xi) Kufanya mapitio ya sheria ya Fedha Namba 12 ya mwaka 2005 na kutoa Rasimu ya kwanza ya Ripoti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya TZS 3,183.57 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 40.00 milioni kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali katika kugharamia Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Aidha, Idara kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali imetengewa jumla ya TZS 66,056.00 milioni kusimamia matumizi ya Mfuko Mkuu. Mambo yatakayotekelezwa kwa mwaka 2013/2014 ni kama yafuatayo:

i) Kusimamia mapato na kuendelea kuimarisha udhibiti na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
ii) Kusimamia matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali;
iii) Kutoa mafunzo mafupi ya Uhasibu na Ukaguzi kwa wafanyakazi wa kada ya uhasibu na ukaguzi wa fedha wapatao 70;
iv) Kufunga hesabu za Serikali za mwaka 2012/13;
v) Kusimamia na kuimarisha mfumo wa fedha wa *IFMS* kuendana na mfumo wa *PBB* na kubadilisha "*Server*";
vi) Kuchapisha vitabu 22,000 vya Risiti za Serikali;

vii) Kuziimarisha na Kuzijengea uwezo Kamati za ukaguzi za Wizara za SMZ;
viii) Kusimamia Deni la Taifa;
ix) Kuratibu vikao kumi na moja (11) vya kila mwezi vya Kamati ya Ukomo wa Matumizi;
x) Kusimamia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma ili iendane na wakati;
xi) Kuhudhuria vikao mbalimbali vya Kamati ya Wataalam wa deni la Taifa na kamati ya Ukomo vinavyofanyika huko Tanzania Bara;
xii) Kusimamia ukusanyaji wa TZS 26,000.00 milioni kutokana na wafanyakazi wa SMT wanaofanya kazi Zanzibar.

B2. IDARA YA BAJETI

Mhe. Naibu Spika, Jukumu la Idara hii ni kusimamia Bajeti na matumizi ya Serikali pamoja na kuratibu mifumo ya Bajeti Serikalini. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 21,712.77 milioni kwa kazi za kawaida. Kati ya Fedha hizo, TZS 5,010.00 milioni ni kwa ajili ya marekebisho ya Mishahara Serikalini, TZS 426.4 milioni ni matumizi ya Idara na TZS 16,276.0 milioni kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni 2013 Idara ilitumia jumla TZS 21,712.77 milioni sawa na asilimia 100 ya Makadirio, ambapo TZS 2,490 milioni zimetumika kwa marekebisho ya Mshahara, TZS 426.4 milioni kwa kazi zake za kawaida za Idara na TZS 2,520 milioni zilihaulishwa kwenda katika kifungu cha safari za Nje za Viongozi Wakuu. Fedha za Idara zilitumika katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kusimamia, kufuatilia na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013;
ii) Kuratibu shughuli za kibajeti kwa kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi za Serikali zinatekeleza bajeti zao kulingana na mfumo wa *MTEF*;
iii) Kuratibu utayarishaji na kutoa mafunzo kwa maofisa mipango na wahasibu wa Wizara na Taasisi husika juu ya Bajeti inayozingatia Programu (PBB);
iv) Kuandaa Warsha ya uwasilishaji wa taarifa (*feedback*) kutoka *IMF* East *AFRITAC* juu ya mfumo wa PBB kwa Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti baada ya mapitio ya Wizara sita za SMZ;
v) Kuwapeleka wafanyakazi wanne (4) kwenye mafunzo ya kivitendo nchini Mauritius na wanne (4) nchini Rwanda yanayohusiana na mchakato wa utayarishaji wa bajeti inayozingatia programu (*PBB*);
vi) Kusimamia utayarishaji wa maelezo ya bajeti inayozingatia Programu kwa ajili ya kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi;

vii) Kufanya uhakiki juu ya mishahara kwa wafanyakazi wanaopelekea mishahara yao benki;
viii) Kuandaa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya TZS 36,834.12 milioni kwa kazi za kawaida, zikiwemo TZS 17,500 milioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara Serikalini, TZS 18,663.00 milioni kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na TZS 671.1 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Idara. Mambo yaliyopangwa kutekelezwa na Idara hii ni haya yafuatayo:

i) Kukamilisha Mswaada wa Sheria mpya ya Fedha;
ii) Kutayarisha na kutoa muongozo wa bajeti kwa Wizara na Taasisi husika za Serikali hadi kufikia Disemba 2013;
iii) Kuratibu utayarishaji na kutoa mafunzo kivitendo kwa Wizara zote kumi na sita (16) juu ya Bajeti inayozingatia Programu (*PBB*);
iv) Kuandaa database ya viashiria vya utekelezaji na matokeo (*KPI Database*), Muongozo wa Viashiria vya utekelezaji na kutoa mafunzo kwa maofisa OR-FUMM;
v) Kuwapatia Mafunzo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Baraza la Wawakilishi, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi za Kijamii (*CSO*) juu ya Muundo na mfumo wa bajeti inayozingatia Programu (*PBB*);
vi) Kwa kushirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali, kuandaa mafunzo na kufanya marekebisho ya kitaalamu katika mfumo wa hesabu (*Charts of Account*) pamoja na kuoanisha fedha na bajeti;
vii) Kwa kushirikiana na Idara ya Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Ukuzaji Uchumi na Idara Fedha za Nje, kutoa taarifa za bajeti kwa wananchi kwa lengo la kuwaelewesha mafungamano (*Intergration*) ya uchumi wa nchi na bajeti;
viii) Kuimarisha uwezo wa watendaji wa Idara kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo ya uandaaji na uchambuzi wa taarifa pamoja na kuwapatia vitendea kazi;
ix) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na *database* ya Mishahara na Taarifa za Watendakazi.

B3. IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Naibu Spika, jukumu la Idara ya Fedha za Nje ki ujumla ni kuimarisha uhusiano wetu na wafadhili kutoka nje pamoja na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo yetu. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 idara Ilitarajiwa

kuratibu na kusimamia upatikanaji wa jumla ya TZS 331,300 milioni ikiwa ni ruzuku na mikopo). Fedha hizo zinajumuisha TZS 105,400 milioni kama ruzuku, TZS 187,800 milioni kama mkopo na TZS 39,900 milioni ni misaada ya kibajeti.

Mhe. Naibu Spika, hadi Kufikia Juni 2013 Idara imeweza kuratibu upatikanaji wa jumla ya TZS 223,400 milioni sawa na asilimia 67.45 ya makadirio kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya kimataifa. Kati ya fedha hizo, TZS 22,110 millioni ni misaada ya kibajeti sawa na asilimia 55 ya makadirio ya TZS 39,900 milioni. Kwa upande wa Programu na miradi ya Maendeleo, Idara imeratibu upatikanaji wa TZS 201,300 milioni. Kati ya hizo TZS 131,800 milioni ni ruzuku sawa na asilimia 125.05 ya makadirio ya TZS 105,400 milioni. Ongezeko hili limetokana na kuwa hakukuwa na makadirio ya matumizi ya mradi wa usambazaji wa umeme Unguja kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*) na makadirio madogo kwa mradi wa utandazaji wa waya wa umeme chini ya bahari kutoka Rasi Kiromoni hadi Fumba kupitia Changamoto ya Milenia ya Marekani (*MCC*-A).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa 2012/2013 Idara iliidhinishiwa matumizi ya TZS 120. 45 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,382.0 milioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia June 2013 Idara ilitumia jumla ya TZS 120. 45 milioni sawa na asilimia 100 za makadirio kwa kazi za kawaida na TZS 399.8 milioni sawa na asilimia 28.9 kwa kazi za Maendeleo na kuweza kutekeleza yafuatayo:

i) Kushiriki mikutano mitano (5) ya kimataifa na mikutano na washirika mbali mbali iliyofanyika nje ya Nchi kwa lengo la kuendeleza mashirikiano na Washirika wa Maendeleo;
ii) Kushiriki mikutano11 ya Taasisi za Serikali na minne (4) ya sekta binafsi ambayo imefanyika kufuatilia taarifa za misaada na utekelezaji wake;
iii) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wanane (8) wa Idara katika fani ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za misaada.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya TZS 94.5 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 995.03 milioni kwa kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Pili na TZS 494.45 milioni kwa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar. Shughuli nyengine zitakazofanyika ni pamoja na:

i) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali itakayofikia TZS 235,411 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kupitia programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo TZS 148,614.0

milioni zinatarajiwa kupatikana kupitia mikopo na TZS 86,797.0 milioni ni ruzuku. Misaada ya kibajeti (*GBS*) inatarajiwa kufikia TZS 40,000.00 milioni kwa mwaka 2013/2014. Kati ya fedha hizo, TZS 26,500.0 milioni zitatokana na ruzuku na TZS 13,500.0 milioni zitatokana na mikopo ya kibajeti. Aidha, Serikali inatarajiwa kupata TZS 2,510.00 milioni kupitia Fedha za Msamaha wa Madeni (*MDRI*);

ii) Kufuatilia na kufanya uchambuzi wa taarifa za misaada;

iii) Kuimarisha ushirikiano na uratibu wa misaada baina ya Washirika wa Maendeleo pamoja na Mashirika na Taasisi za Serikali.

B.4 IDARA YA UHAKIKIMALI NA MITAJI YA UMMA

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia Mali za Serikali hasa katika manunuzi na uuzaji pamoja na Mitaji ya Umma. Kwa mwaka 2012/2013 Idara ilitengewa jumla ya TZS 287.2 milioni kwa kazi za kawaida, ambapo mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2013 jumla ya TZS 287.2 milloni ziliweza kupatikana sawa na asilimia 100 ya makadirio. Aidha, kwa kazi za maendeleo jumla ya TZS 6,000.00 millioni zilitengwa kwa kazi za ujenzi wa Ofisi za Serikali na uhakiki wa mali za Serikali, ambapo jumla ya TZS 3,300.00 milioni sawa na asilimia 55 ziliweza kupatikana. Fedha zote hizi zilitumika katika kutekeleza yafuatayo:

i) Kusimamia ukamilishaji wa Daftari la Mali za Serikali kwa Wizara tano (5); za Miundombinu na Mawasiliano, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Afya na Elimu na Mafunzo ya Amali;

ii) Kufanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara 14 na taasisi zake kwa mwaka 2012/13 sambamba na kuhakiki Mali za serikali;

iii) Kusimamia Mitaji ya Serikali ambapo jumla ya TZS 401.50 millioni zilikusanywa kutoka vyanzo vya mapato vifuatavyo: Mashamba ya Mipira, Kodi katika nyumba ya *Afrika House* na ukodishwaji wa matangi ya mafuta;

iv) Kutoa mafunzo ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mashirika ya Bima, Utalii na Meli ili taasisi hizo ziweze kufanya manunuzi ya vifaa vyao kama Sheria za manunuzi zinavyoelekeza;

v) Kutoa mafunzo ya siku tatu (3) kwa Wahakikimali wa Wizara za Serikali ili kuweza kupata taaluma na njia sahihi za ukaguzi wa manunuzi na Mali za Serikali;

vi) Kufanya tathmini ya utendaji, masoko, muundo na mitaji kwa Mashirika manne (4) ya Serikali likiwemo Shirika la Meli, Utalii,

Bima na Magari. Kwa ujumla Shirika la Magari na Utalii yameonekana kutofanya vizuri katika biashara zao;

vii) Kufanya uchanganuzi wa hesabu za mwaka 2010/11 kwa Shirika la Bima, Bandari, *ZSTC* na *PBZ* yameonesha kutengeneza faida katika biashara zao, kwa ujumla yameweza kulipia Serikalini gawio la faida la jumla ya TZS 400.00 millioni;

viii) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Wizara ya Katiba na Sheria na kwa sasa ujenzi umeshafikia ghorofa ya tano (5) kati ya ghorofa nane.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya TZS 502.70 millioni kwa kazi za kawaida na TZS 7,500.00 milioni kwa kutekeleza miradi miwili ya maendeleo. Malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na yafuatayo:

i) Kuendelea kusimamia na kutathmini Mashirika, Mitaji kwa viwanda vya *ZAPOCO*, Kiwanda cha Sukari na Manukato - Mahonda, Cocacola na Hisa za Serikali zikiwemo ZANTEL na Benki ya Posta;

ii) Kufatilia taratibu za manunuzi pamoja na uhakiki wa Mali za Serikali kwa Wizara 16 na Taasisi zake kwa mwaka 2012/2013;

iii) Kuendeleza tathmini ya Mali za Serikali kwa wizara tatu (3) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Katiba na Sheria, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto;

iv) Kuendelea kuifanyia mapitio Sheria namba 9 ya Manunuzi ya mwaka 2005;

v) Kuwajengea uwezo watendaji watano (5) wa Idara katika masuala ya usimamizi wa Mitaji na Mali za Serikali;

vi) Kuandaa miongozo ya manunuzi (*Procurement Guidelines*) pamoja na kuwapatia mafunzo watendaji wote wa Idara juu ya taaluma hiyo.

C. IDARA ZA URATIBU NA UTAWALA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo inasimamia pia shughuli za Uratibu na Utawala kupitia Idara zake nne (4) ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi Kuu ya Pemba na Idara ya Uratibu wa shughuli za SMZ Dar es Salaam.

C.1 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia masuala yote ya utendaji na Utumishi ndani ya Ofisi ya Raisi fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Idara hii kwa mwaka 2012/13, iliidhinishiwa jumla ya TZS

16,127.49 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida, ambapo mpaka kufikia mwezi Juni 2013 ilishatumia jumla ya TZS 16,127.49 milioni sawa na asilimia 100 ya makadiro. Matumizi haya yalifanyika katika kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapatia watendaji 65 mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya Tanzania katika fani za uhasibu, ununuzi na ugavi, teknolijia ya Habari, fedha, uchumi na rasilimali watu;
ii) Kuwapatia watendaji 90 mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi;
iii) Kusimamia na kugharamia vikao 15 vya Bodi ya Zabuni na vikao vyengine mbali mbali vya uongozi wa Ofisi;
iv) Kusimamia ukarabati na ujenzi wa Ofisi Pemba ambapo tayari Ofisi imekamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo litakalotumiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto;
v) Kuwapatia wafanyakazi 150 likizo zao pale walipostahiki;
vi) Kuwahudumia viongozi wakuu wa Serikali katika safari zao za ndani na nje ya nchi;
vii) Kuendelea na udhamini wa wanafunzi 1,377 katika vyuo mbalimbali nchini Tanzania katika fani za Uchumi, Fedha, Uhasibu, Manunuzi na Ugavi pamoja na Teknolojia ya Habari.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya TZS 3,962.35 milioni ili kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi 85 wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani zinazohusiana na majukumu ya Ofisi;
ii) Kuwapatia likizo za mwaka watendaji 200;
iii) Kwa kushirikiana na Wizara husika, kusimamia kuanza rasmi ujenzi wa jengo la Ofisi huko Pemba kwa ajili ya Ofisi za Wizara tatu;
iv) Kuwapatia udhamini wanafunzi 1,000 katika vyuo mbali mbali kwa fani zinazohitajika na Wizara ambapo Wanafunzi 634 wanaendelea na masomo na Wanafunzi 366 wataanza mwaka wa masomo 2013/2014;
v) Kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 50 kwa lengo la kuielewa vizuri Sheria mpya Namba 2 ya Utumishi wa Umma;
vi) Kuratibu shughuli za ukaguzi wa hesabu na utendaji wa Wizara;
vii) Kuendeleza mazingira bora ya kazi na huduma za kiutawala kwa kuwapatia watendaji vitendea kazi na maeneo bora ya kazi.

C.2 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13, Idara ilikadiriwa kutumia TZS 134.19 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 20,504.69 milioni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Juni 30 mwaka 2013 Idara ilitumia TZS 134.19 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio kwa kazi za kawaida na TZS 2,465.0 milioni sawa na asilimia 12 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/13 Idara imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na kuandaa Ripoti mbali mbali za utekelezaji;
ii) Kusimamia maandalizi ya bajeti ya Wizara mwaka 2013/2014;
iii) Kuandaa warsha mbili za kuhamasisha wafanyakazi kuhusiana na masuala ya mtambuka;
iv) Kuratibu maandalizi ya Sera na Mkakati wa Sekta ndogondogo za Fedha pamoja na kukamilisha marekebisho ya sheria ya *ZSSF* na *ZIPA*;
v) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Ofisi;
vi) Kushiriki katika mikutano minne (4) huko Tanzania Bara iliyojadili mageuzi ya sekta ya fedha na uimarishaji wa Sekta ndogo ndogo za fedha nchini;
vii) Kutayarisha hadidu rejea za kumpata Mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango mkakati na Muongozo wa Utekelezaji wa Programu ya Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma;
viii) Kukamilisha ununuzi magari 17, piki piki 32, vifaa vya kukusanyia taka 1000 pamoja na kukamilisha Ripoti tatu (3) za ushauri kwa mradi wa Uimarishaji Huduma za Kijamii Mijini (*ZUSP*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2013/14, Idara inaombewa jumla ya TZS 285.30 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,250.00 milioni kwa kazi za Maendeleo. Aidha Idara itaratibu matumizi ya TZS 17,000.00 milioni kwa ununuzi wa meli ya Serikali. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

i) Kuiimarisha na kuipanua sekta ya fedha ili iweze kuchangia zaidi uchumi wa Zanzibar kwa kuandaa Sera, Mkakati na Mpango kazi wa utekelezaji;
ii) Kukamilisha Sera ya Taasisi ndogondogo za kifedha;
iii) Kuratibu mapitio ya Mipango, Sera na Sheria za *ZSSF*, *ZIPA*, Sheria za Fedha za Umma na Sheria ya Manunuzi ndani ya Wizara na Taasisi zake;

iv) Kuratibu utayarishaji wa ripoti za robo, nusu na mwaka pamoja na Bajeti ya Wizara;

v) Kuhamasisha na kushajihisha masuala Mtambuka katika Wizara na taasisi zake;

vi) Kuratibu na kusimamia utendaji wa Bodi na Baraza la Rufaa ya Kodi kwa ajili ya kutatua migogoro ya walipa kodi;

vii) Kuwajengea uwezo na kuandaa mazingira bora kwa wafanyakazi wa Idara ikiwemo mafunzo maalum juu ya Uchambuzi wa Sera, uandaaji wa tafiti na tathmini ya sekta ya fedha nchini;

viii) Kuratibu ununuzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya Serikali;

ix) Kuratibu miradi ya Wizara ikijumuisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Maeneo Huru Fumba, mradi wa kuimarisha Huduma za Miji Unguja na Pemba, mradi wa Ujenzi wa Maabara ya komputa (*ZIFA*), Programu ya Usimamizi wa Mageuzi ya Fedha za Umma (*PFMRP*) na mradi wa Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Pili.

C.3 OFISI KUU - PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu Pemba ambayo inatekeleza shughuli za Ofisi kwa upande wa Pemba. kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 iliidhinishiwa jumla ya TZS 663.48 milioni kwa kazi za kawaida, ambapo mpaka kufikia mwezi Juni 2013, Ofisi ilishapatiwa jumla ya TZS 663.48 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio. Shughuli zilizofanywa katika utekelezaji wa majukumu hayo ni kama zifuatazo:

i) Kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuongeza ufanisi bora;

ii) Kulipia gharama mbali mbali za uendeshaji wa Ofisi na huduma;

iii) Kuimarisha huduma za mtandao wa *IFMS*;

iv) Kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi katika fani mbali mbali, ambapo jumla ya wafanyakazi 21 wakiwemo wanawake 6 na wanaume 15 walipatiwa mafunzo ikiwemo shahada ya uzamili ya usimamizi wa fedha (7); shahada ya uzamili ya uhasibu (6); shahada ya kwanza ya uhasibu (5) shahada ya kwanza ya Ununuzi na Ugavi (2); na shahada ya kwanza ya masoko (1);

v) Kuratibu shughuli za manunuzi ya vifaa na huduma katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko na Baraza la Mji la Chake Chake;

vi) Kufanya ukaguzi na uhakiki wa mali za Serikali katika Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais na *MBLM*, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za wakuu wa Wilaya ikiwemo wilaya ndogo ya Kojani;

vii) Kutoa mafunzo kwa maofisa Mipango 24 wa Wizara zote juu ya utayarishaji na uimarishaji wa Daftari la Mali za Kudumu za Serikali (*Fixed Assets Register*);

viii) Kutoa mafunzo kwa Wahasibu na Wakaguzi wa ndani wa hesabu za Serikali 22 juu ya Sheria ya Fedha Nam. 5 ya 2005, pamoja na kuwajengea uwezo wa kazi zao juu ya matumizi ya mtandao wa *IFMS* kwa lengo la kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini;

ix) Kufanya ukaguzi wa shughuli za kiuhasibu pamoja na ukusanyaji wa mapato katika Wizara na Taasisi zote za Serikali;

x) Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa maofisa Mipango 24 wa Wizara zote, Mikoa na Wilaya zote kwa upande wa Pemba juu ya upangaji wa mipango na bajeti inayozingatia malengo ya *MKUZA* II;

xi) Kuratibu mafunzo kwa Kamati za Shehia 62 katika Mkoa wa Kusini Pemba kwa ajili ya uwekaji kumbukumbu za Shehia;

xii) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wote wa Ofisi kuu Pemba masuala ya Shughuli Mtambuka;

xiii) Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Ofisi ya Pemba inaombewa jumla ya TZS 825.075 milioni ili kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuandaa mazingira bora ya kazi na kuleta ufanisi na huduma bora katika kazi;

ii) Kufanya uhakiki wa mali za Serikali na kufanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara na Taasisi zote za Serikali zilizopo Pemba;

iii) Kusimamia na kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini kwa upande wa Pemba;

iv) Kuratibu utekelezaji wa miradi ya kitaifa Pemba na kusimamia utekelezaji wa mipango na bajeti za Wizara na Taasisi zake;

v) Kuratibu shughuli za rasilimali watu pamoja na kuimarisha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu na kuendeleza shughuli Mtambuka (*Cross Cutting Issues*);

vi) Kuendelea kuratibu upatikanaji wa nafasi zaidi za masomo kwa wafanyakazi wake katika ngazi na fani mbali mbali;

vii) Kushirikiana na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kuanza rasmi ujenzi wa Ofisi mpya Pemba;

viii) Kusimamia, kuendeleza na kudhibiti fedha za umma ikiwemo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na mali za serikali na taasisi zake pamoja na kutoa huduma za uhasibu na ukaguzi;

ix) Kuwapatia mafunzo na kuwaweka tayari watumiaji wapya wa mtandao wa *IFMs* kwa Wizara na Taasisi za Serikali, Ufuatiliaji na upatikanaji wa hati za Serikali (*Counterfoils*);

x) Kufuatilia uwekaji wa kumbukumbu katika madaftari ya Shehia kwa Wilaya zote. Kufanya mjadala na wadau juu ya umuhimu wa " *Vital*

registration“ na ukusanyaji wa takwimu zinazozingatia masuala ya idadi ya watu;

xi) Kuratibu mafunzo ya kushajihisha uingizaji wa masuala ya idadi ya watu katika mipango ya asasi za Serikali.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DAR ES SALAAM

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13 Idara iliidhinishiwa kutumia sh. 212.58 milioni kwa kazi za kawaida ambapo shughuli kubwa za Idara ni kutekeleza shughuli za Uratibu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na nje ya Tanzania. Mpaka mwisho wa mwezi Juni 2013 Idara ilishatumia jumla ya sh. 212.58 milioni, sawa na asilimia 100 ya makadirio. Katika kufanikisha malengo yake, Idara ilitekeleza yafuatayo:

i) Kuratibu na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa *Korea Institute for Development Strategy (KIDS*) kuhusiana na mpango mpya wa mafunzo ambao umeandaliwa na Taasisi hiyo kwa nchi tatu za Afrika ikiwemo Tanzania;

ii) Kushiriki katika ziara ya Mhe. Rais Jakaya M. Kikwete nchini Oman ambapo mikataba mbalimbali ilisainiwa ukiwemo mkataba wa Elimu ya juu uliosainiwa na Mhe.Waziri wa Elimu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii) Kushiriki katika mkutano wa Tume ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Kenya ambapo masuala ya kiuchumi, Utawala, Ulinzi na Jamii yalizungumziwa;

iv) Kuratibu mazungumzo baina ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Balozi za Rwanda na Wawakilishi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa China pamoja na Jumuiya ya wafanyabiashara wa Zanzibar, lengo likiwa ni kuzungumzia mashirikiano ya kukuza utalii baina ya nchi zetu;

v) Kushiriki katika warsha ilioyoandaliwa na Jumuiya ya Ulaya (*EU*) kuhusiana na upembuzi yakinifu na mapendekezo mengine kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa ufadhili wa Umoja wa Ulaya wa kuwepo kwa Ofisi ya Ofisa Mamlaka ya Taifa (*National Authorizing Officer - NAO*) ambaye ni kiunganishi kikuu baina ya Miradi na Washirika wa Maendeleo;

vi) Kushiriki kwenye kikao cha matayarisho ya mkutano wa Biashara ya huduma kwa nchi za *SADC*, ambapo kwa upande wa Zanzibar mkazo ni kuimarisha Sekta ya Utalii;

vii) Kushiriki vikao vya maandalizi ya mkutano wa watendaji wakuu, kuhusiana na Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

viii) Kuratibu upatikanaji wa nafasi za mafunzo na kushiriki katika vikao vya uteuzi ambapo wafanyakazi kumi na tano (15) kutoka Zanzibar walichaguliwa kujiunga na masomo katika fani na viwango mbali mbali kwa mwaka wa masomo 2013/2014 katika nchi za Algeria, Uingereza na China.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara inaombewa jumla ya sh. 326.97/= milioni ili kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kuratibu na kukuza ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na zile za Serikali ya Jamhuri ya Muungano;
ii) Kuratibu ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo baina ya SMZ na Ofisi za Balozi za nje na mashirika ya Maendeleo yaliyo na Ofisi zake Dar es Salaam;
iii) Kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kiuchumi na kijamii inayoandaliwa na SMT kwa faida ya Serikali;
iv) Kuratibu upatikanaji wa nafasi za mafunzo kutoka nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa.

TAASISI ZA FEDHA ZINAZOJITEGEMEA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inasimamia taasisi tisa (9) zinazojitegemea ambazo zinajumuisha Bodi ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar, Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, Shirika la Bima Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Benki ya Watu wa Zanzibar na Ofisi ya Mtakwimu MKuu wa serikali ambayo iko chini ya Tume ya Mipango.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi iliyopewa jukumu la kukusanya mapato ya ndani kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Kwa mwaka 2012/2013, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) ilipangiwa kukusanya jumla ya sh. 162,000.0/= milioni, ambapo mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2013, makusanyo halisi yalifika jumla ya sh. 141,708.0/= milioni sawa na asilimia 87 ya makadirio. Pamoja na kutofikia lengo, mapato kutoka ZRB yamekuwa kwa asilimia 17.6 ikilinganishwa na kiasi cha sh. 120,500/= milioni zilizokusanywa 2011/2012. Kwa mwaka 2012/1013 Bodi imeweza kufanya yafuatayo:-

i) Kusajili walipa kodi 687 wakiwemo 575 kwa ajili ya ushuru wa stempu, 34 kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani, 32 watembezaji wageni na 46 kwa ajili ya mikahawa na kodi za Hoteli;

ii) Kutoa elimu kwa walipa kodi kwa kuendesha semina nane (8), vipindi vya Redio na mikutano saba (7) juu ya umuhimu wa kutoa Stakabadhi wanapofanya mauzo;

iii) Kufanya mapitio ya idadi ya Hoteli na viwango vinavyotumika kutoza kodi kwa Hoteli mbali mbali ziliyopo Zanzibar na kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Sheria ya Ushuru wa Hoteli;

iv) Kuchukua hatua za kukabiliana na magendo ya mafuta kwa kutoa elimu kwa Jamii, kufanya mikutano ya wauzaji wa jumla na rejereja na kufanya zoezi maalum la kukamata mafuta ya magendo kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama ambapo lita 32,732 za diseli zilikamatwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Bodi ya Mapato imekadiria kukusanya jumla ya sh. 171,700.0/= milioni sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2012/2013. Ili kufikia lengo hili, *ZRB* imepanga kuchukua hatua zifuatazo:

i) Kutekeleza hatua mbali mbali na kuimarisha mapato kama zilivyotangazwa na Serikali;

ii) Kufanya ukaguzi kwa walipa kodi;

iii) Kuwaongezea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi 65 kwa kuwapatia mafunzo maalum katika utozaji kodi kwenye sekta za Utalii, simu, mawasiliano na mafuta;

iv) Kupitia mfumo wa mapato ya Mawizara;

v) Kuvipitia viwango mbalimbali vya kulipia kodi.

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato inaombewa ruzuku ya sh. 8,410.00/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ili kutekeleza majukumu yake. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15 kutoka ruzuku ya sh. 7,296/= milioni waliyopatiwa mwaka 2012 /2013.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) Ofisi ya Zanzibar ambayo jukumu lake kubwa ni kukusanya mapato ya Muungano kwa upande wa Zanzibar, ilipangiwa kukusanya jumla ya sh. 106,730.4/= milioni. Katika kufikia lengo hilo, Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa ilipangiwa kukusanya jumla ya sh. 67,077/= milioni sawa

na asilimia 63 ya lengo la mwaka na Idara ya Kodi za Ndani ilipangiwa kukusanya kiwango kilichobaki cha sh. 39,653.4/= milioni sawa na asilimia 37 ya lengo la mwaka.

Mhe. Naibu Spika, *TRA* Zanzibar ilimudu kukusanya sh. 103,865.69/= milioni sawa na asilimia 97 ya lengo. Utekelezaji huu unamaanisha ukuaji wa mapato kwa asilimia 13 kutoka sh. 91,666.4/= milioni zilizokusanywa mwaka 2011/2012. Kati ya Fedha zilizokusanywa, Idara ya Forodha iliweza kukusanya sh. 63,822.00/= milioni sawa na asilimia 95 ya lengo au asilimia 61 ya mapato yote yaliyokusanywa na *TRA* Ofisi ya Zanzibar. Idara ya Kodi za ndani imemudu kukusanya sh. 40,043.69/= milioni zaidi ya asilimia 100 ya lengo lake au asilimia 39 ya mapato yote yaliyokusanywa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) – Ofisi ya Zanzibar imepangiwa kukusanya sh. 147,900.00/= milioni sawa na ongezeko la asilimia 42.4 ya mapato halisi yaliyokusanywa kwa mwaka 2012/2013. Kati ya lengo hilo, Idara ya Forodha na Ushuru inatarajiwa kukusanya jumla ya sh. 98,792/= milioni sawa na asilimia 67 ya makadirio na Idara ya kodi za ndani inatarajiwa kukusanya sh. 49,107/= milioni sawa na asilimia 33 ya makadirio.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Mfuko wa Barabara ni kusimamia matengenezo ya barabara zetu. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/13 Mfuko wa Barabara ulilenga kupokea Ruzuku ya jumla ya sh. 5,868/= milioni kwa kazi za barabara na Uendeshaji wa Mfuko. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2013, jumla ya sh. 5,868.0/= millioni walishapokea, Ruzuku ambayo ni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/13 Mfuko ulipanga kutumia jumla ya sh. 6,320.0/= milioni kwa kazi ya matengenezo ya barabara na Uendeshaji wa Mfuko, ambapo mpaka kufikia Juni 30, 2013 jumla ya sh. 4,222.00/= milioni zilitumika sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matumizi hayo jumla ya sh. 3,520.00/= milioni zililipwa kwa kazi za barabara zikiwa ni asilimia 63 ya makadirio ya sh. 5,551/= milioni.

Vile vile, jumla ya sh. 702.00/= milioni zilitumika kwa kazi za Uendeshaji wa Mfuko zikiwa ni asilimia 91 ya makadirio ya sh. 769/= milioni. Aidha, kazi zenye thamani ya sh. 1,800.00/= millioni bado zinaendelea kutekelezwa na malipo yake yatafanyika mara kazi hizo zitakapokamilika.

Mhe Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/13 mfuko uliweza kukamilisha majukumu mbali mbali uliojipangia yakiwemo:

i) Ufungaji wa hesabu za mwaka 2011/12 na kukamilisha ukaguzi wa Fedha na Ufundi kwa mwaka 2011/12 kwa wakati uliopangwa;
ii) Kuandaa Ripoti ya mwaka 2011/12;
iii) Ununuzi wa gari ya ofisi kwa ajili ya ukaguzi wa kazi na majukumu mengine;
iv) Ununuzi wa generata la ofisi kwa matumizi ya dharura;
v) Kumpatia mafunzo ya shahada ya juu mfanyakazi mmoja pamoja na mafunzo ya cheti kwa mfanyakazi mwengine;
vi) Kuendesha semina tatu kwa wadau mbali mbali kuhusu kazi za Mfuko wa Barabara na majukumu ya Taasisi nyengine katika utunzaji wa barabara;
vii) Kutoa mafunzo ya usimamizi na utekelezaji wa kazi za matengenezo ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/14 Mfuko wa Barabara utaendelea na jukumu lake la kuweka utaratibu madhubuti wa utunzaji wa fedha zinazokusanywa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ya barabara pamoja na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ufanisi na kwa lengo lililokusudiwa. Kwa mwaka 2013/2014, Mfuko wa Barabara unaombewa Ruzuku ya jumla ya sh. 6,903/= milioni. Kati ya fedha hizo, sh. 6,046/= milion ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara na sh. 857.0/= milioni kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi.

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (*ZIPA*)

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kushajihisha wawekezaji wa nje na ndani kuekeza nchini pamoja na kuwasaidia wawekezaji kufikia malengo yao ya uwekezaji. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, *ZIPA* ilipangiwa kuwavutia wawekezaji miradi wapatao 38 katika sekta mbalimbali za kiuchumi, kijamii na viwanda.

Aidha *ZIPA* ilipanga kukusanya kutoka vyanzo vyake vya mapato jumla ya sh. 1,754.16/= milioni na kupatiwa ruzuku kutoka Serikalini ya sh 300.00/= milioni na kufanya jumla ya matumizi yao kufikia sh. 2,054.16/= milioni. Hadi kufikia Juni 2013, *ZIPA* imeweza kukusanya jumla ya sh. 1,058.97/= milioni sawa na asilimia 60.4 ya makadirio kutoka katika vyanzo vyake na kupatiwa asilimia 100 ya ruzuku yote iliyopangiwa na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka iliweza kukamilisha kazi zifuatazo:-

i) Miradi 30 iliidhinishwa yenye mtaji wa *USD* 335,428,485.67;

ii) Mamlaka imetangaza fursa za uwekezaji kwa kushiriki katika Mkutano wa Maonyesho ya Biashara nchini Korea na Mkutano wa *EPA* nchini Ubelgiji;

iii) *ZIPA* imeshiriki mikutano miwili ya Kanda nchini Msumbiji na Ethiopia. Mikutano mengine iliyoshiriki ni pamoja na nchi za Geneva, Oman, Kigali, Afrika ya Kusini na Dubai pamoja na mikutano ya ndani ya Dar Es Salaam na Arusha. *ZIPA* pia imeweza kujitangaza nchini China kupitia ziara ya Mhe.Rais wa Zanzibar;

iv) Kukamilisha ujenzi wa barabara kiwango cha lami kwa sehemu ya nje na sehemu ya ndani kiwango cha kifusi na kuweka taa za usalama kwenye eneo la Maruhubi;

v) Kuanza matayarisho ya Utayarishaji wa "*Master Plan"* ya eneo la Fumba;

vi) Kukamilisha michoro ya Ujenzi wa Ofisi ya *ZIPA* Pemba;

vii) Kuratibu shughuli zote za uwekezaji kwa upande wa Pemba ikiwepo ukaguzi wa miradi mipya na ya zamani iliyoekezwa Pemba;

viii) Wafanyakazi wanane (8) wameshiriki mafunzo ya muda mfupi, sita (6) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu kati yao watatu (3) wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya kwanza, wawili (2) shahada ya pili na mmoja (1) Stashahada.

Mhe. Naib Spika, kwa mwaka 2013/2014, *ZIPA* inakusudia kukusanya jumla ya sh. 1,622.79/= milioni kutoka katika vyanzo vyake vya ndani na kupatiwa ruzuku ya sh. 300.00/= milioni. Aidha *ZIPA* imekadiria kupata jumla ya sh. 2,295.39/= milioni kutoka kwa wawekezaji mbali kwa njia ya misaada ili kutimiza mahitaji ya sh. 3,918.18/= milioni kwa kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kawaida na Maendeleo. Katika hilo, Serikali imepanga kuipatia *ZIPA* jumla ya sh. 450.00/= milioni kwa ajili ya uendelezaji wa Maeneo Huru. Katika kukamilisha malengo yake, *ZIPA* imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya utafiti ili kutambua fursa mpya za uwekezaji na zilizopo, ifikapo mwisho wa mwaka 2013/2014;

ii) Kutoa huduma za upembuzi, uchambuzi na kuidhinisha miradi mipya;

iii) Kuimarisha Tovuti ya *ZIPA* kwa kuingizwa habari zilizopo na za kisasa za uwekezaji;

iv) Kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa njia mbali mbali zikiwemo kusambazwa vipeperushi;

v) Kufanya semina na midahalo ya mara kwa mara ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

vi) Kushiriki katika maonyesho ya biashara ya kikanda na kimikoa;

vii) Kukamilisha Mpango wa maendeleo ya Rasilimali watu pamoja na kuandaliwa mfumo wa kuvutia wafanyakazi kimaslahi ifikapo mwaka 2014;

viii) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya *ZIPA* kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA, CHWAKA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha (*ZIFA*) kina jukumu la kutoa mafunzo ya fani ya Fedha na zinazolingana, kuandaa semina za kiutawala na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani maalumu. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kiliweza kukusanya Mapato ya sh. 2,614.12/= milioni na kuweza kutumia Mapato hayo pamoja na Ruzuku ya sh. 1,641.0/= millioni iliyopatiwa na serikali na hatimae kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kukusanya jumla ya sh. 2,614.12/= milioni kutokana na ada za masomo, ruzuku na huduma nyengine na kutumia sh. 1,705.40/= milioni kwa kazi za Kawaida na sh. 908.74/= milioni kwa Kazi za Maendeleo;
ii) Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi walimu 24;
iii) Kuendelea kujenga mahusiano ya kiutendaji baina ya Chuo na "*Governing Bodies*" (*NACTE*), *NBAA*, *TCU* na *AUA* zinazohusiana na masuala ya elimu;
iv) Kuratibu mitihani yote ya wanafunzi katika mihula miwili ya mwaka wa masomo 2012/2013 ambapo jumla ya wanafunzi 1,214 walitahiniwa;
v) Kufanya manunuzi ya vifaa vya kufundishia na ofisini vikiwemo viti, meza, mbao za kuandikia na vitabu vya fani mbali mbali;
vi) Kuwapatia fursa za masomo walimu sita katika Shahada ya Uzamivu (*PhD*) kati yao wanne wanaendelea na wawili wanatarajiwa kurudi masomoni mwaka huu wa fedha;
vii) Kumuwezesha mwalimu mmoja kwenda katika masomo ya Shahada ya Uzamili (*Masters*) na wafanyakazi watatu wa kada ya utawala kwenda masomo ya muda mrefu , mwalimu mmoja kufanya mitihani ya bodi ya *CPA* (T) na wafanyakazi watano (5) wasiokuwa walimu kushiriki katika mafuzo mafupi katika fani za udereva na mafunzo ya masjala;
viii) Kusajili na kusomesha wanafunzi 1,256 katika fani na ngazi mbali mbali;
ix) Kutoa ushauri elekezi kwa Taasisi za Serikali katika kuandaa Mpango Mkakati, Kanuni za Utumishi na Kanuni za Fedha, kufunga mahesabu na kadhalika;
x) Kuanzisha na kuimarisha Kituo cha Ujasiriamali (*Incubation Centre*) kwa kuandaa Mpango Mkakati wa kituo hicho pamoja na kuimarisha shughuli za utafiti na kituo cha utafiti na uchapishaji;
xi) Kujenga ukuta wa dakhalia mpya pomoja na kutengeneza viwanja vya michezo.

Mhe.Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Chuo kimekadiria kukusanya jumla ya sh. 2,675.87/= milioni kutokana na ada na huduma inazozitoa na mkopo kutoka *ZSSF* wa sh. 800.00/= milioni. Aidha Chuo kinaombewa ruzuku ya sh. 1,800.00/= milioni kwa kazi za kawaida na sh. 200.00/= milioni kwa Kazi za Maendeleo. Mambo yaliyopangwa kutekelezwa na Chuo ni haya yafuatayo:-

i) Kufanya mapitio ya mitaala katika fani za Stashahada ya Uongozi wa Fedha-Uhasibu, Stashahada ya Ununuzi na Ugavi na Stashahada ya TEHAMA;

ii) Kuongeza idadi ya programu, ambapo mwaka huu stashahada ya uzamili ya usimamizi wa Fedha itaanzishwa;

iii) Kufanya mapitio ya programu (*Self -Review Study*) ili kuwa na ithibati endelevu;

iv) Kufanya manunuzi ya vifaa vya kisasa vya kufundishia, manunuzi ya vitabu vya kiada na ziada (500) na Basi la Wafanyakazi;

v) Kuwapeleka wafanyakazi kumi na mbili (12) mafunzo mafupi na ya kitaalamu pamoja na walimu thalathini na nne (34) kwenye mafunzo mafupi na ya kitaalamu ikiwemo mafunzo ya njia na mbinu bora za kufundishia, TEHAMA na utafiti;

vi) Kusajili wanafunzi wapya 830, ngazi ya Cheti, *Diploma*, Shahada ya kwanza na Stashahada ya Uzamili na hatimae kufundisha na kuwatahini wanafunzi 1,400 katika fani mbali mbali;

vii) Kuandaa na kufanya mahafali ya kumi (10) ya chuo ambayo wanafunzi 550 wanatarajia kuhitimu;

viii) Kuendeleza wafanyakazi wanne wa kada ya utawala kwenye mafunzo ya muda mrefu (watatu wanaendelea na mmoja mpya);

ix) Kuwawezesha walimu sita katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) wanne (4) wanaendelea na wawili (2) wapya pamoja na mwalimu mmoja katika mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili;

x) Kuchangia shughuli za Maendeleo kwa wanajamii ikiwemo kununua vitabu vya kusaidia shughuli za kitaaluma Skuli za Chwaka na kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa wadau wa Chwaka na maeneo ya karibu;

xi) Kuendesha mafunzo sita (6) ya kuongeza uwezo wa utendaji na mihadhara miwili (2) ya kitaalamu;

xii) Kufanya tafiti mbili (2) za kitaifa juu ya bajeti na fedha (*Finance and Budgeting*) pamoja na mabadiliko ya zao la mwani kibiashara (*commercialization of seaweed*);

xiii) Kuimarisha kituo cha kuwalea wajasiriamali (*Incubation Centre*) pamoja na kutoa Ushauri wa Kitaalamu katika Taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi;

xiv) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Chuo, Kanuni za Fedha na Sheria ya Chuo;

xv) Kujenga jengo jipya la ghorofa tano kwa ajili ya Maabara ya Kompyuta, madarasa na ofisi ambapo kwa mwaka huu wa fedha ghorofa mbili zinatarajiwa kumalizika;

xvi) Kuwawezesha wafanyakazi wawili kushiriki kwenye mafunzo mafupi na ya kitaalamu katika fani za Katibu muhtasi na usimanizi wa ofisi;

xvii) Kufanya matengenezo ya zahanati ya chuo na ununuzi wa vifaa vyake.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, shirika hili lina jukumu la kutoa huduma za Bima kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika lilikadiria kukusanya mapato kutokana na ada za Bima ya sh. 11,747.00/= milioni ambapo mpaka kufikia mwezi Disemba 2012, Shirika limeweza kukusanya jumla ya sh. 10,516.00/= milioni sawa na asilimia 90 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya sh. 3,391.00/= milioni kwa kazi za kawaida na sh. 1,000.0/= milioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Disemba 2012 Shirika liliweza kutumia jumla ya sh. 3,291/= milioni kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 97 na sh. 636.00/= milioni kwa shughuli za Maendeleo, sawa na asilimia 64. Mbali ya fedha za Uendeshaji, Shirika limetumia jumla ya sh. 4,075/= milioni kuwalipa wateja wa Bima waliopata ajali.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2013 hadi kufikia Disemba linakadiria kukusanya jumla ya sh. 12,370/= milioni kutokana na vianzio vyake mbali mbali vya mapato. Makadirio haya ya mapato ni zaidi ya mapato halisi ya mwaka 2012 uliopita kwa asilimia 18. Aidha, Shirika linatarajiwa kutumia jumla ya sh. 3,854/= milioni kwa kazi za kawaida na sh. 692.0/= milioni kwa kazi za Maendeleo. Kutokana na hali ya ushindani wa kibiashara kwa mwaka 2013 Shirika limejiwekea kutekeleza yafuatayo:

i) Kutumia asilimia 43 ya fedha za kazi za Maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi (magari) kwa ajili ya Kanda zilizoko Tanzania Bara;

ii) Kutoa huduma bora na za kisasa kwa wateja wake kwa kuwafatilia baada ya kupatiwa huduma na kueleza matatizo yao na kulipa madai kwa wakati;

iii) Kuongeza mapato kwa asilimia 18 kwa mwaka;

iv) Kukuza mtaji wa kutoa gawio kwa Serikali ambayo ndiyo mmiliki pekee;
v) Kuongeza wafanyakazi watano (5) wenye ujuzi na uzoefu wa kufanya kazi;
vi) Kukuza mtaji katika uwekezaji wa dhamana za Serikali na hisa;
vii) Kufanya matumizi kwa kiwango kisichozidi asilimia 20 ya mapato;
viii) Kujihusisha zaidi katika masuala ya kijamii ikiwemo utoaji wa misaada kwa vikundi vidogo vidogo na utoaji wa vyandarua katika Hospitali mbali mbali;
ix) Kuongeza kiwango cha soko kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 5 ifikapo 2015 ambapo kwa mwaka 2013/2014 kilifikia asilimia 4.7.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (*ZSSF*)

Mhe.Naibu Spika, jukumu kubwa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ni kukusanya michango ya wafanyakazi na kuwekeza katika miradi yenye tija na hatimae kutoa mafao kwa wanachama pale tu muda unapofikia kama Sheria ya Mfuko inavyoagiza. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mfuko umetekeleza kazi zifuatazo:

i) Kusajili waajiri 73 dhidi ya lengo la kusajili waajiri 85 hii ni sawa na asilimia 86. Wanachama waajiriwa waliosajiliwa ni 3,405 sawa na asilimia 85 ya lengo la kusajili waajiriwa 4,000;
ii) Kulipa mafao yenye jumla ya sh. 6,524/= milioni sawa na asilimia 112 ya lengo lililoekwa la kulipa jumla ya sh. 5,853/= milioni;
iii) Kukusanya michango ya wanachama yenye jumla ya sh. 24,756/= milioni dhidi ya lengo la kukusanya sh. 24,858/= milioni sawa na asilimia 99.6;
iv) Kuanza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru (Kariakoo) na kuanza matayarisho ya ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Umoja (Tibirinzi).

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mfuko unatarajia kufanya kazi zifuatazo:-

i) Kuongeza wigo wa kusajili wanachama kwa kutumia Mfumo wa uchangiaji wa hiari (*Zanzibar Voluntary Social Security Scheme*) pamoja na kuimarisha ukaguzi wa Taasisi mbali mbali za binafsi;
ii) Kufanya mageuzi ili kuufanya Mfuko uwe endelevu kwa kukamilisha zoezi la mageuzi ya Sheria ya Mfuko;
iii) Kuwekeza jumla ya sh. 39,000/= milioni katika maeneo ya muda mrefu na yale ya muda mfupi, zikiwemo dhamana za serikali, hati fungani za serikali, hesabu za muda maalum, ununuzi wa hisa pamoja

na mikopo. Jumla ya sh. 18,200/= milioni zinategemewa kukusanywa kama mapato ya uwekezaji;

iv) Kukamilisha ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru (Kariakoo) pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Umoja (Tibirinzi);

v) Kuendelea na ujenzi wa kumbi za mikutano, nyumba za kisasa na jengo la biashara huko Mbweni;

vi) Kuwapeleka wafanyakazi 20 masomoni, kati ya hao wafanyakazi saba (7) kwa mafunzo ya muda mrefu na 13 kwa muda mfupi katika fani za Uhasibu, Ununuzi na Ugavi, TEHAMA na usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza kazi hizo, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mfuko umetenga jumla ya sh. 13,500.00/= milioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji, kati ya hizo sh. 7,000.00/= milioni kwa kuendeleza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru kwa Unguja sh. 4,000/= milioni kwa kuanza ujenzi wa kiwanja cha Umoja kwa Pemba na sh. 2,500/= milioni kwa mradi wa ujenzi wa kiwanja cha Mbweni. Aidha, Mfuko umepanga kutumia TZS 3,216 milioni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Mhe. Naibu Spika, jukumu kubwa la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni kupokea amana za wateja wake na kukopesha kwa wanaohitaji pamoja na kuwapatia wateja huduma mbalimbali za kibenki. Kwa mwaka 2012 Benki imetekeleza yafuatayo:

i) Kupokea amana za wateja zenye kiwango cha TZS 212,937.00 milioni ikiwa ni asilimia 96 ya lengo lililowekwa la TZS 220,191.11 milioni.

ii) Kutoa mkopo wa jumla ya TZS 109,424.16 milioni sawa na asilimia 112 ya lengo lililowekwa la TZS 97,265.11 milioni kwa mwaka.

iii) Kuongeza kiwango cha rasilimali ya Benki kufikia TZS 247,838.00 milioni ikilinganishwa na lengo la TZS 252,691.62 milioni.

iv) Kukusanya mapato ya TZS 21,667.17 milioni yanayotokana na huduma mbalimbali za kibenki ambayo ni sawa na asilimia 104 ikilinganishwa na makadirio ya TZS 20,983.88 milioni.

v) Kuanzisha uhusiano na Benki ya Viwanda na Biashara ya China "*Industrial and Commercial Bank* ya China" (ICBC) kwa nia ya kurahisisha biashara kati ya pande hizi mbili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya Benki ya Kiislamu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013, Benki imeweza kujipatia wateja 26,588 wenye amana zinazofikia jumla ya TZS 25,592.56 milioni. Kwa upande wa mikopo inayofuata misingi ya shariah za kiislamu, benki imeshatoa mikopo yenye thamani ya jumla ya TZS 8,191.00 milioni, ambapo wakopaji ni wafanyakazi wa Serikali, taasisi za Serikali na mashirika binafsi.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Benki imeweza kuanzisha njia mpya ya kuwafikia wateja kupitia mtandao wa simu na mtandao wa *Internet (PBZ Mobile Banking* na *PBZ Online Banking)* pamoja na kufungua vituo vya huduma za Benki huko Makunduchi na Mazizini kwa upande wa Unguja na Wete na Mkoani kwa Pemba. Benki tayari imeshatengeneza sera ya mikopo ya nyumba pamoja na sera ya mikopo ya wateja wadogo wadogo na wateja wa kati.

Mhe. Naibu Spika, katika kujiimarisha zaidi, Benki imejiunga na huduma ya kusafirisha fedha ya *(World Remit)* ambayo inarahisisha usafirishaji fedha kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Tanzania Diaspora). Huduma hii itarahisisha na kuweka mfumo wa kuaminika zaidi kwa usafirishaji Fedha kati ya Watanzania wanaoishi nje na ndugu zao wanaoishi Zanzibar na Tanzania bara.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, PBZ imekusudia kutekeleza yafuatayo:

i) Kuendeleza majukumu yake makuu ya kukusanya amana TZS 262,182 milioni hadi kufikia Disemba 2013 za wateja na kutoa mikopo TZS 119,370 milioni hadi kufikia Disemba 2013,

ii) Kuongeza mapato ya TZS 24,958 milioni yanayotokana na vianzio mbalimbali;

iii) Kuzindua tawi la Benki ya Kiislamu ya PBZ, katika jengo la BIMA lililoko mtaa wa Mpirani Unguja;

iv) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ambalo litaendana na hadhi ya Benki ya Watu wa Zanzibar Ltd;

v) Kueneza huduma za ATM katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ikiwemo Tunguu (SUZA), Michenzani (Majenzi) na Bandarini Malindi;

vi) Kufungua matawi mengine zaidi Tanzania Bara katika mikoa ya Mtwara na Mwanza baada ya kukamilika utafiti juu ya mahitaji ya huduma za kibenki katika maeneo hayo;

vii) Kuanzisha vituo vya huduma za kibenki Kaskazini Unguja na Dar es Salaam;

viii) Kujiunga na mitandao ya *VISA* na *Master Card* ambayo itawawezesha wateja wa Benki ya Watu wa Zanzibar kupata huduma za kibenki popote pale duniani na pia Benki kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wageni wanaokuja Zanzibar.

MAMBO YALIYOJITOKEZA KATIKA KIKAO HIKI CHA BARAZA

Mhe. Naibu Spika, katika mijadala ya mapendekezo ya bajeti za Wizara na Taasisi mbalimbali, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza walihoji mambo kadhaa ambayo baadhi yao yaliweza kupatiwa majibu. Hata hivyo kuna mambo machache ambayo walihitaji maelezo zaidi likiwemo suala la utekelezaji wa mradi wa "*E–government*". Naomba nitumie fursa hii na mimi kutoa maelezo machache ya ziada.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi dhamira ya serikali ya kuimarisha matumizi ya Teknohama Serikali ipo siku nyingi ambapo chimbuko la Mradi wa sasa wa "*E-government*" ni Mradi wa Usajili wa Wazanzibar Wakaazi. Mandalizi ya mradi huu yalibainisha haja ya kuimarisha na kuunganisha matumizi ya Teknohama serikalini kwa upana mkubwa zaidi. Maeneo yaliyobainishwa katika waraka wa Mradi wa mwaka 2004 ni pamoja na Daftari Kuu *(Core Registry)* na Madaftari (*Registries*) zinazohusisha masuala ya utambulisho wa Ardhi na Makaazi. Wakaazi wa Manispaa, Wanafunzi, Wasimamizi wa mipaka, Bandarini na Viwanja vya Ndege, Leseni za udereva, Daftari la wapiga Kura na Huduma za Afya. Kama lilivyo, hili ni suala pana sana na linahitaji kujengwa kwa awamu.
Mhe. Naibu Spika, mradi uliotekelezwa na unaotakiwa kutolewa maelezo umehusisha maeneo makubwa matano ambayo ni:

i) Miundo mbinu *(fibre optic)*
ii) *"Intranet na Internent*"
iii) Maeneo ya matumizi *(Application and Potray)*

iv) Elimu
v) Masuala ya Usalama (*Security*).

Mhe. Naibu Spika, mradi ulikadiriwa na hatimae kuidhinishiwa jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 20 (USD 20.00 milioni) ambazo zilipatikana kama mkopo nafuu kutoka Serikali ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim ya China. Kampuni ya *ZTE Corporation* ya China ndio iliyopendekezwa na hatimae kuhusika na ujenzi wa miundombinu hiyo. Kimsingi maeneo makuu yaliyotekelezwa na mradi ni pamoja na haya yafuatayo:

i) Uwekaji wa mkonge wa *fibre optic* Unguja na Pemba ambapo jumla ya kilomita 352 zikiwemo (266 kwa Unguja na 86 kwa Pemba) zilihusika pamoja na ununuzi wa vifaa vyake;

ii) Ujenzi wa jengo lililopo Mazizini na uwekaji vifaa katika kituo hicho cha taarifa *(Data Center)* ikiwemo *"hard ware"* Software na basic applications" masuala ya mtandao na usalama wa kituo. Kituo hiki kimeimarishwa kwa kuwekewa:

- Mitambo ya usalama kwenye milango yake,
- Vifaa vya kutambua ishara za moto *(Fire Alert and Smoke detector),*
- Vifaa vya kuzimia moto vya *automatic,*
- Mitambo ya mawasiliano ya *CCTV,*
- Uzio wa umeme *(Elecrtic fence),*

iii) Mafunzo kwa timu ya TEHAMA

iv) Ujenzi wa minara miwili ya Microwave Unguja na Pemba

v) Kununua transforma mbili (2) kwa kuhudumia minara na *towers*

vi) Kununua standby generators (13) kwa kuhudumia viunganisho vya waya *(pops)*

vii) Kununua standby generator moja (1) kwa ajili ya kitua cha mashine *(Data Center).*

Mhe. Naibu Spika, juu ya kwamba gharama zinaelezwa kuwa ni kubwa, kiasi hicho cha gharama kimefikiwa baada ya kupunguzwa upeo wa mradi kwa kuondoa uwekaji wa mkonga chini ya bahari baina ya Unguja na Pemba. Makisio yaliyowasilishwa awali ni Dola za Kimarekeni Milioni 36 kwa Kampuni ya Huawei na Dola 33 milioni kwa kampuni ya ZTE ambayo ilibarikiwa.

Mhe. Naibu Spika, wakati mradi ukitekelezwa, kumefanyika pia mazungumzo na kampuni ya Zantel kwa ajili ya ubia katika uwekezaji na uendeshaji. Chini ya makubaliano yaliyofikiwa, Zantel inatarajiwa kuwekeza kwa kuunganisha ofisi zote za Serikali kwa kumalizia *(Last mile)* na mkonga *(Fibre optic)* na hivyo kuleta ufanisi zaidi kuliko njia ya *"Wireless"* iliokusudiwa kutumika hapo awali. Kwa bahati mbaya mazungumzo na Zantel yalichukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri kuanza rasmi kunufaika na mtandao huo zikiwemo ufanisi katika mawasiliano na kupata huduma za Internet bila ya malipo kwa Serikali yote.

Mkataba wa Zantel umetiwa saini tokea mwezi Febuari mwaka huu na kwa sasa matayarisho ya mwisho ya utekelezaji yamekamilika. Kukamilika kwa uwekezaji wa Zantel kutaunganisha visiwa vya Unguja na Pemba kwa njia ya kupitia mikonga ya umeme (Dar-Unguja na Pemba-Tanga).

Mhe. Naibu Spika, natumai baada ya maelezo hayo sasa Waheshimiwa Wajumbe wamepata, japo kwa muhtasari maelezo ya mradi huo. Nia ya serikali ni kuendelea na kuimarisha maeneo mengine ya TEHAMA kama vile katika kuimarisha huduma za afya, usimamizi wa mapato na mengineyo.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kukupongeza tena jinsi ulivyo endesha kikao hichi na kuendelea kulijengea heshima Baraza letu hili ambalo ni nguzo muhimu kwa ustawi wa Zanzibar na Wazanzibari. Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kufanikisha kazi zetu hadi leo hii tunakaribia kukamilisha kikao hichi cha Bajeti kwa kumalizia na Ofisi hii ambayo ndio moyo wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kufikia hatua hii leo, ni dhahiri kuwa tumekuwa na safari ndefu sana. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa wajumbe wataidhinisha mapendekezo ya Bajeti kwa ofisi yangu bila ya vikwazo. Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima kwa mwaka wa fedha wa 2013/14, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya TZS 409,892.4 milioni na matumizi ya jumla ya TZS 160,773.20 milioni kati yake ikiwa TZS 44,794.00 milioni ni kwa kazi za kawaida, (zikiwemo TZS 28,695.00 milioni kwa matumizi ya Idara zake Kiambatisho VII) na TZS 42,438.40 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Fedha hizi ni kukidhi pia matumizi ya Tume ya Mipango ya Zanzibar ya TZS 2,564 millioni kwa kazi za kawaida na TZS 4911.80 millioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, ofisi inaomba iidhinishiwe jumla ya TZS 66,065.00 milioni kwa matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali kama uchambuzi unavyoonesha hapo chini.

MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

VOTE 19	(OR) FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO	TZS Bilioni
I	**Matumizi ya Kawaida**	**44,794.00**
	Mishahara	3,414.00
	Matumizi mengineyo (O/C)	6,517.00
	Ruzuku kwa Taasisi	17,363.00
	Marekebisho ya Mishahara	17,500.00
II	**Matumizi ya Kazi za Maendeleo**	**42,438.40**
	Mchango wa Serikali	7,950.00
	Ruzuku na Mikopo	17,488.40
	Ununuzi wa Meli mpya ya abiria	17,000.00
VOTE 49	**TUME YA MIPANGO**	
III	**Matumizi ya Kawaida**	**2,564.00**
	Mishahara	866.50
	Matumizi mengineyo (O/C)	397.50
	Ruzuku kwa Taasisi (OCGS)	1,300.00
	Matumizi ya Maendeleo	**4,911.80**
	Mchango wa Serikali	985.00
	Ruzuku na Mikopo kutoka Nje	3, 926.80
VOTE 45	**MFUKO MKUU WA SERIKALI**	
IV	**Gharama za Mfuko Mkuu wa Serikali**	**66,065.00**
	JUMLA KUU (VOTES 19, 49 na 45)	**160,773.20**

Mhe. Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajet iliyopita pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya mwaka 2013/2014 pamoja na muhtasari wa maelezo mengine unaonekana katika viambatisho ambavyo tumeviweka.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hotuba hiyo naomba kuwasilisha muhtasari wa maelezo ya bajeti inayozingatia program maalum ya *program basic budget* ya Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kiambatisho Nam. I

UKUSANYAJI WA MAPATO KUTOKA VIANZIO VYA NDANI

S/N	CHANZO	MAKADIRIO KWA MWAKA 12/13	MAKUSANYO HALISI KWA MWAKA 2012/2013	MAKADIRIO KWA MWAKA 2013/2014
1	Ukodishwaji wa mashamba ya Mpira	140,000,000	79,072,000	145,000,000
2	Uuzwaji wa Risiti	23,000	29,020,026	28,000,000
3	Ukodishwaji wa Hoteli ya Afrika House	96,000,000	100,520,341.73	100,000,000
4	Uuzaji Vifaa Chakavu	36,000,000	41,420,500	42,993,000
5	Mapato kutokana na Uhamiaji	3,419,000,000	3,319,303,664.21	3,870,000,000
6	Ukodishwaji wa matangi ya Mafuta	218,400,000	211,952,400	221,000,000
7	Mapato Mengineyo	40,000,000	44,007,932.56	45,000,000
8	Uvuvi wa Chini ya Bahari	100,000,000	96,605,641	
9	Malipo ya Mkonga wa Taifa	0	0	1,440,000,000
	JUMLA	**4,049,423,000**	**3,921,902,506**	**5,891,993,000**

Kiambatanisho Nam. II

MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2012/2013				
KASMA	**IDARA**	**MAKADIRIO 2012/13**	**MATUMIZI HALISI**	**UFANISI %**
03	AFISI KUU PEMBA	663,481,789	663,481,789	100%
04	MPANGO SERA NA UTAFITI	134,191,600	134,191,600	100%
07	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	2,371,204,314	2,371,204,314	100%
08	URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ-DSM	212,587,150	212,587,150	100%
09	FEDHA ZA NJE	120,452,964	120,452,964	100%
10	MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI	115,315,900	115,315,900	100%
11	MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI	225,906,800	225,906,800	100%
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	287,202,276	287,202,096	100%
19	UENDESHAJI NA UTUMISHI	16,127,819,952	16,127,494,741	100%
21	UKUZAJI UCHUMI	288,018,111	288,018,111	100%
22	BAJETI	426,452,217	426,452,216	100%
	RUZUKU	16,276,374,502	16,276,374,502	100%
JUMLA		**37,249,007,575**	**37,248,682,183**	**100%**

KIAMBATISHO III

ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2012/2013									
AFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO TZS '000'									
JINA LA MRADI	**MAKISIO KWA MWAKA 2012/2013**			**MATUMIZI HALISI**					
	SMZ	**MUHISANI**		JUMLA	**SMZ**	%	**MUHISANI**	**%**	**JUMLA**
Programu za kuimarisha Uwezo - ORFUMM									
I. Kuijengea uwezo OR-FUMM		-							
II. Kuanada Moduli za Bajeti		-							
III. E-Government		-							
Programu ya changamoto ya Millenia (MCA - T)	260,000	-	-	260,000	28,183	11%	-		28,183
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)		World Bank	500,000						
Programu ya									

UNDAP									
I. Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini yenye kuleta Matokeo ya MKUZA II	50,000	UNDP	862,400	912,400	15,211	30%	15,905	2%	31,116
II. Pro-poor Growth Zanzibar	40,000	UNDP	548,800	588,800	0	0%	-	0%	-
III. Kujenga Uwezo kwa Taasii za Serikali	20,000	ICAP/CDC/CHAI/GF	392,000	412,000	0	0%	-	0%	-
IV. Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar	5,000	UNDP	867,400	**872,400**	4,101	82%	95,262	11%	**99,363**
V. Kuimarisha jitihada za kupunguza umasikini				**0**					-
Uratibu wa Uimarishaji Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST)	15,000	World Bank	-	**15,000**	3520	23%	22,396		**25,916**
Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar	5,800,000			**5,800,000**	3,133,918	54%			**3,133,918**

I. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko									-
II. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano									-
III. OR-Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo									-
IV. Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake									
V. Wizara ya Katiba na Sheria									
VI. Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora									
Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	50,000	World Bank	19,954,691	**20,004,691**	35,834	72%	2,429,214	12%	**2,465,048**
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)	40,000	Norway	2,487,338	**2,527,338**	38,481	96%	24,412	1%	**62,893**

Programu ya Mpango wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)		URT	392,000	**392,000**	0		85,098	22%	**85,098**
MIRADI				**0**					-
Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka (Maabara ya Computer na madarasa	500,000			**500,000**	221,340	44%			**221,340**
Ujenzi wa ukuta wa Dahalia	250,000			**250,000**	0	0%			-
Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto	20,000	UNICEF		**20,000**	18,780	94%			**18,780**
Uimarishaji wa Takwimu	300,000	ICAP		**300,000**	138,021	46%	1,399,017		**1,537,038**
ZANSTAT	100,000		400,000	**500,000**	0	0%	21,550	5%	**21,550**

Kuoanisha masuala ya idadi ya watu katika afya ya uzazi, jinsia na kupunguza umasikini	20,000	ICAP		**20,000**	15,869	79%	43,604		**59,473**
Mradi wa utafiti wa watendakazi	150,000	EAC	1,247,743	**1,397,743**	150,000	100 %	117,857	9%	**267,857**
Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili	5,000	AFDB	509,600	**514,600**	5,000	100 %	295,392	58%	**300,392**
Mradi wa kufanya tathmini ya mali zaSerikali	200,000			**200,000**	200,000	100 %			**200,000**
Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba	150,000			**150,000**	150,000	100 %			**150,000**
Kuifanyia mabadiliko na kuimarisha Tume ya Mipango	100,000	-	-	**100,000**	7,479	7%	-		**7,479**
Mradi wa mashirikiano ya sekta za umma na ubinafsi	150,000	-	-	**150,000**	22,828	15%	-		**22,828**
Mradi wa kujenga uwezo wa Takwimu (STATCAP)	100,000			**100,000**	13,567	14%	146,004		**159,571**

JUMLA	**8,325,000**		**28,161,972**	**35,986,972**	**4,202,132**	**50%**	**4,695,711**	**17%**	**8,897,843**
UNUNUZI WA MELI	**17,000,000**			**17,000,000**					

Kiambatanisho IV

MATUMIZI YA FEDHA ZA SMZ KWA KAZI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

KASMA	IDARA	MAKADIRIO 2012/13	MATUMIZI HALISI	UFANISI (%)
07	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	40,000,000	38,481,266	96%
04	MIPANGO, SERA NA UTAFITI	50,000,000	35,834,100	72%
09	FEDHA ZA NJE	10,000,000	9,100,546	91%
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	6,000,000,000	3,333,918,853	56%
10	MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI	190,000,000	184,649,000.00	97%
11	MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI	485,000,000	54,393,000	11%
	BAJETI	1,400,000,000	522,929,271	37%
21	UKUZAJI UCHUMI	150,000,000	22,828,180	15%
JUMLA		**8,325,000,000**	**4,202,134,216**	50%

Kiambatanisho Nam. V

PROGRAMU/MRADI	MCHANGO WA SERIKALI	MATUMIZI HALISI 2012-2013
PROGRAMU		
Programu za kuimarisha Uwezo - ORFUMM		-
I. Kuijengea uwezo OR-FUMM		
II. Kuanada Moduli za Bajeti		
III. E-Government		
Programu ya changamoto ya Millenia (MCA - T)	260,000	28,183
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)		
Programu ya UNDAP		
I. Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini yenye kuleta Matokeo ya MKUZA II	50,000	15,211
II. Pro-poor Growth Zanzibar	40,000	-
III. Kujenga Uwezo kwa Taasii za Serikali	20,000	
IV. Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar	5,000	4,100
V. Kuimarisha jitihada za kupunguza umasikini		

Uratibu wa Uimarishaji Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST)	15,000	3,520
Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar	5,800,000	3,133,918
I. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko		
II. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano		
III. OR-Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo		
IV. Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake		
V. Wizara ya Katiba na Sheria		
VI. Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora		
Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	50,000	35,834
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)	40,000	38,481
Programu ya Mpango wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)		-
Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka (Maabara ya Computer na madarasa	500,000	221,340
Ujenzi wa ukuta wa Dahalia	250,000	0
Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto	20,000	18,780

Uimarishaji wa Takwimu	300,000	138,021
ZANSTAT	100,000	0
Kuoanisha masuala ya idadi ya watu katika afya ya uzazi, jinsia na kupunguza umasikini	20,000	15,869
Mradi wa utafiti wa watendakazi	150,000	150,000
Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili	5,000	5,000
Mradi wa kufanya tathmini ya mali zaSerikali	200,000	200,000
Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba	150,000	150,000
Kuifanyia mabadiliko na kuimarisha Tume ya Mipango	100,000	7,479
Mradi wa mashirikiano ya sekta za umma na ubinafsi	150,000	22,828
Statistic Capaity Building Project (STATCAP)	100,000	13,567
JUMLA	**8 ,325,000**	**4,202,131**

Kiambatanisho Nam. VI

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014			
KASMA	**DEPARTMENT**	**MAKISIO YA MWAKA 2012/2013**	**MAKISIO YA MWAKA 2013/2014**
3	AFISI KUU PEMBA	962,751,000	825,075,000
4	MPANGO SERA NA UTAFITI	404,731,000	285,297,000
7	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	2,782,587,000	3,183,570,000
8	URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ-DSM	258,275,000	326,970,000
9	FEDHA ZA NJE	206,688,000	173,868,000
10	MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI	188,466,000	149,104,000
11	MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI	397,354,000	688,200,000
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	359,012,000	502,750,000
19	UENDESHAJI NA UTUMISHI	11,246,720,000	3,962,349,000
21	UKUZAJI UCHUMI	335,578,000	426,696,000
22	BAJETI	543,838,000	671,121,000
	MAREKEBISHO YA MSHAHARA	5,010,000,000	17,500,000,000
	RUZUKU	16,888,000,000	18,663,000,000
JUMLA		**39,584,000,000**	**47,358,000,000**

Kiambatanisho Nam. VII

ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA OFISI KWA MWAKA 2013/2014						
OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO TZS "000"						
JINA LA MRADI	**MCHANGO WA SERIKALI**		**MCHANGO WA WAHISANI**			**JUMLA YA BAJETI**
	MAKISIO YA MWAKA 2012/2013	**MAKISIO YA MWAKA 2013/2014**	**WAHISANI**	**RUZUKU**	**MKOPO**	
1	**2**	**3**	**4**	**5**	**6**	**3+5+6**
Programu za kuimarisha Uwezo - ORFUMM						
I. Kuijengea uwezo OR-FUMM		0	-			-
II. Kuanada Moduli za Bajeti		0	-			-
III. E-Government		0	-			-
Programu ya changamoto ya Millenia (MCA - T)	260,000	50,000	-			50,000
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)		0	World Bank	500,000		500,000

Programu ya UNDAP						-
I. Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini yenye kuleta Matokeo ya MKUZA II	50,000	50,000	UNDP	700,000		750,000
II. Pro-poor Growth Zanzibar	40,000		UNDP			-
III. Kujenga Uwezo kwa Taasii za Serikali	20,000	15,000	ICAP/CDC/CHAI/GF	900,000		915,000
IV. Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar	5,000	5,000	UNDP	700,000		705,000
V. Kuimarisha jitihada za kupunguza umasikini						-
Uratibu wa Uimarishaji Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST)	15,000					-
Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar	5,800,000	7,000,000				7,000,000
I. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko						-
II. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano						-
III. OR-Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo						-

IV. Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake						-
V. Wizara ya Katiba na Sheria						-
VI. Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora						-
Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	50,000	50,000	World Bank		15,200,000	15,250,000
Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM)	40,000	40,000	Norway			40,000
Programu ya Mpango wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)			URT	262,800		262,800
MIRADI						-
Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka (Maabara ya Computer na madarasa	500,000	200,000				200,000
Ujenzi wa ukuta wa Dahalia	250,000					-
Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto	20,000	20,000	UNICEFF	32,000		52,000
Uimarishaji wa Takwimu	300,000	250,000	ICAP	32,000		282,000

ZANSTAT	100,000					-
Kuoanisha masuala ya idadi ya watu katika afya ya uzazi, jinsia na kupunguza umasikini	20,000	140,000	ICAP			140,000
Mradi wa utafiti wa watendakazi	150,000	150,000	EAC			150,000
Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili	5,000	5,000	AFDB		1,088,403	1,093,403
Mradi wa kufanya tathmini ya mali zaSerikali	200,000	500,000				500,000
Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba	150,000	150,000				150,000
Kuifanyia mabadiliko na kuimarisha Tume ya Mipango	100,000	60,000				60,000
Mradi wa mashirikiano ya sekta za umma na ubinafsi	150,000	150,000				150,000
Mradi wa kujenga uwezo wa Takwimu (STATCAP)	100,000	100,000		2,000,000		2,100,000
JUMLA	**8,325,000**	**8,935,000**		**5,126,800**	**16,288,403**	**30,350,203**
UNUNUZI WA MELI	**17,000,000**	**17,000,000**				**17,000,000**
JUMLA KUU	**25,325,000**	**25,935,000**		**5,126,800**	**16,288,403**	**47,350,203**

Kiambatanisho Nam. VIII

MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2012-2013

TZS Billioni

MAELEZO	2011/2012			2012/2013		
	MAKISIO	**HALISI**	**ASILIMIA**	**MAKISIO**	**HALISI**	**ASILIMIA**
Mishahara	105.78	118	112%	139.8	132.6	95%
Matumizi Mengineo	47.17	52.75	112%	71.1	59.3	83%
Ruzuku	33.61	31.74	94%	44.3	40.7	92%
Mfuko Mkuu wa Serikali	47.62	31.39	66%	54.9	54.9	100%
Jumla Kazi za Kawaida (A)	234.18	233.88	100%	310.1	287.6	93%
Matumizi ya Kazi za Maendeleo (B)	378.91	210.45	56%	37.3	31.2	84%
JUMLA (A) na (B)	613.09	444.33	72%	347.4	318.8	92%

Chanzo : Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali 30/6/2013

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mhe. Mwenyekiti Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ifuatayo ni hotuba ya Mwenyekiti, wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia uzima, siha na nguvu zilizoweza kutufikisha hapa Barazani na tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga, hatuna budi kusema Alhamdulilah!

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu za dhati pia zije kwako kwa kunipa nafasi hii ya kusimma hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kutoa muhutasari wa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio ya mapato na matumzi kwa mwaka 2013/14 ambayo punde hivi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo amewasilisha mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika**,** nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi zetu za kawaida za Kamati. Tunawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa wajumbe na makatibu wa kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti, nawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii, naomba sasa niwataje kwa majina wajumbe na makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Masoud Hamad	-	Mjumbe

4. Mhe. Viwe Khamis Hamad	-	Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayub	-	Mjumbe
7. Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu
9.Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	-	Katibu.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina majukumu makubwa na mazito ya kitaifa na yale ya kisekta kama zilivyo wizara nyengine. Wizara hii huratibu Tume ya Mipango, kupitia Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza umaskini, Kukuza Uchumi, Maendeleo ya Watendakazi na pia kusimamia takwimu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, mbali na majukumu hayo, Ofisi hii pia husimamia ukusanyaji wa mapato yanayoratibiwa na Bodi ya Mapato nchini (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na yale yanayoratibiwa na Idara ya Fedha za Nje.

Mhe. Naibu Spika, suala la kusimamia matumizi ya serikali ni muhimu, wizara husimamia Idara ya Bajeti na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuona kuwa matumizi ya serikali yanatumika kwa mujibu wa sheria za fedha na sheria za matumizi ikiwa ni pamoja na kufuatwa kanuni zilizopo na kuhakikisha kuwa fedha zinagawiwa kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo na si vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majukumu hayo mazito pia husimamia Idara mbali mbali za kisekta na taasisi zilizo chini ya Wizara hii ya Fedha, lakini pia hufanya kazi kwa karibu na taasisi za Muungano kama vile Tume ya Pamoja ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Kusimamia Bima (TIRA), Benki ya Posta na taasisi nyenginezo.

IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ina majukumu makubwa ya kuitunza Hazina ya Serikali, kusimamia mwenendo wa Deni la Taifa, kudhibiti mapato na vilevile kusimamia shughuli za kihasibu na Ukaguzi wa Ndani kwa kuhakikisha kwamba taratibu na sheria zote zinazohusika zinafuatwa katika suala zima la kudhibiti mapato na matumizi ya serikali.

Katika suala zima la jumuisho la Hesabu za Serikali ni kwamba bado kuna baadhi ya idara na taasisi za serikali huchelewesha kufunga hesabu zake za mwisho wa mwaka na pia baadhi ya mashirika na halimashauri hazifungi

hesabu zake kabisa. Hali hii inapelekea kutofahamika kwa mwenendo ya taasisi hizo na matokeo yake ni kuwa taasisi hizo zinajiendesha kwa hasara na hatima yake ni kushindwa kujiendesha wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwa kuna sheria zimetungwa za kuwachukulia wale wote wasiofunga hesabu zao lakini bado hakuna Taasisi hata moja iliyochukuliwa hatua, hivyo ni vyema tukaondosha muhali na tukatekeleza wajibu wetu kwa kuwachukulia hatua wale wote wazembe wasio funga hesabu za mwaka.

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza serikali kwa kuweza kuwalipa wastaafu viinua mgongo na pencheni zao kwa wakati muwafaka, lakini bado kuna malalamiko ya kulipwa wastaafu hao fedha nyingi zaidi ya zile wanazostahiki kulipwa na pia kulipwa wafanyakazi ambao bado hawajafariki na kuelezwa kuwa wamefariki. Tunashauri wizara kufanya uchunguzi wa kina kabla ya kuanza kulipwa mafao kwa wafanyakazi kwani kuna wasi wasi mkubwa wa kufanyika kwa ubadhiru wa fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imekuwa ikisisitiza sana suala la kuwaweka wahasibu kwa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi na tunasema kuwa kukaa muda mrefu wahasibu kunapelekea kuzoeana na viongozi wa taasisi husika na mashirikiano au mazoea hayo yanawapelekea kujiamini sana wahasibu hao na kuchukua mamlaka na nguvu za viongozi na mwisho kujiamulia mambo wanavyotaka wenyewe. Taasisi nyingi zinazotokea upotevu wa fedha za umma wahasibu wake wanakuwa ndio wale waliokaa kwa muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake Idara hii pia inaratibu na kusimamia wakaguzi wa ndani wa hesabu waliopo katika taasisi mbali mbali za serikali. Hata hivyo kumekuwa na malalamiko kadhaa ya kutowajibika vyema kwa wakaguzi hao wa ndani. Hivyo, Kamati inaitaka wizara kuharakisha utekelezaji wa hatua mbali mbali inazokusudia kuchukua katika kuimarisha ukaguzi wa ndani wa hesabu zikiwemo kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani wa hesabu kwa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara, kuimarisha Kamati za ukaguzi pamoja na kubadilisha mfumo mzima wa ukaguzi wa hesabu za ndani.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile suala la kutaka kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu limechukua muda mrefu, Kamati inaona ni vyema Wizara ikalieleza Baraza lako tukufu juu ya hatua zilizofikiwa kuhusiana na suala hilo, kwani ni suala muhimu litaloweza kuongeza uwajibakaji katika utendaji wa shughuli za serikali.

IDARA YA BAJETI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Bajeti ina majukumu ya kusimamia utatayarishaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na kusambaza maelezo yanayohusu mbinu bora za kibajeti pamoja na kupanga na kudhibiti matumizi ya rasilimali fedha kwa taasisi mbali mbali za umma.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sote tunaamini kuwa, ukuwaji wa uchumi ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya kila Nchi, ni vyema basi serikali kupitia Wizara hii ikaelekeza nguvu zake katika Idara ya Bajeti kwa kuwapatia wataalamu wa kutosha katika fani za uchumi. Kama sote tunavyofahamu kuwa serikali imeingia katika mfumo mpya wa bajeti inayotumia programu (PBB)kwa baadhi ya wizara na ina lengo la kutumia mfumo huu kwa Wizara zote tungelipenda kufahamu ni mafanikio yapi hadi sasa yamepatikana katika kipindi chote na ikiwa kuna mapungufu basi ni vyema tungelifahamishwa ili tuweze kuyafahamu na ikiwezekana tuweze kuyatatua.

Mhe. Naibu Spika, mfumo huu mpya unaotumia program bado haujaeleweka vizuri, ni vyema basi Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ikiendelea kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili wapate uelewa zaidi kuhusu dhana hii mpya na kujua umuhimu wake katika kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, bado mwenendo wa matumizi ya fedha za umma sio mzuri, matumizi ya fedha za umma yasiyolingana na uhalisia *(value for money)* ni tatizo kubwa katika Idara za Serikali na Taasisi za umma. Kuendelea kutumia fedha nyingi za umma kwa semina na makongamano ni jambo lililozoweleka siku hizi, suala la kutumia fedha nyingi za umma kwa maandalizi tu ya jambo fulani ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako limeshuhudia hili katika bajeti mbali mbali za wizara zenye matumizi ya aina hii, mafungu makubwa ya fedha kwa mamilioni yametumika kwa kuandaa sera, kanuni, sheria na kuacha kutumia fedha za umma kwa jambo linaloonekana machoni.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwasilishwa ndani ya Baraza la Wawakilishi taarifa za makadirio ya mapato na matumizi kwa kuonesha mafungu na kasma mbali mbali kwa mwaka unaohusika wa fedha kwa Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali zinazosimamiwa na Bodi mbali mbali ikiwa ni pamoja na kueleza hatua za utekelezaji kwa kazi za mwaka ni muhimu sana, ili Baraza la Wawakilishi kuelewa jinsi mashirika hayo yanavyofanya kazi zake

kwa umma na jinsi ya wanavyokusanya wanavyotumia mapato ya umma na isiwe kama ilivyo hivi sasa.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara ya Fedha, pamoja na mambo mengine inaratibu masuala mtambuka, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, moja kati ya mradi ulioratibiwa na Idara hii ni mradi wa *E. Government*, ambapo jumla ya dola za kimarekani shilingi 20 millioni zimetumika katika utekelezaji wa mradi huu, fedha ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Exim ya China.

Mhe. Naibu Spika, mradi huu wa *E. Government* haukupata mafanikio, ingawaje umeripotiwa kukamilika, na hata huo ukamilikaji wake ni wa mashaka.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu kwa Wizara kama Wizara ya Fedha kujiingiza katika matumizi mabaya ya fedha za umma, matumizi yanayotiliwa mashaka na Wawakilishi wako Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na kurushiana mpira kati ya Wizara na Wizara juu ya nani anayehusika na mradi huu, huku mamilioni ya fedha za wanyonge zimeshapotea, huku matumaini ya matumizi ya mradi ule kwa manufaa ya nchi yamekuwa yakipigwa danadana na fedha zaidi zikihitajika, kuendeleza mradi ule.

Mhe. Naibu Spika, niungane na wajumbe wenzangu wa Baraza lako la Wawakilishi, kuonesha wasiwasi wangu juu ya utekelezaji wa mradi huu wa *E. Government* na Baraza Lako Tukufu lifanye uchunguzi wa kina juu ya utekelezaji wa mradi huu na baadaye taarifa za uchunguzi huo ziwasilishwe ndani ya Baraza la Wawakilishi.

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Zanzibar (ZIPA) ina jukuimu kubwa la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini. Suala la kujiuliza Mhe. Naibu Spika, Jee, jukumu hili kubwa kwa maendeleo ya nchi hii limetekelezwa ipasavyo?

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Vitega Uchumi imekuwa ikijitahidi kutekeleza jukumu hili, lakini bado juhudi hizi zimegonga mwamba kutokana na urasimu mkubwa uliopo kati ya taasisi na taasisi. Kumekuwa hakuna mashirikiano ya dhati katika vyombo au taasisi zinazohusiana na masuala ya

uwekezaji nchini, jambo linalosababisha kuzorotesha kasi ya uwekezaji nchini.

Mhe. Naibu Spika, mara kwa mara Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imekuwa ikizungumzia umuhimu wa kuanzishwa kwa *"One Stop Center"* ikiwa na lengo la kuwaweka pamoja wadau wote wanaohusika na uwekezaji ili iwe rahisi kutoa maamuzi juu ya uwekezaji nchini.

Mhe. Naibu Spika, dhana hii imekuwa ni ndoto, lakini wale watendaji wenye dhamana na maamuzi ya ama na vitengo vyao au taasisi zao au Idara zao hawahudhurii katika vikao vinavyoitishwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitega Uchumi, badala yake huwapeleka maofisa wa chini wasio na maamuzi ya jambo lolote.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa suala hili tumekuwa tukililalamikia sana bila ya mafanikio, na kwa kuwa Wizara yako ina lengo la kuifanyia mapitio sheria ya mamlaka ya vitega uchumi, basi katika shera hiyo kiwepo kifungu cha sheria kinachowalazimisha wakuu wanaohusika na uwekezaji kushiriki katika vikao hivyo kisheria kwa manufaa ya nchi na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, uwekezaji nchini ni dhana pana lakini pia uwekezaji una eneo pana katika kulipeleka taifa hili katika maendeleo. Nchi haiwezi kuendelea bila ya kuwa na uwekezaji, mapato ya nchi hayawezi kuongezeka bila ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, Jamhuri ya Watu wa China imekuza uchumi wake kutokana na uwekezaji. Serikali ni lazima itoe kipaumbele katika eneo hili la uwekezaji, maeneo huru ya uchumi Fumba na Micheweni ni lazima yashughulikiwe ipasavyo, ile *master plan* ya maeneo huru ya uchumi ya Fumba ni lazima mwaka huu wa fedha imalizike, ili tutoe fursa kwa wawekezaji waweze kuwekeza katika eneo lile. Suala la miundo mbinu katika maeneo ya uwekezaji lipewe kipaumbele kama vile barabara, maji na umeme ili iwe kivutio kwa wawekezaji.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ndio wakala mkuu wa serikali katika ukusanyaji wa mapato ya ndani yanayotokana na vianzio vya ndani.

Mhe. Naibu Spika, jukumu hili ni kubwa na linahitaji umakini wa hali ya juu, linahitaji uaminifu, linahitaji moyo wa kujituma, bila ya wafanyakazi wake

kuwa na mambo hayo muhimu basi hali ya ukusanyaji wa mapato haitapiga hatua au haitafanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kikawaida wananchi au wafanya biashara huwa hawapendi kulipa kodi kwa hiari na mara zote maofisa wa kodi huonekana kama ni kero kwa wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inatoa wito kwa wananchi na wafanyabiashara kulipa kodi zao kwa hiari bila ya shuruti na wasiwaone maofisa wetu wa kodi kama ni kero kwao. Maofisa hawa wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na wanatekeleza majukumu yao ya kazi kama wafanyakazi wengine.

Mhe. Naibu Spika, nchi bila ya kukusanya kodi haiwezi kupata maendeleo, tunapozungumzia madawa hospitalini maana yake ni kulipa kodi, tunapozungumzia elimu bora nchini maana yake ni kulipa kodi, tunapozungumzia maji safi na salama maana yake ni kulipa kodi. Kwa maana hiyo huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi bila ya kuhusisha ulipaji wa kodi nchini.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inampongeza Kamishna wa Bodi ya Mapato nchini (ZRB) pamoja na maofisa wake wote kwa kutekeleza majukumu yao vizuri hali inayoonesha mafanikio makubwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaamini kuwa mapato zaidi yataweza kupatikana ikiwa mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

1. Ikiwa serikali itasimamia kisawasawa ukwepaji wa kodi unaotokana na wafanyabiashara wengi kutokutoa risiti wanapofanya biashara zao.
2. Ikiwa serikali itawawekea vitendea kazi vya kisasa (ZRB) ambavyo itakuwa ni rahisi kuvitumia kwa kukusanya kodi kama vile utumiaji wa risiti uliounganishwa na mtandao (electronic receipt) kwa wafanyabiashara kubwa na wadogo kama vile nchi nyengine (Tanzania Bara, Kenya n.k)
3. Ikiwa serikali itaachana na utaratibu wa kukubali kupokea watalii wa makundi (Package tours) katika mahoteli. Utaratibu huu hupoteza mamilioni ya fedha, nchi nyingi duniani zimeachana na utaratibu huu.
4. Ikiwa serikali itadhibiti kisawasawa mapato yanayotokana na VISA yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji katika viwanja vya ndege.
5. Ikiwa serikali itadhibiti mapato yanayotokana na utalii (VAT) mahotelini na kuwadhibiti wale wafanyakazi wa ZRB waliokuwa sio waaminifu katika kufanya kazi zao.

6. Ikiwa serikali itadhibiti kisawasawa suala la magendo ya mafuta ya petroli na diesel nchini.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inataka maelezo jinsi gani serikali itakavyojipanga katika kukabiliana na maeneo haya tuliyoyataja katika kuhakikisha mapato yetu yanaimarika.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)

Mhe. Naibu Spika, Taasisi nyengine yenye jukumu kubwa la kukusanya kodi ni Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA). Mamlaka hii Mheshimiwa Spika hukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa, kodi ya mapato na kodi nyengine zinazotokana na biashara za kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo inampongeza sana Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na watendaji wake wote kwa kutekeleza majukumu yao vizuri na kufikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimwa Spika, pamoja na kuwa mamlaka hii hupata fedha za kutendea kazi kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, fedha wanazopatiwa ni kidogo mno ukilinganisha na mahitaji halisi. Hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iangalie uwezekano wa kuwapatia fedha zaidi za uendeshaji ili taasisi hii iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi. Na zaidi ukitilia maanani kwamba mapato yanayokusanywa na taasisi hii ni kwa ajili ya matumizi yetu wenyewe hapa Zanzibar.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ, DAR ES SALAAM

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za S.M.Z Dar-es-salaam ina umuhimu wa pekee kwani mbali na kushughulikia masuala ya kiuchumi na maendeleo kati ya Wizara ya fedha na Uchumi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri Tanzania pia ni kiungo kizuri kati ya serikali ya mapinduzi ya Zanzibar na Ofisi ya kibalozi za nchi za nje pamoja na taasisi za umoja wa mataifa na mashirika ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, inapasa tujiulize hivi kutokana na umuhimu mkubwa iliyonayo Idara hii, Serikali imeipa kipaumbele gani katika kuhakikisha inafanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Serikali inalazimika kujipanga vizuri katika eneo hili muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Nchi yetu, utaalamu wa hali ya juu unahitajika katika kusimamia kazi katika Afisi hii, Afisi zenye hadhi

pamoja na vitendea kazi vya uhakika na vya kisasa vitakavyoweza kuunganisha taarifa mbali mbali za kidunia..

Mhe. Naibu Spika, jengo la Afisi ya Uratibu wa SMZ, haliridhishi hata kidogo, Jengo hili halilingani na hadhi ya Afisi ya SMZ, Jengo ni bovu kiasi cha kutishia usalama wa wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwa jingo lile sio letu, lakini sisi ndio tunaolitumia tena kwa muda mrefu na hatutegemei kama tutapata jengo jengine au tutahamishwa.

Tunaishauri Wizara ya Fedha itenge bajeti maalum kwa ajili ya kulifanyia matengenezo makubwa *(Major repair*). Ili afisi ile iweze kutumiwa na Wizara mbali mbali za SMZ na iwe ni kiungo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Afisi nyengine za ndani ya nchi na nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, haipendezi hata kidogo kuona mikutano ya Balozi mbali mbali zinafanyika katika mahoteli makubwa wakati jengo la Serikali ya Mapinduzi lipo, lakini halistahiki kwa ubovu.

Itapendeza kama mikutano inayohusu Serikali ya Zanzibar kule Dar es Salaam ifanyike katika Afisi ya SMZ Dar es Salaam.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika, mfuko wa barabara unaendelea na majukumu ya uratibu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa lengo kuu la kuanzishwa kwa mfuko huu ni kuzifanyia matengenezo barabara ambazo zimeshajengwa na Serikali au Washirika wa Maendeleo ili kuzifanya barabara hizo ziweze kudumu badala ya kujenga barabara mpya, kila mara fedha hizo zinatumika visivyo.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako Tukufu limeshuhudia kukiukwa kwa lengo hili kuu na badala yake fedha za Mfuko wa Barabara kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikitumika kwa kujenga barabara mpya, kufanya matengenezo ya zana za UUB, kulipa fedha kwa wahanga wa barabara, matumizi mbayo yanakwenda kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

Mhe, Naibu Spika, Serikali inatakiwa iwe makini katika kuzitumia fedha zinazochangwa na wananchi kupitia mauzo ya mafuta kwa kuzitumia katika malengo yale yaliyokusudiwa na si vyenginevyo na itenge bajeti maalum ya Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya

kujenmga barabara mpya, pia kulipia fidia kwa wananchi wanaoathirika na ujenzi wa barabara na kuachana na tabia ya kuzitegemea fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na urasimu wa upatikanaji wa fedha hizi, fedha za Mfuko wa Barabara hupitia mikono mitatu (3) ndio ziwafikie walengwa.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu sio mzuri hata kidogo kwa sababu huchelewesha shughuli za Mfuko. Kamati ya Fdha, Biashara na Kilimo inaishauri Wizara ya Fedha iondoshe urasimu huu wa upatikanaji wa fedha huku wakuelewa wazi kuwa fedha hizo sio zao

IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Naibu Spika, Idara ya fedha za nje inajukumu la kutafuta,kusimamia,kuratibu na kutathimini misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Idara hii imekuwa kifuatilia na kusimamia upatikanaji wa fedha za misaada ya kibajeti (*GBS*) na mikopo. Katika kutekeleza jukumu hili Serikali kupitia Bajeti Kuu ya Serikali hutoa maelezo ya kiasi kilichopatikana kutokana na mikopo na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hupatiwa asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti kutokana na misaada ya Wafadhili, cha kusikitisha ni kuwa kiwango kinachotolewa na Serikali yetu kama ni msaada wa Washirika wa Maendeleo kwa Tanzania cha asilima 4.5 ni kidogo mno ikilinganishwa na kiwango halisi kinachotolewa na Washirika wa Maendeleo kutokana na takwimu zinazotolewa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Fedha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, hali hii haileti taswira nzuri kwa wanachi wetu. Hivyo, Idara hii ya fedha za Nje inatakiwa iwe macho katika kusimamia upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo kama ilivyotolewa na Washirika wa Maendeleo na isikubali kubabaishwa na wasioitakia mema Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo itafuatilia kwa karibu sana fedha zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo kwa Tanzania.

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ina jukumu la kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za Kitaifa kwa watumiaji mbali mbali hapa nchini na hata nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, takwimu ni kitu muhimu sana katika kufikia maendeleo yoyote duniani. Takwimu za hali ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, takwimu za hali ya pato la Taifa, takwimu za watu na makaazi na takwimu za aina nyengine mbali mbali ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, hebu tujiulize ni kwa kiasi gani Serikali yetu imeweza kuzitumia kikamilifu takwimu zinazotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka huwezi kupata jibu ila takwimu inaiwezesha Serikali kujua hali halisi ya jambo fulani na kupanga mipango yake kulingana na takwimu hizo. Hapa kwetu Mhe. Naibu Spika, takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu hubakia katika mashelf ya ofisini bila ya kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, inawezekana maofisa wetu hawaelewi umuhimu wa takwimu katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku. Ni vyema basi kwa Serikali ikatoa mafunzo maalum kwa maofisa wake juu umuhimu wa kuzitumia takwimu katika utendaji wa shughuli zao za kila siku.

CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA (ZIFA)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha (*ZIFA*) kina jukumu la kutoa mafunzo ya fani ya fedha na fani zinazolingana.

Mhe. Naibu Spika, Chuo hiki kimepiga hatua kubwa za maendeleo katika kutoa mafunzo na katika maendeleo ya majengo. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaupongeza uongozi wa Chuo hiki kwa kupiga hatua kubwa za kukiendeleza chuo.

Mhe. Naibu Spika, hatua ya kukamilisha ujenzi wa dakhalia ya kisasa na kukamilisha ununuzi wa samani za jengo la dakhalia sambamba na kuanzisha Shahada ya kwanza ya fedha na Benki pamoja na Shahada ya Uzamili katika fani ya Uhasibu ni hatua kubwa na inastahiki kupongezwa.

Mhe. Naibu Spika, tunaishauri Serikali kukipa nguvu zaidi chuo hiki cha fedha ili kiwe chuo cha mfano kwa Zanzibar kwa maendeleo ya wa Zanzibari.

Aidha, tunaishauri serikali isishawishike na wazo la kukiunganisha chuo hiki na Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA).

Kwa kufanya hivyo kutaweza kusababisha chuo hiki kurudi nyuma kimaendeleo. Bado ni mapema mno kufikiria wazo hilo.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar lina jukumu la kutoa huduma za bima Zanzibar ikiwa ni pamoja na bima za ajali na majanga.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inalipongeza Shirika hili la Bima chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji kwa kufanya shughuli zake kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Naibu Spika, tunalipongenza shirika kwa kuongeza matawi mbali mbali Tanzania bara, hii ni dalili njema ya mafanikio katika shughuli za Bima nchini.

Mhe. Naibu Spika, mbali na mafanikio ya kuanzisha matawi mapya, lakini pia Shirika limeweza kujenga jengo jipya la kisasa kabisa tena kwa thamani inayokubalika *(Value for money).*

Kamati inatoa wito kwa Wizara na taasisi nyengine kuiga mfano wa Shirika la Bima wa kujenga majengo mazuri yenye thamani inayokubalika ili kuokoa fedha za wanyonge walipa kodi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inawaomba wananchi na wafanyabiashara wote kujiunga na Shirika la Bima la Zanzibar. Kwani Shirika la Bima Zanzibar ni Shirika lao kwa maendeleo yao lakini pia linalipa malalamiko *(claims*) kwa haraka sana.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Mhe. Naibu Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni benki ya wananchi wa Zanzibar yenye jukumu la kupokea amana za wateja wake na kukopesha kwa wale wanaokopesheka.

Mhe. Naibu Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar imepiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwa ni kupokea amana za wateja, kutoa mikopo ya aina mbali mbali kwa Wananchi wa Zanzibar, kuongeza kiwango cha rasilimali ya Benki na kukusanya mapato yanayotokana na huduma mbali mbali za kibenki.

Mhe. Naibu Spika, majukumu haya yote yametekelezwa na benki hii hadi kufikia yale malengo yaliyojiwekea, tunawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, lengo la kuanza matayarisho kwa ujenzi wa jengo jipya la makao makuu amabalo litaendana na hadhi ya Benki ya watu wa Zanzibar Ltd ni jambo muhimu,kwani bado Benki hii ya Watu wa Zanzibar haina jengo lenye hadhi na linaloendana na heshima na Taasisi yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo inaishauri Benki ya watu wa Zanzibar kulipa kipaumbele suala hili ili liweze kufanyika katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, lakini pia suala la kufungua matawi mengine zaidi Tanzania Bara katika mikoa ya Mtwara na Mwanza baada ya kukamilika utafiti juu ya mahitaji ya huduma za kibenki katika maeneo hayo ni jambo muhimu kwani litaongeza wigo wa biashara katika benki hiyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la uwiano ya mishahara ya wafanyakazi wa Benki hii ni jambo muhimu sana ambalo litaongeza ari kwa watumishi wake.

Mhe. Naibu Spika, inashangaza kuona mameneja wa Matawi ya Benki hii kutofautiana mishara kati ya meneja na meneja. Jambo hili Mheshimiwa Spika halikubaliki hata kidogo.Hivyo Kamati ya fedha biashara na kilimo inaiagiza Bodi na Manejimenti ya Benki hii irekebishe kasoro hizi haraka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Rais Fedha,Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaombewa idhini ya kukusanya mapato ya Tshs 409,892.4 milioni na Tshs 160,773.20 milioni kwa ajili ya matumizi kati hizo Tshs 44,794.00 milioni ni kwa kazi za kawaida na Tshs 42,438.40 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014, na inawaomba wajumbe wako waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimefurahi sana mimi kunipa mtu wa mwanzo na hasa kwa kuwa tunajua hii ni bajeti ya mwisho na tunaamini kuwa Wajumbe tutapata ile kipindi kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria ya dakika 30. Ninaamini hivyo dakika 30 nitazianza mimi kwa utiifu wako nakuomba sana hilo Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijaalia leo hii. Mimi niende moja kwa moja na kuingia katika kitabu kuweza kuchangia hotuba hii ya leo hasa pale Mhe. Waziri alipoanza na neno kubwa la jina la mtukufu wetu Mwenyezi Mungu kumtaja pale jina la Bismillahi hapa kidogo nilifarajika nikasema alhamdulillahi waziri .

Sasa nakwenda katika maudhui yale ambayo yanatakiwa. Mhe. Naibu Spika, hapo ukurasa huu ambao unatokana na ukurasa wa 17 na ninaingia 18 huku. Mhe. Naibu Spika, hapa kuna namba za kirumi namba III amesema kufanya utafiti katika sekta ya uzalishaji wa viwanda wa utalii na uwekezaji, mimi hapa sitokuwa na jambo kubwa nakubaliana nao na utafiti huo lakini haioneshi dhahiri katika utafiti huo mpaka sasa hivi mafanikio yake naona yako katika hali ambayo hayajaridhisha, ningemuomba sana Mhe. Waziri asichukue muda tena wa kufanya utafiti huo ili aende kusaidia wananchi kuondoa umaskini na hasa katika wananchi wetu wa Zanzibar lengo lao kubwa ni kuondoa umaskini na kwenda katika hali ya maisha mazuri.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Mhe. Naibu Spika, bajeti iliyopita ya Wizara ya Majenzi nilimtetea mtu lakini pale nilipeleka *message* ya kuwa anajiandaa na kuja Idara husika. Tuna matatizo katika Idara zetu niseme ukweli ulivyo na hasa ukiwa mnyonge maskini ya Mungu na hasa ndio hapo wewe unapotafutiwa sheria ya kuweza kukandamizwa na kukosa haki zako.

Mhe. Naibu Spika, Mhasibu huyu Mkuu nilimsema hapa ambaye anafanya kazi Idara ya Majenzi kwa kweli hakutendewa haki. Ninamuomba tena Mhe. Waziri kwa kuwa leo asubuhi alianza na jina kubwa sana la Bismilillahi na kuwa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani inaambatana nayo hiyo kwa sababu mwezi huu ni mwezi mtukufu, mwezi mkubwa kwa Waislamu. Kwa hivyo ninamuomba sana huyu kijana kwa kweli hakutendewa haki na nilikuwa nataka niseme nimnyang'anye shilingi lakini hainyang’anyiki kwa sababu ni moja ambaye ni mtetezi wetu wa haki wa wanyonge. Kwa hivyo sitaki nimnyang'anye shilingi yake kwa kuwa ni mkweli na muwazi.

Mhe. Naibu Spika, kama tunataka kumpeleka kwenye vyombo vya sheria huyu atashinda tu kwa sababu ana vielezo tosha vya kuwa yeye hakuhusika na jambo hilo. Lakini kwa kuwa mnyonge hana watu wa kumtetea, hapa ndio maana anasingiziwa sakata ambalo halimhusu lililokuwa nje na yeye. Mhe.

Naibu Spika, nani asiyejua kuna watu wengi wezi, jana hapa tumesema Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akasema hatokubaliana na suala hilo la watu wizi lakini hii ni lugha ya siku zote wapo watu wanaojilimbikizia mali tu ya wanyonge, lakini mpaka leo hawajatiwa pingu wala hawajadhalilishwa kwa kuwa nini? wana uenyeji, wana fedha na nini. Kwa kweli hili jambo linasikitisha sana sana Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana mheshimiwa huyu kijana arudishwe kazini. Naomba hoja yangu atakapokuja hapa anikubalie kwa sababu hana kitu cha kufanya huyu mtu, mpaka leo amewekwa nje, anapewa mshahara mdogo hakuna sababu hiyo lakini kwa kuwa mnataka kulinda jambo ndio mnatoa sababu hizo.

Naomba sana kijana huyu arejeshwe kazini *immediately* kabisa iwezekanavyo. Mimi nimeshaangalia vielelezo vyake na kila kitu kwa kuwa kidogo nimepitia sheria, nimekungua hana tatizo. Lakini kuna *block* ambayo inataka kumlinda mtu ndio sababu na yeye akaona atiwe kwenye kundi. Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, hili suala liangaliwe kwa uhakika kabisa na mwenendo wa sheria za utawala wa kazi zifanyike aweze kurudishwa kazini.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika uhakiki mali, nimshukuru sana Mkurugenzi huyo kwa kusimamia vizuri mali za serikali na kuzitolea taarifa ambazo kwa mujibu wa sheria na kuziweka ndani ya *database* zake kwa mujibu wa sheria, ninamshukuru sana kwa utendaji huo wa kazi na inshaallah Mungu amjaalie kwa kuwa yeye ni mpya basi aendeleze vizuri Wizara hiyo na atimize wajibu wake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika Bodi ya Mapato na hapa nimpongeze sana na azidishe sana kwa sababu asilimia kila siku kukicha inaonesha inazidi kupanda juu katika makushanyo yao. Nimshukuru sana Naibu wa Kodi ya Mapato, Kamishna huyo kwa utendaji wake wa kazi nzuri na ufanisi wake mzuri na katika kulinda mali ambazo kwa ukushanyaji kama alivyosema mwenyekiti wangu kuwa wafanyabiashara waendelee kulipa kodi ili kuweza kutusaidia kupata madawa, kusaidia kujenga majumba yetu hayo ya kiserikali, mishahara kuweza kupandishwa kwa wanyonge, zaidi mimi naomba sana.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, katika Mamlaka ya Mapato (*TRA*), halikadhalika hapa bado nataka kumwambia Kamishna muhusika bado hali halisi hapa bado mapato yanavuja, watu hawalipi ipasavyo tunaomba sana usimamizi wa hali ya juu ufanyike ili na yeye afikishe malengo ambayo yanakusudiwa na serikali ipasavyo. Ninamuomba sana awe mkali afuatilie sio akae kwenye kiti anazunguka na huku mambo yanavuja, naomba sana hilo suala alifanyie kazi kwa uadilifu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa huu mfuko wa barabara. Mimi hapa ninakuwa na wasi wasi Mhe. Naibu Spika, kuwa bado ninaiomba sana Mhe. Waziri uikubali kamati yako ya *PAC* iende ikafanye uchunguzi katika mfuko huu wa barabara, nina mashaka makubwa sana, sio utani kabisa Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nina mashaka makubwa sana na ndio maana hata zile fedha zenyewe hazitoki vizuri hazifaidiki katika malengo ambayo aliyokusudia.

Mimi naomba sana hapa tuwe *serious* kabisa katika jambo hili, naomba sana uikubalie *PAC* kwa makusudi iende ikafanye utafiti hapa ya mahesabu yetu jinsi gani mfuko huu unavyotekeleza. Na nikikuuliza uje unijibu suala ambalo tangu ianze kutoa fedha hizi na mpaka leo kiasi gani mmeshaanza kutumia na kiasi gani kimo ndani. Naomba hizo *data* Mhe. Waziri uje kuniletea kwa hakika kabisa ili kufika pahali tufanye kazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega Uchumi. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wetu na Naibu wake wa vitega uchumi. Mhe. Naibu Spika, wanafanya kazi vizuri lakini wanafanyakazi katika mazingira magumu, kuna sheria ambazo bado zimepitwa na wakati, tunaomba sana zirekebishwe kwa utekelezaji huo ili tufike pahali pazuri sana. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunapowapa watu mamlaka ya kufanya kazi katika Idara husika tusiwaingilie tuwaachie sheria zao wanazo za utekelezaji. Tunapofika sisi tunawaingilia inakuwa hawendi vile malengo ambayo tumekusudia. Mimi naomba sana Mkurugenzi atumie sheria, atumie wataalamu wake, tuwape *power* hiyo tuwaachie kwa sababu tayari tushawajengea sheria lakini baadae tunawanyang'anya zile sheria tunaamua sisi yale ambayo tunayoyataka. Mhe. Naibu Spika, mimi hilo sikubaliani nalo.

Ninaomba sana tunapompa mtu haki yake basi tumwachie atekeleze haki yake kwa mujibu wa sheria afike pahali mwenyewe ajiridhishe kwa sababu huyo ana timu ya wataalamu, ana sheria lakini tunafika pahali tunambana anashindwa kutumia wajibu wake, anashindwa kutekeleza sheria ambayo tuliyoitunga. Hapa kwa kweli hiyo haiji katika mantiki nzuri. Lakini nataka nimwambie mshauri wangu tunapokuwa sasa hivi tunawapa wawekezaji waekeze Zanzibar tuongeze na sheria ambayo tuwaambie kuwa Zanzibar kuna wafanyakazi ili tuwapatie wafanyakazi kwa asilimia, kwa sababu sasa hivi utakuta kuekeza vitega uchumi kwa neema ya wa kuwapatia wananchi wa Zanzibar, wanakosa fursa hiyo ya kufanya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hii haingizi na kinachoingiza tunakiomba waachiwe wenyewe, kwa sababu hawa wana kitu huwa wanakwenda katika maeneo kukagua wanakuwa wanafanya ukaguzi kwenye *visit site* huko, basi

naomba waheshimiwa hiki kilichopatikana mle waachie wenyewe ndio walichokuwanacho kwa sababu hawazalishi hawa isipokuwa kuingiza chao ni hicho tu. Naomba sana Mhe. Waziri hichi kitonge kidogo waachieni wenyewe ili waweze kujitosheleza vizuri kufanya kazi zao kwa ufanisi kabisa. Na tukisema tukichukue hiki basi itakuwa wale watashinda hata kupata *fuel*, mambo ya petroli hizo mambo ya *oil* na kwenda kule katika *site*. Itakuwa kila siku ndio yale yale tunasema kuwa tunatumia kiti kuliko kazi zenyewe.

Ninawashukuru sana Mkurugenzi na Naibu wake na watendaji wake wote wakuu, wapo kitu kimoja wanafanyakazi kwa uadilifu kwa mujibu wa sheria tuliowatungia sisi na kuwapa wao. Hilo moja niwape hongera hiyo na wazidishe, kwa sababu sasa hivi kila siku ukicha *ZIPA* wanapokea miradi tu, nalo hilo ni la kuwapongeza na wapo *faster* kweli hawakawii wanatekeleza wajibu wao wa kazi. Kwa hivyo na wao ni lazima tuwape *special request* ya kuwapongeza katika jitihada zao za kazi na Mungu awajaalie waendelee kufanya kazi hiyo na Wazanzibari lengo lao na kitovu chao wanaangalia wao kuwepo miradi mingi wana mategemeo Wazanzibari kupata kazi, wana mategemeo kupata mahitaji yaliyokuwa muhimu ya lazima.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika mfuko wa *ZSSF* na hapa nimsifu sana Mkurugenzi lakini kuna kasoro ndogo ndogo lazima niziseme siwezi kuzimezea ndani ya nafsi yangu. Bado Mkurugenzi na maafisa wale baadhi ya maeneo hawajakamilisha kufuatilia uwekaji wa fedha na kuwaletea kutoka kwenye mahoteli kuja katika wizara husika. Naomba sana wafanyakazi wengi wa mahotelini, wanadhalilishwa kusema la ukweli pesa zao zinakusanywa lakini hazipelekwi kunakohusika. Ninakuomba Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi kesi ngapi ambazo umeshazihukumu ambao wale watu waliokuwa hawapeleki fedha za wafanyakazi. Naomba unambie hilo suala ambalo hapa nitakuwa sina tatizo.

Lakini nimefurahi sana Mkurugenzi huyo ukimpigia simu tu ukimuelekeza basi anakuitia vizuri lakini sijui kama anatuma wale wafanyakazi wake, namuomba sana kwa suala hilo ajitahidi sana ili tupate mafanikio mazuri kwa hawa ambao ni wanachama wake, naomba sana hilo Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi awe *strictly* sasa hivi aiache meza aende *field* kabisa hoteli hadi hoteli na sisi tuko tayari Waheshimiwa kwa sababu Waheshimiwa sasa hivi tunajitolea tuko *free* hatutaki posho, hatutaki chochote lakini tunataka kuhakikisha katika bajeti inayokuja hatutaki tena malalamiko yale kwa yale. Hilo Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mkurugenzi mimi niko tayari wakati wowote watu wanadhalilishwa kutokana na hali halisi kwamba wao wanakatwa lakini fedha hazifiki, wawatie ndani hawa wawekezaji wala wasiwaweke kabisa, wawaweke ndani ambao wanawadhalilisha wafanyakazi

wasiolipia kodi ambapo kwa mujibu wa sheria wawafutie na wawaweke ndani, tusiogope bwana Mungu ndiye mleta riziki.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika Benki yetu ya Zanzibar. Niwashukuru sana Benki ya Zanzibar na hasa nilipokwenda katika tawi la Dar es Salaam. Kule tawi la Dar es Salaam kila baada ya muda wanakuwa na *morning meeting* ya kujisawazisha wao wenyewe ili kujua leo tumekosea wapi, leo tumemkera nani, leo tumefanya nini. Mhe. Naibu Spika, na hapa kama hakuna hiyo *meeting* ya aina hiyo ningeomba na wao wafanye ili kusawazisha hilo suala. Kwa kweli hii ni moja katika *correction* iliyokuwa ni nzuri na inaonesha ufanisi mzuri na ndio maana ukakuta sasa hivi tawi letu la kule Dar es Salaam la *PBZ* linakubalika asilimia kubwa, tena si mchezo nimeshuhudia mimi mwenyewe watu walivyomiminika na watu wanavyopeleka fedha zao kwenda kuweka. Lakini na serikali nayo iangalie sana benki hii kwa kuwawezesha na kuwatafutia fungu la fedha ili kuwapa *competition* na hizi benki ambazo zinaingia kama utitiri hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, benki hii kama ikipata fedha nyingi ikija *LC* ya kampuni ya kutoka nje kwenda kuwekeza kama itakuwa na uwezo wa fedha nyingi, leo inashindwa hii kwa sababu mtaji wake ni mdogo. Sasa nalo hilo naomba tulione, wananufaika mabenki mengine kwa kupata ile *percentage* ambayo ya kuichukua *LC* na hawa benki wengine kuwadhalilisha wana kampuni vile vile katika ku-*delay time* ya kuweza kufuatilia kule benki za nje ili kupata *income* hapa mabenki yakaweza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa hii hatua iliyofikia sasa hivi ya kusema kwamba wana njia ya matayarisho ya uundaji wa sera ya mipango ya nyumba na sera ya mikopo ya wateja wadogo wadogo. Hapa nimefurahi sana kwa sababu mara nyingi sana benki yetu hii haikuwa na mfumo huo, lakini kwa kuwa sasa hivi imeshajitosheleza inataka kujitanua na *practice* kubwa wameifanya katika jimbo la Kitope baada ya kuvikusanya vikundi na kuvipa semina na kujiandaa katika kuwapa mikopo hiyo. Nawaomba sana Mhe. Waziri uniambie mpango huu lini utaanza ili kuweza kuwaneemesha wananchi hawa wafanyabiashara wadogo wadogo katika majimbo yetu. Mimi naomba sana Mhe. Waziri uje kunijibu.

Lakini kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa hivi sasa kwa kusema la ukweli lazima wakae wizara tatu; nimekusudia Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumi, Fedha na hawa watu wa utalii na *ZIPA* tuone jinsi hivi sasa, kwa sababu sasa hivi kuna ma-*PO* wa nje, wakati sisi sasa hivi tuna uwezo wa kuweka ma-*PO* wetu hapa Zanzibar na ndio nikasema tuangalie sheria inasemaje. Sheria inasema kuwa hata *foreigner* akikaa hapa kwa muda wa miaka sita kwa maana hiyo awe ameshamfundisha mtu na aweze

kuondoshwa, lakini sheria hiyo mpaka sasa hivi haijatekelezeka. Namuomba sana Mhe. Haroun na watu wake wakae vizuri ili kwa kuliokoa hili suala Wazanzibari na wao waweze kutumia fursa hii ya uwekezaji. Mimi naamini Mkurugenzi ni hodari sana wa *ZIPA* na wakati wowote simu yake ipo wazi.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa si mwingi wa shukurani kutomshukuru Katibu wa Wizara hii, ninamshukuru sana Katibu wa Fedha na Manaibu wake wawili; mama na baba niwashukuru sana kwa kutuandalia semina ile na kutupa maelekezo mazuri na kutupa faraja kubwa sana. Mimi namuelewa Katibu hakuanza jana na leo, tulikuwa naye katika *TRA* aliendesha kazi vizuri na ndio Mungu akamjaalia akampa mpaka kufika Katibu, ni mtu ambaye madhubuti ni mzuri hana tatizo la aina yoyote, ni mtu ambaye anasimamia haki za wafanyakazi, haki za Mawizara katika utekelezaji. Nimeona niseme hivyo kwa sababu ni mtu ambaye ni mahiri na mtekelezaji mzuri na ndio maana Rais akamuona.

Kwa kumalizia nimshukuru sana Mhe. Waziri halikadhalika na yeye ambaye ni mtu mwenye *experience* wa kazi hizi na ndio maana Dkt. Shein hakupotea kumchagua yeye kumuweka katika Wizara hii ambayo ni mahiri, ukimpigia simu Waziri hana maringo anafanyakazi yake. Tulimwambia suala la uvujaji mapato bandarini, Waziri kalifanyia kazi amekwenda kufanya kazi nzuri, nimshukuru sana Mhe. Waziri na inshallah Mungu ambariki na hasa kwa lugha ya leo ya Bismillahi ile aliyoitaja leo basi namuomba kuwa Mwenyezi Mungu amzidishie kila pamoja na yeye.

Mhe. Naibu Spika, ninamuunga mkono asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ya pili lakini vile vile niwashukuru wenzangu wote niliokuwa napata mashirikiano. Vile vile Mhe. Naibu Spika, kwa sisi Waislamu tuko katika *lailatul kadri* ni mwezi mzuri sana kwa wiki tunayoimalizia.

Mhe. Naibu Spika, nianze kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi, kaka yangu, mwenzangu Mhe. Omar Yussuf Mzee, vile vile niushukuru uongozi mzima wa Wizara yake, maana yake nikiushukuru uongozi mzima wa Wizara yake inakuja *TRA*, *ZIPA*, *ZRB* taasisi zake zote. Mhe. Naibu Spika, ninataka nikuhakikishie kwa sababu ya uwezo waliokuwa nao ninaamini kama watapata nguvu za Baraza hili la Wawakilishi, uwezekano wa sisi Zanzibar kujikwamua kiuchumi tunaweza tukafika mbali sana kwa sura na uongozi waliokuwa nao na naamini watendaji wake kwa kuwaona wana uchungu na nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pamoja na kaka yangu Mhe. Salmini Awadh, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha amechambua mambo mengi pamoja na Mhe. Waziri, lakini yote waliyokuwa wameyazungumza ni namna gani ya kuweza kutafuta vianzio vya mapato ili visaidie maendeleo kwa ajili ya wananchi wa Unguja na Pemba na ndio maana tukafika hapa tulifanya mapinduzi ya Zanzibar kuwaletea maisha bora wananchi ya maji, barabara, umeme na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika haya na humu ndani tuliokuwepo zogo letu sote sisi Wawakilishi ni kuwatetea wananchi wa Zanzibar na kumsaidia Waziri. Mhe.Naibu Spika, haya ni mambo *fresh* nimekuja nayo, yale ya juzi sinayo tena, haya ni mapya nimekuja nayo wala si ya marejeo *hansard* ipo. Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuchukua magazeti yetu ya Serikali na ya Chama. Gazeti hili la Habari Leo kodi ya simu kutobadilika. Gazeti la Uhuru, tozo ya simu iko pale pale.

Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Bara au Waziri wa Tanganyika kasema wana mapungufu, wenzetu Bara wana mapungufu kwa zaidi ya shilingi bilioni 160. Sasa njia ya kuweza kukidhi yale mahitaji ya wananchi wao, maana yake yeye kasema kwa ajili ya Bara tu mwisho Chumbe anasema wameamua kutoza wananchi shilingi elfu elfu ili kwa Tanganyika zikasaidie vijijini maji, barabara, umeme haya ndio maelezo yao. Sasa Mhe. Naibu Spika, suala hili ni suala la muungano, hii ya ukataji wa simu kwa shilingi elfu elfu kwa sababu Zanzibar wako wananchi ambao wanazitumia hizi simu. Sasa mimi nataka nimwambie tu Mhe. Waziri, ushauri huu na ninaomba Wawakilishi tufike pahala tuelewane, aseme mawili kwamba kodi hizi zinazotaka kukatwa ili zifidie kwa wenzetu Bara shilingi bilioni 160 lisiwaguse Wazanzibar mwisho ziwe Chumbe. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, la pili kama kodi hizi zitaweza kutekelezeka basi sisi Zanzibar tuna wateja na tuna wananchi na matumizi ya Zanzibar kwa kodi hizi zibakie Zanzibar ili ziende zikasaidie visiwa vya Unguja na Pemba kwa maji, barabara, umeme na kadhalika. Sasa Mhe. Waziri nataka kumwambia kwamba hapa huyu Waziri wa Bara kachemsha, huu ndio ushahidi. Hakupaswa kutamka bila ya kuishirikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mimi nasema kwamba Waziri wa Bara, Waziri wa Fedha Zanzibar tuko sawa sawa kimuungano, hakuna mkubwa wala mdogo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine lililonishitua zaidi, tunaambiwa deni la serikali linafikia *trillion 22.* Naibu Waziri wa Bara anasema bado tunakopesheka. Mhe. Naibu Spika, hii unaposema deni la Serikali la Tanzania, pesa hizi walizokuwa wamezikopa nataka tu kwa Waziri ufafanuzi, bajeti hii ya Baraza la Wawakilishi pesa waliokopa ni sawa sawa na miaka 25

kwa bajeti hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa hapa kama hatujakaa hili deni unalosema la Tanzania, mimi nina hakika na nina ushahidi madeni haya si ya muungano na kama ya muungano ni madogo tu. Sasa ninachoogopa Mhe. Naibu Spika, tukikaa Mhe. Waziri atufafanulie jee *trillion* hizi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunadaiwa ngapi na hii Serikali ya Bara imekopa ngapi ili tuelewe tutakuja kuwaumiza wajukuu zetu, virembwe zetu sote tutaondoka humu kwa sababu wanasema bado tunakopesheka, watakwenda kukopa hawa kwa jina la muungano na kwa jina la Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri kwa utaratibu wake atuambie Zanzibar tunadaiwa ngapi na wao wanadaiwa ngapi. Sisi Zanzibar tunalipwa je mambo au pesa hizi wanazokopa si ya muungano analipa nani ambayo si ya muungano. Sasa nasema sote tunaipenda nchi yetu lakini tunataka ufafanuzi kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Waziri mimi sitaki nionekane labda ni mkorofi kwamba Mohammedraza anakuja hapa anazungumza mambo ya muungano tu aah! kwa sababu haya mengine wenzangu wanayaweza, mimi katika mmoja wa waoshaji maiti ninayajua mambo mengi, kuna wengine wamekuja kwenye matanga tu.

Mhe. Naibu Spika, unajua mti wa mbirimbi haukodishwi zinapuputika tu, sasa sisi Wazanzibari tunapuputika, maana mmesikia mbirimbi kukodishwa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninachoomba kuona kwamba masuala haya yanakaa sawa ili sote tupendane, mimi mwenyewe ninaupenda umoja, ninaupenda muungano lakini uliokuwa na usawa, nchi mbili zimeungana huru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, hichi kitabu nimezungumza zaidi ya miaka 20 na kimetiwa saini na Rais aliyekuwa madarakani Dkt. Salmin Amour Juma (Komandoo) Rais wa Zanzibar tarehe 14 Septemba, akiwa madarakani na haya mambo nimeyaeleza. Nimeyaeleza vile vile kabla ya muungano wetu huu nchi kumi na saba tulikuwa tuna ubalozi Marekani, Ufaransa, Uingereza, China yote. Sasa Mhe. Naibu Spika, tuko katika masuala mazuri sana lakini wenzetu *are there serious?* kwa sababu mimi sioni kwamba tugombane lakini naona haya mambo kila tukenda yanazidi na kama hayana rekodi tutazidi kuja kuumizana, leo tupo watoto wetu wengine hawajui haya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna Kamati ya pamoja hii na ndani ya kitabu nilieleza miaka kumi na nane, Tume ya Pamoja ya Fedha ili kujua sehemu zote au kuchangia muungano wetu huu, muungano una historia, kuna historia ya udugu, Tume ya Pamoja ya Fedha ilimaliza kazi yake na ikawasilisha pendekezo kwa upande wa Zanzibar na ushahidi tulimaliza kamati ya pamoja ya fedha Agosti, 2006 wenzetu Bara wana sababu zao, sisi tulimaliza hapa Zanzibar mpaka leo wameinyamazia kimya hii hawaitaki na kwa sababu gani

hawaitaki. Nataka nikuhakikishie Mhe. Naibu Spika, kama kuna michango ya muungano basi inatosheleza sisi kuchangia na kuwa na akiba kubwa katika fedha.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka nielewe kuwa Wazanzibari sisi hatuna tatizo na haya yote tunachopenda kwamba ni nchi ambayo tumeungana kila nchi huru, maana umeshasema nchi huru, Serikali mbili, maana yake Serikali ya Tanganyika, Serikali ya Zanzibar, ukaita Serikali ya Tanzania mimi niko hapo tu kwamba nchi huru, hakuna bwana wala hakuna mdogo wala mkubwa. Sasa Mhe, Naibu Spika, Kamati hii ya Fedha mpaka leo Mhe. Waziri, 2006 Agosti hivyo jamani viongozi wenzetu huko, maana yake usile na kipofu ukamgusa mkono, huwezi kujenga nyumba kwenye mawingu. Mimi nafikiri tufikie pahala Mhe. Naibu Spika, haya matatizo tusisubiri tu mambo mengine ya Katiba hayamo, kila mtu ana uchumi wake lakini leo wenzetu tulifurahikia kupata na mimi niliwaambia miaka 10 iliyopita, wakasherehekea wenzetu tumepata bendera, bendera hata mimi ninayo Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Simba na Yanga zinazo bendera, tunataka uchumi huru Zanzibar. Sisi tukitaka kukopa, tukitaka tufanye jambo tuende kwa wenzetu, wenzetu wanapotaka kuamua jambo wao hawataki kibali, sasa hapa tuna nchi mbili? Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Mhe. Waziri ninamuheshimu sana angalau watusaidie kuweka hizi kumbukumbu, hili la deni, hili la bilioni 160 tunafanyaje, tunakubaliana vipi hili ndio Baraza la kutoa maamuzi.

Mhe.Naibu Spika, vile vile suala la mapato yetu, tumeona matatizo hadharani, tuna pesa zetu, wale wenzetu wanakusanya, zinatumika, tunapokwenda kudai ngumi mtu, shida yaani kuna mengine wenzetu wameshapiga kahawa nzuri imekuwa tatizo kubwa sana kwa watendaji na wala hawajui umuhimu wa muungano wetu, hawa wamekuja kutuumiza tu wala hawana habari na muungano wetu huu ulikujaje. Muungano huu ulikuwa wa kuaminiana na mpaka tulipofikia ulikuwa wa kuheshimiana, kuvumiliana na kujadiliana.

Sasa Mhe. Naibu Spika, juzi naona kwenye gazeti Bara wanatuambia Zanzibar Shirika la *ZECO* la Umeme. Mimi nimpe ushauri Mhe. Waziri, sisi tuna fedha zetu nyingi huko nyingi tena tunazowadai. Mimi ninakumbuka awamu ya tano Shirika la Umeme la *Tanesco* pamoja na Shirika la Zanzibar hatukuwaomba tuliamua tu, tuliwaambia wenzetu kule awamu ya tano, bwana Shirika la *Tanesco* mnalidai Shirika la Zanzibar bilioni tatu, sisi tuna bilioni kumi hatuombi eeh! tunasema bilioni kumi kata bilioni zako tatu tuweke hesabu sawa, hakuna suala la kuomba. Sasa nimwambie Mhe. Waziri kama wenzetu juzi wanasema tunadaiwa sisi tuna fedha zetu nyingi mabilioni, wafanye hesabu wamwambie Waziri wa Fedha pale kama kuna hili mimi nimeshafanya utaratibu, nishafanya mahesabu Shirika la *ZECO* linadaiwa bilioni tano au sita basi hamna tatizo limalize kata hizi milioni tano,

imekwisha hatuombi, hiyo tunakwenda tunatoa tunasema hamna bwana. Maana yake katika mambo kama haya tutaweza kufika pahala ambapo tutafika lakini ninachotaka kusema Mhe.Naibu Spika, nimekuja hapa kwa nia moja ya kukuza udugu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima la mapato, hili suala sote tunahitajia. Mimi ningeliomba taasisi zote zilizokuwepo, sote tunahitajiana kati ya wafanyabiashara pamoja na wapokeaji kodi na walipa kodi sote tunahitajiana. Nafikiri uzuri zikatumika na busara na hekma katika kufuatilia haya mambo ili tuone na mimi ninatoa wito kama mfanyabiashara kwamba bila ya sisi wafanyabiashara kulipa kodi hata haya yaliyokuwemo humu ndani hayawezi kutekelezeka. Kwa hivyo ili tuweze kutekeleza kuanzia mimi Raza na wenzangu tulipe kodi ili huduma za vijijini ziende zikatekelezeke ya maji, barabara, umeme na mambo mengine. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, suala la kodi ni suala muhimu sana na suala ambalo linafaa lipewe kipaumbele.

Kweli Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Salmin Awadh alisema na mimi ninaunga mkono kwamba kuendelea kupokea watalii na pesa kubakia nje Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili litakuwa linatuumiza siku zote, tutapokea watalii milioni 2 lakini watalii wote wanalipa huko. Sasa kama hatukuwa na mfumo wa pamoja na hapa tunataka mashirikiano tunataka mashirikiano *ZRB*, *ZIPA*, Shirika la Utalii, Wizara ya Habari haya yote yawe *co-ordination* na yakiwa na *co-ordination* tutaweza kufanikiwa kwa pamoja. Ndio maana nikasema sote tunahitajiana na Wizara zote hizi zinahitajiana. Sasa ni kukaa kitako kuona jinsi gani.

Mhe. Naibu Spika, *ZRB* wanaweza kuwa na hali nzuri ya kuona upeo ule lakini huyu mmoja akawa hana uwezo wa kuona yale. Sasa hapa ni tatizo lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, kweli kuna haja ya kufuatilia mapato yetu mengi, bado mimi ninaomba watendaji wawe wafuatiliaji lakini wapewe nguvu. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, inaweza kuwa kampuni tu ya kigeni inadaiwa milioni 200 lakini akadaiwa John, Hamad au Pandu milioni tatu mtakwenda kuwatia pingu, *that is not fair*, lazima tutizame udugu na uzalendo wetu. Sasa ni uzuri tukajua kwamba na madeni kutopokea na kuacha kwa sababu tu kwa urafiki tutakuwa siku zote tunaumizana katika masuala yetu ya jumla. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mimi naamini kwamba Mhe. Waziri ni msikivu, ana hekma, ana busara na watendaji wake wote Mungu amjaalie lakini na sisi tutoe mashirikiano kuona jinsi kwamba haya mambo yanatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, haya mambo yamejitokeza juzi na mazito, sipendi kurejea rejea, mtu anasema ana upungufu wa bilioni 160 hana habari kabisa na Zanzibar na anakusanya na magazeti ya Uhuru, maana ningemletea gazeti la

Mwananchi na nini mkasema aah! hayo si yetu hayo. Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachosema mimi kwa hisia nzuri pengine hawa wenzetu wachache hawatutakii kheri umoja wetu huu na ndio matokeo yake yanatokea hayo. Sasa Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Waziri mambo kama haya asichelewe kutoa tamko la Zanzibar. Sasa hivi fedha kama tutapata mgao wetu hawatufanyii hisani tutamaliza matatizo mengi sana ya vijijini haya ya maji, kilimo, barabara zetu za ndani ambazo toka jana tunaumiza vichwa kwa mambo madogo tu. Kwa hivyo mimi nafikiri Mhe. Waziri mambo kama haya pamoja na watendaji wake wawe makini.

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee kushukuru na kukushukuru wewe na Baraza lako nitatatoa mashirikiano, nitakuwa mkweli katika kuwatetea Wazanzibari na nimekuja hapa kuyashughulikia maslahi ya Wazanzibari kuweka mbele. Viongozi ninachotaka kusema tuekeni alama tukiondoka tukumbukwe, kiti hichi cha Uzini mimi sikuja nacho wala sikuzaliwa nacho. Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono kama nilivyounga mkono Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa Mhe. Nassor Mazrui, yeye nilimuunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Uzini asilimia 110 kuliko asilimia 100, basi mimi namuunga mkono Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Uzini, asilimia 120 bila ya tatizo lolote. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe:Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa tatu katika hotuba hii muhimu. Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna wanavyojitahidi, wanavyokwenda mbio katika suala zima la kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Lakini vile vile pongezi zangu naomba nizipeleke kwa Kamati ya Fedha kupitia Mwenyekiti wake Mhe. Salmin kwa namna ya ripoti na uwasilishaji wa ripoti. Hakika ripoti ya Mwenyekiti leo imekwenda skuli, ni ripoti iliyokwenda skuli.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara ya mwisho katika majadiliano ya bajeti hii, tunafunga mjadala wa bajeti yote ya Serikali na ni bajeti ambayo inayojumuisha takriban hali yote ya fedha pamoja na uchumi wa nchi yetu, kwa kuwa Wizara hii ndio yenye jukumu hasa la kusimamia maendeleo ya uchumi lakini vile vile Wizara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa sababu Wizara inashughulikia na mipango ya maendeleo ya uchumi, lakini vile vile masuala mazima yanayohusiana na fedha. Naomba nianze na kipengele cha mipango na maendeleo ya uchumi.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunaingia katika miaka hamsini, tunafikia miaka hamsini tangu tujitawale lakini ndani ya miaka hamsini huu ni mwaka wa tatu wa uongozi huu wa Serikali ya tatu kwa uongozi huu wa Serikali ya awamu ya tatu. Kwa kuwa ni zaidi ya nusu ya kipindi lakini kwa kuwa ni kipindi sasa cha miaka hamsini nadhani wakati umefika wa kujitathmini, miaka hii hamsini lazima tuitumie kwa kujitathmini, tulikotoka, tulipo na tunapoelekea miaka mengine hamsini ni wakati muafaka na mimi naomba nitoe rai kwa Wizara, katika kusherehekea miaka hamsini basi iandae kama ni kongamano, kama ni namna yoyote lakini linalohusiana na Zanzibar ilipo sasa kuangalia tunakotoka na tunakoelekea, suala zima la maendeleo pamoja na uchumi, ni wakati muafaka. Kwa hivyo napendekeza hilo lifanyike ili Wazanzibari wenyewe waweze kujitathmini na katika kujitathmini, naomba nianzie mimi binafsi katika mchango wangu huu.

Mhe. Naibu Spika, unapochukua muda tuliotoka tangu tujitawale kwa kipindi cha miaka 50 ukilinganisha na udogo wa visiwa vyetu kwa maana ya nchi yetu ya Zanzibar, ukichukua na wingi wa raslimali zetu, ukichukua na idadi tuliyopo kwamba hivi sasa tuko 123 milioni unaweza ukapata jawabu ukaona kwamba hali ya maendeleo ya nchi kwa kweli hairidhishi. Hiyo ukaichukua ukalinganisha na wenzetu ambao tuna muda sawa sawa tangu tupate uhuru pengine wao ni wengi zaidi, pengine wao wana raslimali chache zaidi tabaan utafika pahala utaona kwamba hali ya maendeleo ya nchi yetu bado haijaridhisha.

Lakini vile vile mbali ya maendeleo ya nchi Mhe. Naibu Spika, utaweza kubaini kwamba hali ya kipato cha wananchi na ongezeko au utanuzi wa pato baina ya walionacho na wasionacho, maana yake hicho ni kigezo na ndio siasa iliyokuweko mwanzo na mwisho tukajiunga katika siasa ya ujamaa na kujitegemea kwamba lazima tufike pahala tuweke hali za wananchi sawa. Ukiliangalia suala hilo kwamba hali ya kipato cha wananchi kwa kulinganisha kati ya walionacho na wasionacho, utaona pengo hili takriban linakuwa halijifichi. Vile vile ukilinganisha na hali ya ukuaji wa uchumi kama tunavyoambiwa kwamba unakua kwa asilimia 7 nukta hailingani kabisa na hali ya ukuaji wa uchumi na hali halisi ya maisha ya wananchi wa kawaida. Sasa katika hali hiyo Mhe. Naibu Spika, unaweza ukajiuliza hali hii inasababishwa na kitu gani?

Kwa maoni yangu Mhe. Naibu Spika, nadhani hali hiyo imesababishwa kwamba kwanza hatujaweza kuzitumia kikamilifu raslimali tulizonazo. Zanzbar tunazo raslimali, bahari ni raslimali kubwa sana na watu wameitumia bahari katika kujiletea maendeleo katika nchi. Zanzibar tuna raslimali ya ardhi, bahati nzuri sana ardhi ya Zanzibar ni ardhi inayozalisha, tofauti sana

kuna nchi ambazo ardhi zao hazizalishi lakini Zanzibar hakuna zao hata moja lisilozalisha.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba bado hatujaweza kutumia raslimali tulizonazo lakini bado hatujaitumia Zanzibar katika *geographically position* yake ilipo. Mwenyezi Mungu kuviteremsha visiwa hivi pahala hapa vilipo Mhe. Naibu Spika, hiyo ni sababu moja ya uchumi wa kutosha lakini bado hatujatanabahi na bado hatujalijua hilo kwamba tuko katika *position* ambayo kama laitani tutaitumia vizuri *position* hii wanajiografia wanajua kwamba Zanzibar tuko katika bahari ya Hindi katika eneo ambalo takriban ukingo wote wa bahari ya hindi kutoka Durban mpaka Somalia ya juu Zanzibar tuko katika *position* nzuri sana.

Lakini vile vile ukiacha mbali upande huu wa Magharibi ukija mashariki Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kumezungukwa upande wote wa mashariki. Mashariki ya mbali, mashariki ya kati na sehemu nyengine. Hivyo kweli hatuwezi kuitumia *position* hii katika kujiendeleza kiuchumi au katika kujenga uchumi wetu. Mimi naamini kama laitani tungeliweza kuitumia vizuri *position* yetu hii *geographically position* tuliyonayo basi tungelipiga hatua kubwa sana za kimaendeleo kwa sababu ni eneo ambalo tunaweza tukaunganisha Zanzibar ikawa ni kiunganishi kati ya nchi za Afrika, Afrika Mashariki na Kati, Afrika ya Kusini pamoja na Mashariki ya Kati.

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu hatujaweza kutumia vizuri vipawa na raslimali watu tulivyonavyo Zanzibar na leo ukiuliza hebu tuambiwe wataalamu tulionao wa Zanzibar ni wangapi, Zanzibar tuna wataalamu wa fani gani, jawabu utakaloambiwa kwamba Zanzibar tunao Wazanzibari wenye ma-*PhD* waliokuwa ni maprofesa ambao wanatumikana katika nchi mbali mbali za ulimwengu. Ile ni raslimali Mhe. Naibu Spika, unapomsomesha mtu mpaka akategemewa na mataifa mengine na wewe mwenyewe ukawa hujatanabahi kama ni raslimali yako hilo ni tatizo, tuiulize serikali yetu kuna wataalamu wangapi wenye fani gani na wanaotumika pahala gani. Naomba jibu hilo Mhe. Naibu Spika, serikali hii makini itakapokuja inijibu. Kwa sababu tunapozungumza raslimali hatuwezi tukazungumza raslimali nyengine kama gari na nini, raslimali inayotumika kubwa ulimwenguni ni raslimali watu iliyotanabahi, yenye elimu wanaofanya kazi wote wavumbuzi wa viwanda ni watu walio taalamika, Wazanzibari tunao. Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, serikali ijibu na kwa kuwa tayari tumeanzisha kitengo cha *DIASPORA* na tunakitengemea bajeti kwa kazi hiyo tu, naomba serikali kwa sababu ni eneo sasa hili tunataka kulitumia kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika eneo hili labda niseme pengine hatujawa na mipango mizuri au hatujaweza kuitekeleza kwa vitendo mipango mizuri tuliyonayo, vitu viwili pengine ama hatuna mipango mizuri au pengine hatujaweza kuitekeleza kwa vitendo hiyo mipango mizuri ambayo tunayo katika vitabu vyetu. Katika hilo unaweza kujiuliza tatizo nini?

Mhe. Naibu Spika, wataalamu walitwambia na wana siasa mahiri wa nchi hii walitwambia ili tuendelee tunahitaji mambo manne. Walitwambia tunahitaji tuwe na watu, siasa safi, uongozi bora na ardhi. Mimi binafsi nakubaliana na hoja kwamba tutakapokuwa na watu kama nilivyotangulia kueleza, tutakapokuwa na siasa safi, uongozi bora, ndio tutakavyoweza kuitumia vizuri ardhi basi hakika maendeleo hapo ni nje nje. Na tunapozungumzia watu tunazungumzia katika kuona ni watu ambao wana vipawa ndio maana ya watu, lakini tunapozungumzia watu tunazungumzia watu katika suala zima la nguvu kazi, hatuwezi kuzungumzia watu katika nadharia ya kwamba watu asubuhi hii sasa hivi wamekaa katika vijiwe na hawana kazi ya kufanya, huwezi ukazungumza watu katika hali kama hiyo. Ni watu wangapi wameajiriwa, watu wangapi wamejiajiri na watu wangapi ni wazalishaji wa uchumi wa nchi. Hapo ndipo tunapozungumza watu lakini tunapozungumza suala linalohusiana na siasa safi ni kwa maana ya kuwa na sera bora, sera zenye kulenga maslahi na maendeleo ya wananchi ndio maana ya siasa safi kwa maana ya sera, unaweza ukawa na siasa safi sera zako mbovu, sera hazitabiriki, sera zenye kuleta umaskini na njaa hapo huwezi kusema kwamba una siasa safi. Lakini tunapozungumzia suala la uongozi bora tunazungumzia katika kuwa na viongozi wenye *commitment* ya kuleta maendeleo, lakini vile vile suala la uongozi mbali ya *commitment* tunazungumzia suala zima linalohusiana na viongozi kuwajibika katika nafasi zao.

Suala la ardhi Mhe. Naibu Spika, wataalamu waliozungumza suala hilo la ardhi walizungumza katika mukhtadha wa kwamba ardhi ndio inayozalisha na ardhi ndio inayowekeza. Tujiulize ardhi yetu ndogo Zanzibar inazalisha kiasi gani kwa ajili ya uchumi wa nchi, lakini tunaitumiaje ardhi yetu ndogo Zanzibar katika suala zima la uwekezaji ambao unakuwa uwekezaji tija kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, kimsingi Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na nadharia hiyo kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne. Mimi kwa fikra yangu kwamba mambo yote hayo manne kwa upande wetu tuna matatizo nayo bado hatujakamilika katika maeneo yote manne. Watu wapo lakini idadi kubwa ya watu hawana ajira, ardhi tunayo lakini mpaka leo tunapozungumza katika chombo hiki bado hatujawa na ardhi, *management* nzuri na matumizi ya ardhi yetu, hatujawa na tatizo hilo.

Lakini jengine ni suala la viongozi, tunao viongozi lakini viongozi wetu tulionao ni viongozi kusema tu, ni viongozi kulalamika tu, hakuna viongozi

ambao wana *commitment* ya kikweli kweli, viongozi tulionao bado hawajawa na utashi wa kuwajibika, hivyo hatuwezi tukaendelea kama hatujabadilika.

Mhe. Naibu Spika, sasa tufanyeje, ukiacha mbali matatizo yaliyomo ndani ya kero za muungano kwa sababu naomba niseme kwamba tunapoutaja muungano na vikwazo vya muungano tunataja kwamba vikwazo vilivyomo ndani ya muungano vinaleta tatizo kwa uchumi wa Zanzibar, tumekuwa tukilizungumza hilo katika Baraza hili na sehemu mbali mbali kwamba kero zilizomo ndani ya muungano zinasababisha usumbufu mkubwa katika maendeleo ya uchumi kwa nchi yetu. Naamini kwa kipindi hiki ambacho sasa hivi tuko katika mchakato wa Katiba, Wazanzibari wataitumia vizuri fursa hii kwa sababu ni fursa pekee ya kuweza kutokana na tatizlo hili, naamini kwamba mambo yatakwenda vizuri baada ya mwaka mmoja tukijaaliwa unaokuja mbele kufuatia mchakato wa Katiba.

Lakini ukiacha mbali na suala la vikwazo vilivyomo vya kimuungano Mhe. Naibu Spika, bajeti hii aliyoiwasilisha Mhe. Waziri leo ilikuwa ije na jibu juu ya namna ya kufanya mapitio juu ya sera za kiuchumi na mipango ya maendeleo katika nchi yetu, tulitaraji sana mimi binafsi nilitaraji sana, kwamba bajeti ya leo hii ikiwa ni bajeti ya tatu itakuja na majibu juu ya yale yanayohusiana na mipango pamoja na mapitio ya sera za kiuchumi na mipango mengine ya kimaendeleo hasa katika maeneo manne hayo nitakayoyazungumza.

Kwanza suala zima la uwekezaji katika eneo la vyanzo vya mapato. Mhe. Naibu Spika, vyanzo vyetu vya mapato tulivyonavyo ni vichache mno na hatuwezi tukakuza uchumi wetu sasa kwa kuendelea kuvitegemea vyanzo tulivyonavyo, ni vyanzo ambavyo tayari tushavikamua na havina tena uwezo, tunaweza tukafikiria kuongeza kodi na tukafanikiwa ndani ya muda mfupi lakini hatimaye tukapata athari kwa muda mrefu unaokuja kwa kutegemea vyanzo hivi. Kwa hivyo, ili tujikwamue na uchumi kwa vyovyote vile iwavyo tunahitaji sasa kuwa na vyanzo vipya vya mapato katika nchi yetu.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, tulitegemea bajeti hii ije na jawabu juu ya namna ambavyo tunaweza tukaifanya *private sector* kuwa ni *by brand*. Hakuna uchumi wowote duniani ulioendelea pasipo kuitegemea *private sector* lakini sio *private sector* hii tunayoizungumza. Lazima tuwe na sekta binafsi ambayo inawezeshwa na inajengewa mazingira mazuri sana ya kusaidia uchumi wetu, ukienda takriban nchi zote maana yake mawaziri wetu sisi ni mabingwa sana wa kusafiri na mimi naamini katika safari zao hilo watakuwa wanaliona kwamba chumi zote katika nchi zilizoendelea na zinazoelekea kuendelea basi zinaitegemea sana sekta binafsi. Sasa leo serikali mara zote huzungumza kwamba *private sector*, lakini inazungumza kinadharia tu, bado

hakujawa na mipango hasa ama mikakati madhubuti ya kuiwezesha sekta binafsi ikawa ni sehemu ya kujenga uchumi wa nchi yetu. Nilitaraji kwamba bajeti ya Mhe. Waziri ije na mpango kamili na sio hadithi.

Mhe. Naibu Spika, eneo la tatu ambalo nilitegemea kutoa jawabu ni suala zima la kuwa na mpango wa ukusanyaji na udhibiti wa mapato katika eneo hili tuna matatizo. Katika suala zima linalohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato Mhe. Naibu Spika, tuna matatizo, serikali ilikuwa ije na jawabu juu ya kulidhibiti eneo hilo.

Eneo jengine nilitaraji kwamba mpango tulionao Mhe. Naibu Spika, ni mpango wa MKUZA. MKUZA ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Ingawa juzi nilishangaa sana kwa kweli nilikuwa sipo lakini nilishangaa sana, kwamba mpango wetu wa taifa ni huu kukuza uchumi na kukuza kipato cha wananchi, ndio *package* hiyo iliyomo katika MKUZA lakini utapozungumzia kukuza uchumi na kuongeza kipato cha wananchi wakati huo huo ukaleta kuku hapa sekta hiyo ya uzalishaji inakuwa hai-*reflect* na haiendi pamoja na sera hii ya taifa, unawezaje ukakuza kipato cha wananchi lakini unawaruhusu wafanyabiashara wachache kwa kutegemea tu kwamba watu wale, lakini huangalii kitu kile kitaathiri watu wangapi na mapato mangapi, unaangalia upande mmoja tu kitu ambacho si sahihi kwa kuangalia na *policy* ya sera ya MKUZA. Kwa vyovyote vile hatuwezi kuzuwia kwamba watu wasilete kuku lakini kwa vyovyote vile serikali ingeliangalia sera zake na kuangalia kwamba ikiwa *policy* yetu sisi ni kuhakikisha watu wetu wanapata kipato, basi unatengeneza mazingira ili wazalishaji wa ndani wazalishe. Yalizungumzwa juzi lakini leo nilisema pale tulikwenda kinyume kabisa na sera yetu ya serikali sera ya taifa ya MKUZA.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba katika hali ya kutoka katika hatua moja kwenda hatua nyengine, katika hatua ya kutoka kwenye uduni kuelekea kwenye maendeleo tunajiona kwamba tuko katika kipindi cha mpito. Kwa vyovyote vile kwa sababu tuko katika kipindi cha mpito Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ingelikuwa ina malengo mahsusi iliyojipangia na kama ingelikuwa ina malengo mahsusi iliyojipangia katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwa vyovyote vile serikali ingelikuwa ina vipaumbele. Inaonekana serikali yetu haina vipaumbele mtu tu, analala asubuhi awamu inakuja lakini hakuna kitu tulichokiweka kwamba hiki ni *target* ndani ya mwaka huu, hiki ni *target* ndani ya miaka mitano, kazi yetu sisi tunachukua vitu vingi kwa raslimali chache hatuwezi tukafika tulikokusudia.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda wako naomba nimalizie dakika zangu tatu kwa kusema hivi kwamba tuna tatizo katika ukusanyaji na matumizi ya fedha ya umma, na katika hilo basi tulimtaraji Mhe. Waziri

angelikuja hapa akatwambia kwamba lazima tuimarishe mfumo wetu wa ukusanyaji kwa sababu mfumo wetu wa ukusanyaji wa mapato una mapungufu. Mhe. Naibu Waziri naomba nikwambie kwa mkato sana tuna tatizo katika suala zima la risiti, hadi leo tunapokwenda katika taasisi za umma serikali haina utaratibu maalum wa risiti. Risiti zinapochapishwa zinaruhusu wizi kwa sababu hakuna *security* lakini vile vile malipo hadi leo kuna baadhi ya taasisi zinafanya malipo kwa kupokea risiti za mchele. Tuna tatizo katika ukusanyaji wa mapato, lakini vile vile tuna matatizo katika ukadiriaji wa mapato.

Jengine Mhe. Naibu Spika, tuna mapungufu katika matumizi ya fedha za umma ni tatizo na hili mimi nilikuwa nizame kwa undani sana, lakini kwa sababu ya muda wako sitakwenda mbali. Ninachotaka kusema kwamba hadi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali, ahadi hizi ambazo zitawasilishwa karibuni bado zinaonesha kwamba tuna matatizo makubwa katika matumizi mazima ya fedha za umma. Mhe. Naibu Spika, hivi tutafika lini tuone kwamba tunapunguza haya matatizo kama ikiwa kila siku ripoti zinajirudia jirudia Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hataki kuchukua hatua sasa itabidi tumchukulie yeye, kama ameshindwa kuwawajibishwa watendaji wizi hatuwezi kustahamili tena katika kuliona suala hili.

Lakini jengine katika hilo ili tuimarishe mfumo wa ndani Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri anielezee alivyojipanga sasa kuwezesha wakaguzi wa ndani kuwawezesha kibajeti, kwa sababu hatuwezi tukawa na udhibiti wa fedha kama tukiwa hatujaimarisha ukaguzi wa ndani katika taasisi zetu. Hadi leo tunavyozungumza wakaguzi wa ndani ambao wanatakiwa popote pale inapokwenda fedha na wao wende hadi leo hawana bajeti. Lakini vile vile tulizungumza suala hili kwamba haiwezekani wakaguzi wa ndani wakaripoti kwa Mhasibu Mkuu, lazima na wao wawe na idara yao inayojitegemea. Mhe. Waziri atakapokuja naomba anieleze.

Lakini chengine cha mwisho katika hilo tuna tatizo katika sheria zetu, sheria za fedha, sheria za manunuzi zina mapungufu Mhe. Waziri atakapokuja naomba aje anieleze. Mwisho naomba niseme kwamba Zanzibar tuna idadi ndogo sana ya watu tutakapokuwa na mipango mizuri na sahihi Mhe. Naibu Spika, hapana shaka tutaendelea. Ninachoomba viongozi wasiishie tu kulalamika na kuonesha kwamba wao wanakerwa na rushwa. Sasa naomba viongozi wawajibike na wachukue hatua za vitendo sio kiongozi kuja akatwambia mimi nachukizwa na rushwa lakini hachukui hatua kwa kweli hatuwezi kumfahamu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuwa mchangiaji wa nne leo hii siku adhimu tunayoelekea ukingoni mwa shughuli yetu hii ya kuwatumikia Wazanzibari na Watanzania kwa umoja wao.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwatakia kheri na mafanikio ya funga na malipo mwanana Waislamu wote wanaoendeleza ibada hii ya funga ya Mwezi Mtuku wa Ramadhani. Inshaallah MwenyeziMungu azitakabalie funga zao na sala zao na dua ili tupate mafanikio mema Inshaallah.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nataka nianze kusema kwamba tumefanikiwa kwa sababu Mwenyezi Mungu anawapenda waja wake na kwa sababu hiyo, kila taifa kulipa raslimali ili iweze kutumika kwa faida yao na maslahi ya hilo taifa lao. Mhe. Naibu Spika, tumefanikiwa kuwa na visiwa vilivyobarikiwa, idadi ndogo ya wakaazi wake, tukazungukwa na bahari iliyojaa tuvijuavyo na tusivyovijua hadi sasa, akatupa ardhi ndogo yenye rutba nyingi.

Mhe. Naibu Spika, tuitumie bahari hii tupite juu tusafiri, twende tukavue lakini tuvue mvuo wa kileo, lakini twende chini ya ardhi tukavitafute vilioko huko chini kwa faida ya nchi hii. Kazi hiyo bado haijafanyika, ni imani yangu kwa umahiri mkubwa wa swahiba mufti wangu, ndugu yangu Mhe. Omar Yussuf na timu yake wanao uwezo wa kuyapanga haya na Mungu akiwawezesha tukaweza kufanikiwa. Wasi wasi wangu Mhe. Naibu Spika, ni mmoja na ni mkubwa sana wapi wenzetu hawa wataweza kupenya ili waifikishe Zanzibar huko tunakokutaka.

Nasema hilo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu uchumi wa nchi yoyote ile unasimamiwa na Benki Kuu ya nchi hiyo. *Monitoring*, *supervision* ya uchumi mipango ya nchi ni Benki Kuu. Benki Kuu imetwambia haiwezi kusimamia chumi mbili ndani ya nchi moja. Tokea jibu hili nilipolipata kutoka mdomoni mwa mkuu wa benki hiyo, nilikuwa na wenzangu akina Mhe. Salmin Awadh tuliondoka na baridi kali ya hofu kwamba kumbe bado tumekabiliwa na kazi nzito.

Mhe. Naibu Spika, hebu Mhe. Waziri atukonge nyoyo zetu atafanyaje ili dhamira hii na mikakati hii ya kiuchumi kuondoa ama kupunguza umaskini uliyokithiri wa wanyonge wa nchi hii. Siku moja itakuwa ni hadithi, tutapenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, mazuri na muhimu yamezungumzwa na wenzangu waliokwishatangulia lakini kwa namna ya pekee naomba nimuombe sana Mhe. Waziri hii tozo ya simu za mkononi imezungumzwa pamoja na wewe

ukiwemo ama lilikuwa la kule upande wa pili wa ndugu zetu peke yao. Sababu iliyotajwa ya maji kuna wenzangu kule Bungeni wamo humu ndani ya Baraza hili, suala la maji tayari limeshatengewa fedha yao na leo imetajwa tozo ya simu kwamba ni kwenda kusukuma harakati za maji vijijini. Je, sisi hapa hatuna tatizo la maji lakini wenzangu wamesema tozo hii imalizie Chumbe. Mimi niseme kama ishaingia huku juu *ZRB* wakusanye tozo hii kwa faida na maslahi ya Zanzibar yetu.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na Idara ya Kuweka Hali za Wananchi Sawa, ilikuwa inakwenda sambamba na maazimio na malengo ya mapinduzi ya nchi hii, hali za wananchi wetu ziwe sawa. Mzee Karume amekufa na hii imo ndani ya kichwa chake na akiitekeleza kwa vitendo. Nilitaja raslimali bahari na nikasema ardhi ndogo tuliyonayo, Mzee Karume aligawa eka tatu tatu kwa wale ambao hawakumiliki ardhi wakati ule. Keshokutwa Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atufikishe tuione miaka 50 ya mapinduzi matukufu. Mhe. Naibu Spika, ilikuwa ni matarajio yangu tufanye tathmini ya miaka 50, halafu tujiulize kwa 50 itakayowakuta watoto wetu. Zanzibar tuliyoikuta mwaka 1964 tulio wengi na miaka 50 ya kesho 2014 iko wapi na 50 ijayo tutaipeleka wapi, kwenye nini ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia ambapo uchumi wake unategemea hiyo TEHAMA.

Mhe. Naibu Spika, katika hili nitamuomba ndugu yangu swahiba wangu mpenzi, tuna huu mkonga wa serikali, hebu aje atunyambulie nyambulie na sisi tupate uelewa. Hadi sasa kimatumizi umefikia wapi na tunatarajia kumalizika kwake utafikia kima kipi. Tunapata mashaka bado kitaalamu huu mkonga tunaona unazikwa karibu sana na barabara zetu tutakapohitaji matanuzi ya barabara haitatupa matatizo? Kwani hivi sasa kule Pemba linalozungumzwa baadhi ya barabara Wete – Chake Chake kwamba imekwama ujenzi mkonga huu ikitanuliwa barabara utafunikwa na barabara juu jambo ambalo litatishia mawasiliano ama litakapotokea *break down some where* ni tatizo litakuwa. Kwa hivyo, na mkonge kuhaulisha sasa unahitaji gharama kubwa ya milioni zisizopungua tano, hebu na hili uje unitoe mashaka mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Wete niweze kusaidia wananchi wangu kuhusu hili.

Mhe. Naibu Spika, tuna *ZIPA* lina jukumu kubwa kushajihisha wawezekazaji wa nje na ndani kuekeza, mbona tatizo lipo. Tatizo *ZIPA* wanafanyakazi kubwa kazi nzuri walioko kule wanaongozwa na ndugu yetu Dr. Salum Mwenyezi Mungu amjalie kheri na maisha marefu ya kheri aendelee kutusaidia. Lakini tumempa ng'ombe kamba tumekamata wenyewe. Mhe. Naibu Spika, hivi ni lini tutamkabidhi vyote viwili nitaomba jibu hili kwa Mhe. Waziri. Lini *ZIPA* tutawakabidhi ng'ombe kuchunga pamoja na kamba na lini ile *Stop Center* itafanya kazi kama iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, haileti maana hata kidogo, tunazungumza kitu kama kuna mwenzetu au wenzetu wana mawazo mengine tofauti ni vyema yaletwe kwenye meza ya majadiliano tumalize. *One Stop Center* ilipo sasa haimalizi masuala tunayotahitaji, wanapelekwa watu hawana maamuzi, wenye maamuzi bado wanabaki maofisini wafuatwe maofisini kwao. Hatuwezi kwenda kwa namna hii.

Mhe. Spika, Mfuko wa Hifadhi dhana mzuri sana na duniani kote inatumika. Ndugu yangu Mhe. Waziri mfuko huu ulianza hapakuwa na taaluma hata kidogo kwa wananchi lakini ukaja na ushawishi mkubwa nakumbuka na vipeperushi vitasaidia wanachama kwa mikopo, nini na kile tukaingia. Lakini kwenye safari Mhe. Naibu Spika, kuna kufika mwisho na kuna kukata kati kati. Kuna wafanyakazi hapa Mhe. Waziri naomba unisikilize sana ambao wamekatisha utumishi wao kabla ya miaka 60 na katika kukatisha huko sheria zimewaruhusu wafaidike na kile walichokiweka cha mfuko, mambo mawili, wapate kiinua mgongo lakini jengine ni pencheni.

Nina barua ya mfanyakazi mmoja ambayo kaacha kazi kwa mujibu wa sheria na kuachishwa kwake basi barua imemtaka hayo afanyiwe kwenye mfuko huu kwa sababu hajafikia umri na mfuko unasema ni mafao ya uzeeni. Huyu hajazeeka lakini hana kazi sasa, huyu hapati pencheni lakini hata kile chake kilichohifadhiwa na mfuko ambacho kinaekezwa kinazalishwa Mhe. Waziri inakuwaje yeye asifaidike nacho ni haki yake. Mimi siamini kwamba zimewekwa zimefungiwa tanuri zinatumika. Kutumika huko zinazalisha, nadhani ili kuhalalisha na huu mfuko uwe halali na yeye mwenye chake apate kasma.

Mhe. Naibu Spika, jengine nije ni *ZRB* niwapongeze kazi nzuri ya mafanikio yenye ufanisi pamoja na matatizo ya hapa na pale. Mhe. Waziri hebu ukija unambie hivi bado tumekwama wapi kazi ile ya *TRA* kwamba bado haijaweza ikafanywa na *ZRB*, ni swali tu kwangu nataka nipate majibu. Nina mashaka humu kichwani kwangu najiuliza mengi. Kwa sababu *TRA* inaambiwa ni kukusanya kodi hizi za muungano lakini pesa hizo wanazokusanya zinabaki hapa hapa wanapokusanyia. Hivi ni kwa nini basi zisikusanywe na *ZRB* za ndani na zipewe hilo hilo jina la muungano. Nadhani tunaongeza tu matumizi ambayo hayana ulazima hapa, kwa sababu ni mambo ya kitaalamu ndio nikataka Mhe. Waziri unisaidie kidogo.

Mhe. Naibu Spika, nije *PBZ* Mhe. Waziri nikupongeze kwa mara nyengine tena. Taasisi hii kwa udhati wa nafsi yangu nasema sijaiona nyengine ndani ya Zanzibar hii kwa utendaji wa shughuli zao kwa ufanisi mzuri. Na kwenye nidhamu ya utumishi wake ni wa hali ya juu mno. Mhe. Naibu Spika, pana

nidhamu ya hali ya juu mno *BPZ*. Hayo ni maoni yangu lakini nimewasikia na wenzangu wakisema. Kwa hivyo, ni haki yao tuwapongeze.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu hawa kama si umahiri mkubwa tena wa Baraza lako tukufu ambao ulioneshwa hapa tulitakiwa leo *PBZ* hii tuwe na hadithi nyengine. Nalishukuru Baraza la Wawakilishi niushukuru pia na uongozi na nashukuru Serikali ilitusikiliza kwa hili naishukuru na naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitusikiliza na ikatenda wajibu wake na leo *BPZ* tunayo na inafayakazi nzuri Mwenyezi Mungu aisaidie tufike kwenye malengo.

Mhe. Naibu Spika, tumeona imeongeza kiwango cha raslimali imekusanya mitaji ya wananchi na imekusanya mapato vizuri kufikia malengo, imeanzisha uhusiano na Benki ya Viwanda ya Biashara China, jambo zuri ambalo leo Wazanzibari wanafanyabiashara nyingi na kubwa Jamhuri ya China.

Hili pia litazidisha uhusiano wetu wa udugu wa karibu sisi na watu wa Jamhuri ya China, kuna mazuri mengi yamefanywa na yanaendelea kufanywa na benki yetu. Lakini zuri zaidi tawi hili la Benki ya Kiislamu. Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua wengine riba hii ya moja kwa moja ina mashaka yake hatuitaki na wenzetu ikawa wanakosa fursa wengine za kupata mikopo kwenye benki yao hii. Nashukuru kwenye sifa ile ile niliyoanza nayo ndani ya jitihada zao wamefungua eneo hili na sasa wale wote wanaotaka huduma ya *PBZ* ama kwa kulia wanaipata ama kwa kushoto ni uamuzi wako mwenyewe. Mhe. Waziri hongera sana katika hili na pia salamu zangu uwapelekee wenzetu huko wazidishe kamba.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nimuombe Mhe. Waziri kwamba nimeona humu kama wanataka kujitanua pia kwa mikoa mengine ya Bara. Ni vizuri tutafute soko tuongeze nguvu imetajwa Mtwara Kusini mwa Tanzania. Lakini hebu tutizame maeneo haya yana wakulima wakubwa na wanazalisha chakula kingi kwa mikoa ya Bara, hebu na wenyewe tutupe jicho huko tuone ni vipi tunaweza labda tukafanikisha jambo hili zuri ambalo litatuongeza na pia ule udugu wetu na wale wano ndoto ya mawazo ya hapa na pale hatutaki hili.

Sisi tunakwenda kufanya utafiti tuweze kujua tukae vipi na kuweka raslimali yetu kabisa haya halafu mkija kutwambia kwamba hatutaki muungano si kweli mnadanganyana. Muungano huu wetu sisi haukuja kwa siasa, muungano wetu ulianza siku nyingi, damu iliungana tena mambo ya siasa ni yenu wenyewe mnaunganisha hapo hatuna tatizo lakini kwa nini tunaamini ama kuwekeana raslimali ni udugu.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili leo si pake, nilitaka nithibitishe kwamba hatuna matatizo na ndugu zetu tusichonganishwe, tunataka tu mambo yetu yaende sawia haki za Wazanzibari zieleweke zifafanuliwe na zipatikanwe, haki za wa Bara zipatikane na zijulikane tuendelee na mambo yetu. Hili ndio kubwa Wazanzibari wanataka yao yaeleweke wasibinywe binywe na yasiingiliwe. Mhe. Naibu Spika, unapofikia umri hata deni tunaamini wengi kila mmoja kusimamia chake si jambo la aibu wala si haramu. Kwa hiyo, isitafsirike vyenginevyo ikakorogwa korogwa ikaingia sitofahamu katika hili, hakuna tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kuna mfuko wa pamoja wa fedha baina ya Zanzibar na wenzetu wa Bara. Mhe. Waziri sasa ni umri mkubwa tunaambiwa Zanzibar tumeshamaliza mambo yetu siku nyingi tunawapelekea wenzetu tunawasubiri hii, tunasubiri hadi lini. Swali langu hivi tunasubiri hadi lini? Kama kuna tatizo Mhe. Waziri haiwezekani basi isiwezekane twende kwenye hilo jengine. Lakini Mhe. Naibu Spika, tumeweka watu kwenye eneo hili watu na elimu zao za hali juu sana, watu mashahuri watu muhimu sana wana uwezo mkubwa wa kuisaidia na kuishauri Serikali zote mbili na kazi hiyo walikwishaifanya kwa taarifa nilizonazo.

Sasa kikwazo kiko wapi, ndipo nikasema Mhe. Waziri kama kuna ugumu wa jambo hili basi, lakini wale wenzetu pale ndani wanaumiza vichwa vyao bure kumshauri mtu ambaye hashauriki, kumshauri mtu ambaye hataki. Mhe. Naibu Spika, utampeleka farasi kwenye mto kama maji hayataki katu abadani hayanywi.

Naomba nimalizie kwa la mwisho Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ndugu yangu Wazanzibari tuna umaskini mkubwa mno wa kutisha, wananchi wetu wanaishi maisha mabaya mno. Hebu wenzetu kaeni mtafute namna ya kutusaidia ili waweze kutumia nguvu zao wapate vipato vyao halali kufuatana na raslimali tulizonazo na raslimali zipo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu iliwasilishwa kwetu na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwanza nimpongeze sana kwa kutuwasilishia hutoba yake hii ya makadiro na mapato ya matumizi ya fedha kwa mwaka huu wa 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitaipongeze wizara hii ambayo ni wizara yangu mama na ni wizara yangu mama kwa kuwasilisha bajeti yake hapa mbele yetu Baraza la Wawakilishi na kuwashukuru pamoja

na watendaji wake akiwemo Katibu Mkuu wa wizara hii pamoja na Makamishna wake na Manaibu wake kwa kutuwasilishia kazi hii nzuri ambayo kama tukiwa ni Wajumbe wa Baraza hili tukufu basi ni kujadili na mwisho wake kupitisha.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba ina majukumu makubwa ya kusimamia mapato na matumizi ya Serikali pia kusimamia kupunguza umaskini na kusimamia uchumi na mipango ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wizara hii ina majukumu mazito na mengi na kwa sababu Wizara ya Fedha, ndio kila kitu bila ya fedha huwezi kufanya kitu chochote. Kwa hivyo, wizara hii ni muhimu na kwa vile ni muhimu yale ambayo yote yameingizwa katika kitabu hiki ni mambo ambayo ni muhimu sana na ni lazima kama Wawakilishi kuyajadili na halafu tuyapitishe. Lakini kwenye suala la kusimamia sheria za matumizi na sheria za manunuzi. Mhe. Naibu Spike, kwa kweli kwenye sheria hizi, sheria tunazo lakini kunakuwa na mapungufu ya utekelezaji wake. Kwa hivyo, ningeomba kama wizara hii ndio msimamizi wa matumizi ya fedha za umma pamoja na manunuzi, ni juu yao kusimamia kwa maeneo na taasisi mbali mbali kuona kwamba sheria hizi zinatekelezwa kwa ufanisi ili lengo lifikiwe.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki Mhe. Waziri amesema kuna changamoto za kuchelewa kufunga hesabu, hili ni tatizo kubwa na ningeiomba wizara hii kwa kupitia taasisi mbali mbali ikasimamia matatizo haya ya kuchelewa kufanya hesabu za Serikali. Iwapo tutachelewa kufunga mahesabu ya Serikali basi Serikali itakuwa haina uhakika wa mahesabu yake.

Mhe. Naibu Spika, nikienda Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali niseme kwamba idara hii ina majukumu na sio pale ndani tu na hata taasisi ambazo zina wahasibu. Kwa hivyo, ningeomba taasisi iwasimamie wahasibu na kuwapa elimu ili tuweze kupata ufanisi katika sehemu zetu mbali mbali. Pia hapa Mhe. Waziri nione kwamba kuna kitengo kimoja hichi cha *Internal Auditors*. Kwa kweli kitengo hiki kinahitaji sasa kiwe kinajitegemea wenyewe kwa sababu tunaona kwamba kuna mapungufu ya *Internal Auditors* ni kwamba anakuwa chini ya Katibu Mkuu. Kwa hivyo, kama atakuwa yeye mwenyewe anajitegemea kwa kweli ripoti zake zitakuwa na uhakika wa kufanyiwa kazi kama atakuwa na *Internal Auditors*. Kwa hivyo, tungeomba kama sheria haipo basi ipitishwe kuanzishwa kwa kitengo hiki. Vile vile Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye kitabu hiki ukurasa wa 26 kuna Idara ya Bajeti. Idara hii ni muhimu sana kwa sababu inashughuli za kuratibu shughuli za kibajeti kuhakikisha kwamba wizara na taasisi za Serikali zinatekeleza bajeti kulingana na mfumo wa *MTEF*.

Mimi nasema kama tutakwenda na mfumo huu kwa sababu mfumo huu ni sawa sawa na mpango kazi na vile vile unafafanua matumizi ya kila kitu na bei zake. Kwa hivyo, hakutokuwa na matatizo ya hapa na pale kwamba kutajitokeza mambo yatakayokuwa yanahitaji pesa kwa kupindi kile isipokuwa yale ambayo umeyapanga katika ule mpango wako wa *MTEF*.

Mhe. Naibu Spika, nikienda mbele kuna Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ina jukumu kubwa la kusimamia mali za Serikali. Kwa hivyo, niseme kwamba idara hii pale inasimamia mali zote za Serikali na vile vile kusimamia kupata hati miliki na kuhakikisha kwamba sekta inakuwepo ili kuepuka upotevu wa mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye Bodi ya Mapato ni taasisi muhimu kwa sababu ni taasisi ambayo inakusanya mapato yote ya Serikali. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na *co-ordination* baina ya zile taasisi zinazokusanya ndani ya mawizara na vile vile kuzikusanya pamoja katika kuziona kwamba pesa hizi hazivuji kutokana na watu ambao hawako na uwazi katika kukusanya mapato hayo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye Mfuko wa Barabara una jukumu la kazikarabati njia mbali mbali katika visiwa vyetu hivi. Vile vile kianzio chake kinaonesha kwamba ni kianzio kimoja kinachotokana na *petrol levy* ambayo nayo vile vile kama alivyosema mwenyekiti kwamba inaonekana pesa hizi zinakusanywa kutoka *ZRB*. Mimi niseme kwamba fedha haina mabwana wawili. Kwa hivyo, ni lazima ilibadilishwe hii kama kuna sheria au jambo lolote basi Mhe. Waziri ili kuuletea ufanisi mfuko huu wa barabara basi kuwe na uwezekano wa kukusanya wenyewe mapato haya.

Vile vile nikienda na Hifadhi ya Jamii Mhe. Naibu Spika, mfuko huu ni mfuko ambao unaweka fedha za wafanyakazi mbali mbali ili kuja kuwalipa hapo baada ya kustaafu. Lakini Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii kuna wafanyakazi ambao sasa labda kwa maana ya kuachishwa au pengine uajiri wao umemalizika, basi ningeomba wizara ikawalipe mafao yao kwa sababu kadri wanavyokwenda na fedha itakuwa haina thamani kama sasa hivi ameachishwa kazi, kwa maana yoyote ile basi hapo baadae haitomsaidia kwa sababu ya ile kushuka kwa thamani ya ile pesa yenyewe.

Ningemuomba Mhe. Waziri aombe au kama kunakuwa na sheria kwa sababu hivi sasa ukenda kudai pesa unaambiwa hupewi na vile vile kwamba fedha hizi zinafanyiwa biashara na kwa kuwa biashara ni kitu cha makubaliano unapoifanyia biashara pesa ya mtu, basi angalau muwe mmekubaliana. Ina maana hapa wanafanya biashara ambayo watu hawajakubaliana nao na vile vile niumuulize kwenye biashara hii ina maana kwenye kufanya biashara

mgawane mapato. Sasa sijui hapa kama biashara hii inapofanywa kuna *income* yoyote ambayo ataipata yule aliyeweka fedha zake.

Kwa hivyo baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, kwa naiba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hoja hii asilimia 140.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nataka kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache katika Bajeti hii ya Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika kufuatilia bajeti ya Mhe. Waziri na mimi nataka nianze katika ukurasa wa 22 wa kitabu hichi kinachozungumzia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.
Mhe. Naibu Spika, mimi hapa kwanza nataka niwapongeze kwa kazi nzuri wanazozifanya lakini vile vile nataka nitoe angalizo.

Mhe. Naibu Spika, tumepata taarifa na kwa sababu Idara hii ndio inayoshughulikia masuala mazima ya kulipa mafao ya viinua mgongo lakini vile vile pamoja na pencheni.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu nimekuwa nikuzungumzia suala hili tokea bajeti ya mwaka 2011 kuhusu suala zima la wafanyakazi hewa na mishahara hewa. Suala hili Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kuna dalili kwamba lipo, kwa hivyo naomba sana idara hebu iwajibike ili kuhakikisha kwamba hakuna upotevu wa fedha za umma.

Mhe. Naibu Spika, haya nataka niyazungumze kwa sababu upo ushahidi ambao unaonesha kwamba kuna watu ambao wamefanyiwa tathmini ya viinua mgongo kinyemela na ile mishahara yao ya mwisho ambacho ndio kigezo kinachotakiwa kufanyiwa tathmini ya kiinua mgongo. Sasa eneo hili Mhe. Naibu Spika, inawezekana mtu alikuwa akipata mshahara wa mwisho tuseme laki tatu. Kwa hivyo, ina maana mshahara wake utafanyiwa mahesabu kwa mujibu wa kile kigezo kile cha laki tatu. Lakini kuna baadhi yao inaonesha kwamba kuna mtu anamalizia mshahara kazini mshahara wa laki tatu, basi kiinua mgongo chake kinafanyia cha laki tano. Kwa hivyo, hii haitoathiri tu kumpatia kiinua mgongo kikubwa lakini vile vile itaathiri mpaka katika kumpatia na pencheni yake. Kwa hivyo, utakuta kuna fedha nyingi hapa za umma zitakuwa zinatokea bila ya utaratibu. Hili sitaki nilisema sana kwa sababu tumeshatoa agizo kwa Afisa Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali na tunawashukuru hiyo kazi imeanza tumesikia katika vyombo vya habari wameanza katika Wizara ya Elimu kuangalia namna gani ya upoteaji wa mishahara.

Sasa hapa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri rafiki yangu na kaka yangu namuomba sana ajitahidi sana kulisimamia zoezi hili kwa sababu yeye ni mtu ambaye katika mawaziri tunawashukuru anatwambia kuwa tumuoneshe hiyo mianya ili na mimi nione ili kapu yangu inone ili niweze kuwatononosha na watendani wengine wa Serikali lakini pamoja na wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, eneo hili namuomba sana Mhe. Waziri ashirikiane sana na Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na awape *support* yoyote wenzetu wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali, Wizara ya Fedha itoe *support* yote ili kuhakikisha kwamba kwamba wanafanya hili zoezi la uhakiki. Lakini vile vile kuhakikisha Mhe. Waziri kama bado kuna wafanyakazi wa serikali ambao hawapokei mishahara yao benki, basi mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, hili tatizo litaendelea kuwepo.

Mhe. Naibu Spika, tulipofanya ziara ya kimasomo nchini China, kimoja walichotueleza kwamba sisi tulikuwa tunafikiria kwamba China hakuna upotevu wa fedha za umma, kumbe hata kule upotevu wa fedha za umma upo lakini lilitoka agizo na kwa bahati nzuri wenzetu linapotoka agizo linatekelezwa hapo hapo, kwamba wafanyakazi wote wapokelee mishahara yao benki. Kwa hivyo, wale ambao walikuwa wanafanya ujanja na ukwepaji basi walifika pahala wakashindwa njia ya kupenya. Kwa hivyo suala hili nilikuwa naomba sana Ofisi yetu ya Mhasibu Mkuu wa Serikali wajitahidi kulisimamia ili kuondokana na huo udanganyifu na upotevu wa fedha za umma zinazotupotea.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nikiendelea katika Idara ya Uhakiki Mali. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana. Hapa tunashukuru ipo programu ambayo wanasimamia hili daftari la mali za serikali. Kimsingi Mhe. Naibu Spika, kuna mashamba ya serikali mpaka leo hayajulikani, kwa hivyo mali za serikali ziko nyingi, tunaomba basi hili zoezi waliharakishe ili kuhakikisha kwamba serikali inajua zile *assets* zake.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niendelee katika Idara ya Bajeti, wameelezea hapa malengo yao na utekelezaji wa shughuli zao. Mimi naomba sana Mhe. Waziri kwamba idara hii uipe *support* kwa sababu wao ndio wanaosimamia utayarishaji wa hizi bajeti ambazo baadae zinaletwa hapa, wenzetu hawa wanafanyakazi kubwa na ngumu.

Pia nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wa idara hii wahakikishe na zile fedha zinazoingizwa katika zile taasisi wanafuatilia na matumizi yake vile vile. Imeelezwa hapa kwamba kuna hii sheria ambayo tumeipitisha ya utaratibu wa matumizi ya fedha za umma. Mhe. Waziri hapa amekiri kwamba bado kuna maeneo ambayo zile taratibu haziendelei kufuatwa. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba kwa kuwa Mhe. Waziri hili

amelitaja yeye mwenyewe kabla ya kulitaja sisi basi naamini uwezo wa kulisimamia atakuwa nao mkubwa. Mimi nilikuwa najaribu tu kumpa changamoto ili azidi kuzidisha hizo jitihada zake ili kuhakikisha hilo suala wanalisimamia vizuri.

Mhe. Spika, vile vile katika hii Idara ya Mipango na Sera kwenye ukurasa wa 37. Mhe. Naibu Spika, samahani ukurasa wa 37 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, nilikuwa nataka nipate taarifa kuhusu lile jengo ambalo lilikusudiwa kujengwa Wizara ya Fedha kule Pemba liko hali gani, litasukumwa lianguke au litasogezwa mbele au atatafutwa mshauri mwelekezi. Maana yake sasa hivi washauri waelekezi wako wengi, kila tunapoharibikiwa tunatafuta mshauri mwelekezi azidi kutumia fedha nyingi zaidi. Mhe. Waziri anacheka pale! Kwa hivyo, mimi nadhani pale ni lazima maamuzi magumu ya serikali yafanyike. Aidha, livunjwe au lifanyiwe ukarabati kama inawezekana ili wenzetu Wizara ya Fedha kule Pemba waweze kupata jengo ambalo litaweza kuwasaidia.

Vile vile Mhe. Waziri hapa ameelezea katika suala zima la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti wanakusudia kufanya marekebisho ya sheria ya *ZSSF*. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba, ZSSF kuna wafanyakazi wengi wanakuja kutulalamikia, hasa wale wafanyakazi wanaofanyakazi za mikataba, wanakuwa bado vijana wanafanyakazi na inatakiwa kwamba mpaka ufike umri wa kustaafu ndio uweze kupata mafao yako, lakini wanatulalamikia wanasema kwa nini wenzetu kule Tanzania Bara kwamba kuna mifuko ya Hifadhi ya Jamii sasa hivi mingi, na wenzetu kule wana uwezo wa kwenda kukopa fedha zile na kufanyia shughuli zao nyengine. Lakini vile vile hii mifuko inawajengea nyumba wale wadau wake au wateja wake sio kuwajengea nyumba kama za kuwagaia. Lakini inawakopesha katika mkopo wa bei nafuu na ile imekuwa kama upatu, zile ni fedha zao wafanyakazi wa serikali pamoja na taasisi binafsi wamechangia wameweka pale. Kama ni upatu ingekuwa angalau wanakopeshana kujengeana nyumba wenyewe kwa wenyewe halafu wanajilipa.

Lakini wao wanasikitika wanasema kwamba *ZSSF* wanajenga viwanja vya kufurahishia watoto, wanasema sisi kule hatuendi kulala, tunataka nyumba za kulala ili tuweze na sisi kuhakikisha kwamba zile fedha tulizoziweka kama akiba yetu zinatusaidia. Kwa hivyo, tunawapongeza kwa kujenga kiwanja cha watoto na pia wana mpango mwengine wa kujenga kiwanja cha kufurahishia watoto kule Pemba. Lakini waje na mpango sasa hivi wa kuboresha makaazi ya wananchi wa Zanzibar na hii ndio itakuwa hasa wanatekeleza ile sera ya muasisi wetu wa mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Abeid Amani Karume kuwapatia wananchi huduma za kijamii yakiwemo makaazi bora. Sasa hili nilikuwa naomba sana Mfuko wa Hifadhi ya Jamii waliangalie.

Mhe. Naibu Spika, hapa hapa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nilikuwa naomba sana. Nilikuwa nasikia tu kuna mpango, labda Mhe. Waziri atakuja kunieleza kushirikiana na *Islamic Bank* kwa ajili ya kuanzisha hii mikopo ya ujenzi wa nyumba. Sasa hivi Mhe. Naibu Spika, wanatoa mikopo ya ujenzi wa nyumba lakini bado ile mikopo ina masharti magumu. Kwa mfano kama mimi hapa nikitaka kwenda kukopa ili kuendeleza ujenzi wangu, inabidi lazima wachukue kigezo cha kulipa kwenye mshahara wangu, kitu ambacho inakuwa sio rahisi kwa mtumishi moja kwa moja ambaye anaweza kufanya na njia zake nyengine zinazoweza kumuingizia mapato kuweza kurejesha yale mapato katika kipindi kifupi.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, hii mikopo wanayotoa ya ujenzi wa nyumba. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, yako mashirika ya kimataifa, ziko taasisi za kimataifa wawasiliane nao basi ili kuweza kupata hizo *fund* kwa ajili ya kujenga nyumba. Wenzetu wanakopeshwa nyumba miaka mpaka 30 watu wanalipa kidogo kidogo. Suala hili nilikuwa naomba *ZSSF* washirikiane na hizi benki zilizokuwepo hapa ili kuweza kuboresha makaazi ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA)*. Hapa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie kwanza mimi bado siridhiki kuona kwamba mpaka leo Zanzibar, taasisi hii au chombo hiki kinaongozwa na Naibu Kamishna.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani kuna Makamishna karibu wanne Tanzania, lakini leo Zanzibar ikiwa kama sio mkoa, hii Zanzibar ikiwa kama ni nchi tuna Naibu Kamishna. Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine hata haya mambo ya kodi, wafanyabiashara wanaolalamika kutozwa ushuru mara mbili kwa sababu hizi kodi zinakwenda katika maamuzi, kwenye *TRA* kuna ile Bodi ya *TRA*. Sasa Mhe. Naibu Spika, ikiwa kama kuna makamishna wao ndio wanaopanga kodi. Naibu Kamishna pale atakuwa na uwezo gani wa kuweza kupangua au sauti yake itakuwa na kigezo gani.

Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri suala hili nimelizungumza kwa muda mrefu tangu nimeanza kuingia Barazani mwaka 2000 na bado nitaendelea kudai kwamba Naibu Kamishma wa Mamlaka ya Mapato *TRA* hapa Zanzibar, awe Kamishna kamili sio awe Naibu Kamishna. Ndio maana haya mambo mengi yanayotokezea yanatokezea kwa sababu hiyo. Kwa hivyo, suala hili nilikuwa naliomba sana Mhe. Naibu Spika, serikali yetu iweze kulisimamia hilo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hili suala la *TRA* nilikuwa nataka niliunganishe katika ukurasa wa 11 mpaka wa 13 Idara ya Ukuzaji wa Bajeti. Hapa vile vile katika Idara ya Ukuzaji wa Uchumi wameeleza, kuna kipengele kinachosema

kupendekeza marekebisho ya sheria za kodi na sera za kodi na kulinda viwanda.

Mhe. Naibu Spika, suala hili pamoja na kwamba mwenzangu Mhe. Omar Ali Shehe ameligusia lakini hii hoja mimi niliizungumza sana tulipokuwa tunazungumzia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika suala zima la kuwalinda wafugaji wetu. Mhe. Naibu Spika, hii Idara ya Ukuzaji wa Uchumi na wao ndio waliopendekeza marekebisho ya sheria, kodi na sera za kodi vile vile ni lazima tuwe na sera nzuri za kodi. Hizi sera za kodi Mhe. Naibu Spika, ziko za aina mbili. Kuna sera ya kodi ya kuongeza mapato ya nchi moja kwa moja, lakini kuna sera nyengine ya kodi ambayo ni ya kulinda. Aidha, viwanda vya ndani au kuwalinda wawekezaji wa ndani yaani wananchi wa kawaida na hapa tunazungumzia zaidi wafugaji.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilipokuwa nazungumzia Wizara ya Mifugo na Uvuvi nilizungumza kwa sauti kali katika suala zima la kuzuia wale kuku ambao wanaletwa ambao wamekuja kuuwa soko la kuku wa Zanzibar. Lakini hili suala ni mtambuka na mimi niliamini Mawaziri watakaa waangalie hoja yangu zaidi imelenga vipi. Hoja yangu nililenga kwamba ile kodi wanayotozwa wale isiangaliwe moja kwa moja kwamba inaongeza mapato ya kodi kwa upande wa Zanzibar, kodi ile iangaliwe katika kulinda hawa wafugaji wetu wa ndani, kama kunatozwa kama asilimia 10 au asilimia 20, basi ile kodi waifanyie tathmini kwa kuwa hii Idara ya Ukuaji wa Uchumi na Bajeti, hii ndio kazi yao. Sasa wapendekeze katika eneo hili ambalo wafugaji wetu wengi, serikali tunaishukuru sana kwa kupitia mfuko wa AK na JK, kupitia miradi ya *TASAF* na kupitia miradi mbali mbali ambayo hata hizi *SACCOS* wananchi wengi wamehamasika katika suala zima la ufugaji wa kuku kwa wamewekeza.

Juzi Mhe. Naibu Spika, nilizungumza kwamba kuna wananchi wetu wa Zanzibar ambao wamewekeza katika mradi wa uzalishaji wa vifaranga vya kuku. Mimi nilisema *plant* moja inatoa vifaranga 3000, niliporudi na kwa sababu kipindi kile nilifanya utafiti mwaka mmoja uliopita. Baada ya kumaliza hapa, kwa kuwa serikali walisema wanakwenda kukaa na mimi nilirudi tena kwa hao wawekezaji au wananchi waliowekeza katika mradi wa ufugaji wa kuku, kumbe ule mtambo mmoja Mhe. Naibu Spika, una uwezo wa kutoa vifaranga 19,000 kwa siku na leo nimekwenda katika hiyo *plant,* yeye ana mitambo mitatu, sasa hebu fanya tathmini. Mtambo mmoja unaweza kuzalisha vifaranga 19,000. Sasa 19,000 mara tatu, ukifanya mahesabu ya haraka hapo utakuta ni vifaranga karibu 57,000 kwa siku, huyo ni mzalishaji mmoja tu aliyetoa vifaranga. Je, leo hawa mimi nilisema wako karibu wazalishaji 6 lakini pengine kwa upande wa Pemba wako vile vile. Kwa hivyo, uwezekano wa wazalishaji Wazanzibari kuwalisha kuku na kuweza

kulihimili soko kwa upande wa Zanzibar, upo uwezekano mkubwa wa kuweza kuzalisha kuku wengi na kuweza kuwasambaza katika mahoteli mbali mbali, yakaweza kuziba lile pengo ambalo lilikuwa limepungua katika mahitaji ya kuku.

Sasa hapa Mhe. Naibu Spika, ndio maana natoa mapendekezo, kama tutaendelea kushusha bei au kuendelea kuwa na kodi inayolipwa sasa hivi katika uingizaji wa kuku, tusitegemee kama hilo pengo lililokuwepo sasa hivi litaweza kuzibika, kwa sababu wale kuku wanauzwa bei rahisi na hawa wa hapa kwetu kutokana na hakuna ufidiaji wowote. Aidha msamaha wa kodi katika kuingiza chakula cha kuku na madawa kwa sababu hivi ndio vitu ambavyo vinaongeza bei.

Mhe. Naibu Spika, kuna Waziri mmoja alizungumza juzi kwamba mfugaji wa kuku wa Zanzibar anauza kuku kuanzia shilingi 7,000/-. Ndio kwa sababu hana msamaha wa bei ya chakula cha kuku, hana msamaha wa bei ya madawa ya kuku wala hana msamaha wa tiba ya kuku. Wenzetu kule Ulaya hayo mambo yanakuwa yanafidiwa na hata kuku kama nilivyosema wanapokufa wanakuwa wanalipwa fidia. Lakini mfugaji wetu sisi, labda awe kapata ule msaada wa *TASAF*, lakini mambo yote yaliyobakia inabidi ajitegemee yeye mwenyewe. Kwa hivyo hapa ndio maana nikasema, tuangalie sera ya kodi ya kuwalinda wananchi wetu wafanye tathmini kuku hawa walioingizwa nyama ya kuku inauzwa bei gani na hapa kwetu ili waweze kulingana na ile bei yao ya mauzo. Naamini tukiweza kuhakikisha hilo au likiweza kutekelezwa hilo basi naamini wafugaji wataweza kufufuka upya na watazalisha kuku kwa wingi na hilo pengo ambalo lipo baina ya *supply* ya kuku au *demand* ya kuku na wafugaji wetu itaweza kukatika. Kwa hivyo, huo ulikuwa ni ushauri wa bure ambao namuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni mtu ambaye msikivu, naamini hilo ataweza kulifanyia kazi na ninaamini katika bajeti ya mwakani, hatutokuja kusikia tena kadhia ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika programu ya kupunguza umaskini MKUZA, moja katika eneo hili ambalo tunatakiwa tuekeze ni hili, kwa sababu sasa hivi mwani hauna soko lakini kuku soko wanalo, hebu tutengeneze mazingira mazuri ili hawa wananchi waweze kupata soko zuri na la uhakika basi mimi naamini kila mtu atafanya biashara ya kuku.

Mhe. Naibu Spika, sisi humu leo tusijione tunapokea mishahara hatuna wasi wasi lakini siku wananchi watakapotuambia bwana wewe pumzika, basi sote tutakimbilia kwenda kufuga kuku, soko si lipo tutakwenda kufuga kuku. Wapo wenzetu ambao baada ya kuambiwa na wananchi wao pumzikeni sasa

hivi wanafuga kuku. Kwa hivyo ni lazima tutengeneze mazingira mazuri ili sote humu tukimaliza Baraza tukawe wafugaji wa kuku wazuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, naomba usinitizamie saa, kwa sababu leo kidogo wajumbe wengi wametupa nafasi wakongwe angalau tuweze kushauri serikali. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niulize tu kuhusu huu mfuko wa barabara, naona Mhe. Waziri umesema kwamba mnawapa ruzuku. Hebu uje unifafanulie mnajua nyinyi ndiye wataalamu wa mambo ya fedha kwa sababu hizi fedha za mfuko wa barabara ni fedha maalum, ile tozo moja kwa moja inakwenda katika mfuko, inapokuwa ruzuku ina maana inakwenda katika mfuko mkuu wa serikali halafu wale mnawapa ruzuku kwa ajili ya utendaji wa kazi. Sasa na hili nilikuwa naomba vile vile nije nisaidiwe.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kutokana na uchakavu wa mitambo ya ndugu zetu wa *UUB*, barabara nyingi za vijijini zilikuwa zinapigiwa kelele. Lakini kwa bahati nzuri juzi mfuko wa barabara wametufanyia semina tunawashukuru, kumbe fedha wanakuwa nazo za kutosha lakini uwezo wa ile taasisi au Idara yetu ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, uwezo wao unakuwa mdogo pengine kutokana na vifaa vyao kuwa duni. Nilikuwa naomba tuangalie kama sheria yetu inaruhusu tuangalie. Aidha, kama kuweza kuwapa vile vitendea kazi ili hizi fedha waweze kuzitumia vizuri na malengo yaweze kufanikiwa. Lakini kwa kweli tunashukuru fedha hizi zinakusanywa vizuri na mpaka sasa hivi bado hatujasikia ubabaifu mkubwa katika fedha hizi za mfuko wa barabara.

Vile vile nije katika *BoT*. Mhe. Naibu Spika, narudia tena suala langu la siku zote, vipi wale wafanyabiashara wa kati na kati, wale *small and medium enterprises* kwa upande wa Zanzibar, kupatiwa ile mikopo ya bilioni 4 kama wanavyopatiwa wenzetu wafanyabiashara wa kati na kati ambao wanapatiwa karibu mikopo ya bilioni 4. Yaani kuanzia fedha anazotaka mpaka bilioni 4 kikomo. Hapa Zanzibar je, bado hawajatimiza vile vigezo wafanyabiashara wetu kupata fedha hizo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba tunakwenda katika Bunge la Baraza la Katiba. Mimi nilikuwa nakuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuna siku moja ututafutie wachumi wako wote, wataalamu wako wote wa Wizara ya Fedha unaowaamini waje wakae na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tena naomba hili suala ikiwezekana kabla hatujatawanyika hapa, waje watupe ni maeneo gani ambayo Zanzibar tunaweza kuyabakisha katika muungano katika mambo ya uchumi na mambo gani tunaweza kuendelea kila mmoja na lake.
Mhe. Naibu Spika, vyenginevyo masuala haya mkituachia sisi wana siasa, mkasema tunayajua sisi lakini mambo ya kiuchumi naamini una kikosi kizuri

cha wataalamu wa fedha wanaweza wakaja kutushauri mambo mengi ambayo yatatusaidia tutakapokuja kuchangia maoni ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *ZIPA* nakwenda haraka. Mimi nataka niseme tena na naunga mkono na wale wenzangu waliozungumza kwamba *ZIPA* bado haijawa *one stop center*. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nirudie tena, ule mradi wa ile *air strip*, mradi ambao hata juzi Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kutokana namambo mengi yalimbana alishindwa kuyatolea ufafanuzi wa kutosha. Lakini nashukuru nimepata *documents* za *ZIPA* ambao waliruhusu ule mradi na ukiangalia *ZIPA* watu wa ardhi wako pale, watu wa sheria wapo na watu wa aina mbali mbali wapo. Leo inakuaje mtu anafika pahala anaambiwa tafuta eneo, ametafuta eneo la kuweza kuekeza kiwanja cha ndege.

Mhe. Naibu Spika, ndio pale tunapozungumza *ZIPA* wao wanatakiwa wahamasishe wawekezaji. Leo mwekezaji huyu amekuja kuekeza, mradi ule wa kufundisha marubani. Mhe. Naibu Spika, ile peke yake ni kuitangaza nchi. Leo mpaka wa-Kenya wamekuja kujifundisha urubani Zanzibar, dogo hilo! Wamekuja Uganda, Rwanda, Waingereza, Wafaransa, Wataliana wote wamekuja kufundishwa urubani Zanzibar. Sasa leo hawa wanataka kuja kuweka kiwanja ili waweze kuwa na nafasi kubwa ya kuweza ku-*invest* mradi wao ule, tunaozungumza mradi miaka mitatu haujawa. Sasa hili naomba sana kwa sababu najua Kamishna wa *ZIPA* mradi huu anaujua, nitaomba Mhe. Waziri nije nipate maelezo ya kutosha, kwa nini huyu amejaribu kufuata vigezo vyote bado mpaka leo haujaweza kufanikiwa. Vile vile katika kitabu ulieleza kwamba *ZIPA* imeweza kujitangaza kufuatilia ziara ya Mhe. Rais nchini China. Sisi hatutaki ni lazima Rais na nyinyi muende mkajitangaze na nyinyi wenyewe *ZIPA* mtoke mwende mkajitangaze.

Mhe. Naibu Spika, sisi tulipokwenda China kuna wale ma-*tour guides* ambao waliokuja wakatutembeza katika miji mbali mbali ya China. Wanatuambia hiyo Zanzibar yenyewe hawaijui. Sasa kama *ZIPA* watakwenda kule na kama watazungumza na wale wenzetu ma-*tour guides* na kampuni nyengine zile, basi mimi naamini kuna mashirika ya ndege ya China yangeweza kuja kutua Zanzibar. Vile vile na watalii kutoka China pia wangeweza kuja kuekeza Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna miradi ya *Real Estate*. Nilizungumza katika bajeti nilimuomba sana Makamu wa Pili wa Rais na namshukuru sana amenisikia na naamini atashiriki katika ule mkutano wa Marekani. Lakini bado na China kule ziko kampuni za ujenzi wa nyumba za kisasa nyumba za kuwajengea wananchi katika bei nafuu na mkopo wa muda mrefu, bado

naomba wawekezaji hawa waweze kuwasogelea ili waweze kuja kuekeza Zanzibar. Lakini bado jengine.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri *ZIPA* bado hawajaweza kuwasimamia wananchi wetu wa Zanzibar katika haki zao hasa katika maeneo yao yaliyochukuliwa na wawekezaji katika mahoteli ya utalii. Mpaka leo ninavyozungumza kuna wawekezaji ambao wamewekeza ndani ya maeneo ya wananchi, wanaendelea kukusanya pesa ndani ya maeneo ya wananchi na wananchi wale wanaendelea kudai.

Narudia tena Mhe. Naibu Spika, kuna *Crestal Hotel* ameendelea kuekeza ndani ya eneo la mwekezaji, ndani ya eneo la Mzanzibari anaendelea kukusanya fedha na *ZIPA* wamekaa wanatumbua macho. Pia kuna Magembe Hoteli kule Michamvi, nasema tena wananchi tena wamesaini mpaka mkataba, amechukua eneo lao analitumia mpaka sasa hivi, wamesaini mkataba atawalipa milioni 16 huu ni mwaka wa tano. Tulimwita mwekezaji yule mpaka kwenye Baraza la Wawakilishi, amesaini *documents* zetu za Baraza la Wawakilishi kwamba atawalipa wananchi wale pesa zao milioni 16, mpaka leo *ZIPA* wapo sijui wanafanyakazi gani.

Mhe. Naibu Spika, ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza umeshatumia dakika 25 nakuachia dakika 5. Saa ile pale mbele angalia na mimi naangalia yangu, ikifika unamaliza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa heshima hiyo, kwa kuwa umenipa hizo dakika 10 ya Mwenyeviti wa Wenyeviti. Mhe. Naibu Spika, pia *ZIPA* naomba hili eneo la maeneo huru la Micheweni na Fumba lipimwe ili lipatiwe hati miliki. Vile vile hii *master plan* katika maeneo haya. Rais wetu ameshakwenda China, kenda kuwaita wawekezaji, Wachina hawana masihara katika uwekezaji, ukiwaambia wakija huna eneo wanaondoka na wakiondoka hawaji tena. Hebu maeneo haya ya maeneo huru ya Micheweni na Fumba tuyapatie hati miliki, tutengeneze *master plan* ili wawekezaji wetu wakija tena wasiwe na danadana.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri eneo la Tunguu wafanye haraka kuweka *ATM* pale, sasa hivi kuna wanafunzi wengi. Leo mwanafunzi anatoka Tunguu anakuja *PBZ* pale Mwanakwerekwe, foleni kubwa. Tunaomba pale muwawekee *ATM*. Ule mji sasa hivi umeshakuwa ni mji wa biashara na ni mji mkubwa pamoja na hiyo mipango yenu lakini pale mutoe kipaumbele vile vile.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana niliwahi kumwambia Mhe. Waziri kabla ya Waziri wa Fedha hajatangaza kodi ya simu. Mimi niliipata kwa kupitia vianzio vyangu na nikawaambia serikali, je Waziri wa Fedha kakushauri Waziri wa Fedha mwenzako, bajeti yake ya mwaka unaokuja anataka kutoza kodi ya simu katika kila kadi. Jee, Zanzibar tutafaidika vipi. Mhe. Naibu Spika, mpaka leo hakuna dalili ya kufaidika na suala hili sisi hatukubali, tunaomba sana Mhe. Waziri kwa sababu huu ni unyang'anyi wa fedha zetu, tunataka na sisi hiyo kodi ya simu kama itapita kule na naamini imeshapitishwa na Bunge kule.

Kuhusu suala la *e-Government*. Mhe. Naibu Spika, mimi naungana na ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi, suala hili tuachiwe Baraza la Wawakilishi tuliundie kamati, tulifuatilie ili tuje tulete ripoti. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo sisi tunakuonea huruma. Wewe kila siku utajibu majawabu ya watu tu, hebu tuachie na sisi tuifanye hiyo kazi tukusaidie tukuletee ripoti, naamini ripoti hiyo itaweza kukusaidia katika kusimamia mambo yako.

Halafu vile vile

Mhe. Naibu Spika: Malizia! Malizia! malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini pia naomba suala la *Visa*. Katika vikao vya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki suala la kutumia *Visa* moja katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na *Visa* ni sehemu ya mapato makubwa katika uchumi wa Zanzibar, naomba sana suala hili bado Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar isimame kwa miguu yake miwili, suala la *Visa* bado Zanzibar iendelee kutoza *Visa* yake wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hili suala wala sio geni ukiangalia kwa wenzetu Jumuiya ya Ulaya, katika Jumuiya ya Ulaya, Uingereza mpaka leo zile nchi zote za *Schengen*, ukipata *Visa* ya *Schengen* unaingia Ufaransa, Ubelgiji na nchi zote zile. Lakini ukitaka kwenda Uingereza ni lazima uwe na *Visa* ya Uingereza. Kwa hivyo, bado naomba sana kutokana na uchumi wetu wa Zanzibar na hali yetu ya uchumi wa Zanzibar, *Visa* ni sehemu ya mapato yetu, naomba endelea kwamba mtu anapokuja au mtalii yeyote anayekuja Zanzibar basi akate *Visa* ya Zanzibar.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii sina matatizo sana. Lakini naunga mkono kwa asilimia 90, hizi asilimia 10 nije nipate maelezo hasa katika masuala ya sera za kodi kwenye ule uingizaji wa kuku itazungumziwa vipi, ili nipate kujiridhisha ili na sisi tujiandae kuwa

wafugaji wa kuku wazuri huko baadae. Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi ya kueleza machache niliyonayo juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hii ofisi inachukua mambo ya fedha, uchumi na mipango ya maendeleo. Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nataka mimi nianze na hili jina la hiki kitabu na sitoanza na fedha, lakini nianze na hii uchumi na mambo ya maendeleo. Uchumi wa nchi unategemea raslimali ziliopo na vitega uchumi vyenyewe.

Mhe. Naibu Spika, sisi Zanzibar vyanzo vyetu vya uchumi ni vipi. Sisi katika nchi hii hatuna viwanda vikubwa, hatuna kilimo kikubwa ambacho kinazalisha chakula cha kula sisi wenyewe na hatimaye kusafirisha. Kwa hivyo, tunao wafanyabiashara wakubwa ambao lakini sehemu kubwa wanaagizia kuliko kusafirisha. Kwa hivyo, mara nyingi fedha yetu inatoka zaidi kuliko ile inayoingia. Sasa sijui huu uchumi wetu unakua vipi wakati ambapo tunatoa zaidi kwa kuagizia kuliko kile kinachoingia ndani ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, haya maendeleo ya nchi ni yepi. Mtu anapokuja Zanzibar, pengine kaondoka miaka 10 au 15 nyuma, bila shaka atakuta mabadiliko yapo, ataona yapo majengo makubwa, barabara nyingi na mambo kadhaa yamebadilika. Lakini kama mtu yule sio mgeni basi baada ya hatua mbili tatu atafuatwa na mtu kumtaka amsaidie, yaani mtu omba omba, sasa yule mtu anaweza kustaajabu, barabara hizi ziliopo, msongamano wa magari, majumba makubwa na mazuri na bado kuna omba omba wa aina hii. Kwa hivyo, haya maendeleo yetu sisi yakoje, kwa hali iko hivi lakini bado umaskini umekithiri. Hata wale ambao wanajitokeza wako wanaovumilia umaskini wao, lakini bado sura ya nchi unapoiona inakuonesha kuwa hii nchi inaendelea, lakini wananchi wake bado asilimia kubwa wanaishi katika maisha duni. Tukiyachukulia maendeleo katika nyanja za majengo ya miundombinu mbali mbali basi tumeendelea, tutathmini maisha ya watu wanavyoishi vijijini bado hatujaendelea hata kidogo. Kwa hivyo, sijui haya maendeleo tunayapa tafsiri gani katika hii nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka nigusie jambo moja dogo tu katika Idara ya Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini. Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kidogo ukurasa wa 7.

Ukurasa wa 7 wa kitabu cha bajeti unaeleza hivi:-

> "Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 kwenye *program* 22 na miradi 81 ya maendeleo kwa Unguja na Pemba ambapo changamoto mbali mbali zimejitokeza zikiwemo fedha za miradi kuhaulishwa na kutumika kinyume na shughuli zilizokusudiwa".

Mhe. Naibu Spika, kwa *program* 22 zilizotajwa na miradi 81, tumejipangia mambo mengi ambayo mara nyingi hatufikii kuyatekeleza yote. Kwa hivyo, nashauri kwamba tupange miradi na *program* ambazo tunaweza kuzikamilisha katika mwaka husika na wala tusiwe na uporo wa *program* au miradi ya maendeleo. Kutokana na hali hii Mhe. Naibu Spika, naomba kujua kwamba hizi fedha ambazo zinahaulishwa kutumika sehemu nyengine kinyume na vile zilivyokusudiwa kwa nini ifanyike hivyo, wakati ambapo palipokusudiwa hapatumiki na zinatumika sehemu nyengine. Kwa hivyo, ni jambo lipi la msingi linalosababisha fedha zifanyiwe hivyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu Mfuko wa Barabara. Kwa kweli mfuko huu ni muhimu sana kwa sababu mfuko huu kazi yake ni kufanyia matengenezo barabara zetu ambazo tayari zimejengwa. Kwa maana hiyo, mfuko huu si wa kujenga isipokuwa ni mfuko wa barabara, pale barabara inapoumwa, yaani kuumwa kwa barabara ni kuharibika kwake basi mfuko huu kazi yake ni kutibu pale palipoharibika.

Mhe. Naibu Spika, mfuko huu mara nyingi huwa unachelewa kufanya tiba mpaka baadhi ya barabara zinafikia hatua ya kuwa haziwezi kupitika tena kwa mashimo na michimbuko mbali mbali wakati ambapo mfuko lengo lake ni kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo ninaomba Mhe. Naibu Spika, kwamba mfuko huu usingojee mpaka barabara ikawa haipitiki tena ndio hatimaye tuweze kufanya hivyo.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, ukitembelea barabara kuu ya Pemba, Wete Chake-Chake na kule Pemba tunaita barabara kongwe na hii takribani imekufa, baada ya kuanzishwa barabara mpya iliyozunguka huku basi hii imekufa na imesahauliwa na ingawaje hivi karibuni wameanza kutia viraka vya hapa na pale, lakini bado barabara hii ni mbovu na inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa na watu wa sasa wanaita kukarabati. Katika ujenzi wa barabara ni lazima tuchague kampuni ambazo zitaweza kujenga barabara zenye ubora ambazo angalau zitadumu kwa muda mrefu kidogo. Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Kusini Pemba umepata bahati mbaya kwa barabara nyingi

zilizojengwa katika miaka hii ya karibuni ambazo kiwango chake ni duni sana.

Ningeuomba Mfuko wa Barabara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ufuatilie hizi barabara sita ambazo tayari zimeshajengwa katika Mkoa wa Kusini na mbili zikiwa katika Jimbo la Mtambile, yaani Mtambile Kangani na Mtambile Mwambe, basi wasingojee mpaka zikachimbuka moja kwa moja lakini waanze kuzifanyia ukarabati mdogo mdogo kabla hazijaendelea kuharibika moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, barabara zinajengwa chini ya kiwango na gari zinapoendelea kupita basi barabara zinadidimia chini. Kwa hiyo, ninaomba wahusika kwa miradi hii ya ujenzi wachague wajenzi ambao wenye uwezo wa kujenga barabara zetu kwa kiwango kinachohitajika.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Naibu Spika, mfuko huu ni mzuri na mwaka uliopita walikuwa na lengo la kusajili waajiriwa 85, lakini walisajili 73 wala hawakufikia lengo. Hali hii ina maana kwamba kuna watu wameajiriwa hawakujisajili au hakukuwa na ajira za kutosha. Lakini naomba kuwashauri waajiriwa kwa maslahi yao wajiunge na Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii kwa sababu wakati watakapostaafu utawasaidia kupata kiinua mgongo kizuri kidogo na halafu na waajiri na wao wajitahidi, kwa sababu muajiriwa anayo sehemu anayoingiza kwenye mfuko na muajiri na yeye sehemu yake ya kila mwezi anaipeleka.

Mhe. Naibu Spika, wapo waajiri wengine hasa wa sekta binafsi ama wanachelewesha au pengine ile sehemu yao hawawasilishi kabisa, kwa hivyo kinachokwenda kule ni ile sehemu ya mfanyakazi inayotokana na pato lake mwenyewe tu. Kwa hivyo ninaomba wizara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ifuatilie kuhakikisha kuwa waajiri na wao wanawaekea akiba wafanyakazi wao.

Vile vile mfuko huu unawalipa wafanyakazi pale wanapostaafu haki zao wakati wanapofikia ule umri ambao umepangwa kisheria. Mhe. Naibu Spika, nimesema mara mbili tatu kuna wafanyakazi wengine ama wanafukuzwa kazi au wanastaafu kabla ya kufikia ule umri, kwa sababu walichoekeza ni chao kwa nini wasipewe na tayari wamestaafu au wamefukuzwa kazi na hata kama amefukuzwa kazi alichoekeza ni cha kwake mwenyewe. Kutokana na hali hiyo, naomba kufanywe marekebisho Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala hili ili wafanyakazi wanapostaafu kwa njia yoyote ile waweze kupata haki yao hata kama ule umri uliopangwa haujafikia.

Mhe. Naibu Spika, jambo moja dogo la mwisho kwamba leo ni tarehe 04/08/2013 sawa na mwezi 26 Ramadhani, bado siku chache kuingia katika siku-kuu wafanyakazi wamepata mishahara yao tarehe 23 au 24 nyuma huko na kesho kutwa wanaingia kwenye siku-kuu hawana fedha. Hivyo, Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hatufanyii maarifa akatulipa kabisa mshahara wa mwezi wa nane, kwa ajili ya kutumia kwenye siku-kuu kwa kweli hali za wafanyakazi ni ngumu sana, kama ikiwa hawezi kutupa mshahara wote basi angalau nusu atupatie. Lakini kuna lugha ya vijana wanasema kwamba 'hali ni ngumu kuliko maelezo'. Vile vile akitukopesha asije atukata moja kwa moja isipokuwa atukate pole pole kwa muda wa miezi sita mpaka kimalizike kile ambacho ametukopesha. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana ninakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru kwa mchango wako. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na baadaye Mhe. Jaku Hashim Ayoub na ajitayarishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu, atafuatia Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na kwanza nianze kwa kushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo tukaweza kukutana hapa hali ya kwamba tuko mwishoni mwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie funga zetu azikubali na tuikaribishe siku-kuu kwa amani na usalama. Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na timu yake ya watendaji kwa kazi nzito ambayo wamekwisha kuifanya na hatimaye kuweza kutufikishia sisi hapa leo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na utangulizi wa bajeti iliyopita Mhe. Waziri pamoja na mambo mengi ambayo nilikuwa nimeyachangia katika bajeti iliyopita mwaka 2012/2013, nilimuomba Mhe. Waziri kwamba tujitahidi mwaka huu tunaoanza nao tuondokane na utaratibu wa kutoa risiti kwa kutumia utaratibu tulionao sasa. Lakini kwa bahati mbaya sikuona mwelekeo ambao umenipa matumaini wa kuweza kuona ni namna gani serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunaondokana na utaratibu tulionao sasa na tunaanza kutumia risiti za *electronics* ili tuweze kuona mapato yetu tunayakusanya zaidi.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie ni sababu zipi zilizosababisha ndani ya kipindi cha mwaka mzima tukawa hatukuweza kufikia malengo ya

kuweza kufanya makusanyo ya kodi zetu za serikali kwa utaratibu wa kutumia *electronics*.

Nikiondoka hapo nikiendelea na kumbukumbu za mwaka uliopita ambapo Mhe. Waziri alipokuja hapa alituelezea kwamba kuna sheria ambazo zilitakiwa kufanyiwa kazi kwenye ukurasa wa 62 wa kitabu kilichopita. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kule kulikuwa na sheria za kodi mbali mbali ambazo Mhe. Waziri alituelekeza kwamba utaratibu wake utafanyika na kuona kwamba mwaka huu wa fedha sheria zile zinafanyiwa mapitio pamoja na kufanya marekebisho ili sheria zile ziweze kuendana na wakati. Lakini kwenye kitabu hichi kipya ambacho kimesomwa hapa sikuweza kuona maeneo hayo ambayo yatakuwa yanatuelekeza namna ambavyo Mhe. Waziri amejipanga katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie kunipa taaluma zaidi katika maelekezo ambayo yamo kwenye kitabu chake hichi kipya ukurasa wa 6 juu ya Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini. Kwa hivyo, tukiangalia kitabu hichi lakini tukioanisha na jadweli ambalo liko kwenye ukurasa wa 83, naona ni kweli tunazungumza suala la kuondosha umaskini katika nchi yetu lakini bado matumizi ambayo yaliyofanyika katika kipindi kilichopita hayaridhishi kwamba ni kweli tuko *serious* kuwaondoshea wananchi wetu tatizo la umaskini ambalo linawakabili.

Sasa naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze kwamba ni namna gani wanajipanga kuhakikisha kwamba ni kweli wamepania kuwaondoshea umaskini wananchi wetu. Kama hiyo haitoshi Mhe. Naibu Spika, wakati atakapofanya majumushi Mhe. Waziri, basi namuomba atupatie maelekezo juu ya msamaha ambao tumesamehe kwa wawekezaji ambao wamekuja kuekeza katika nchi yetu ni kima gani cha msamaha tulisamehe na serikalini ina matarajio ya kupokea nini baada ya msamaha ule ambao tumeutoa kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 na 2013/2014.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba kuzungumzia kuhusu suala zima la mchango ambao tuliutoa wakati wa vipindi vya maswali na majibu pia kwenye vikao tofauti juu ya kulitumia eneo la Nyamanzi, kwa ajili ya kuondoa msongamano wa magari pamoja na biashara ya vyombo vya moto ambayo inafanyika katika mji wetu wa Zanzibar. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho pamoja na maombi na mapendekezo ambayo tuliyompa, ni namna gani wizara yake imejipanga kuhakikisha kwamba hapa magari ambayo *show rooms* za

magari ambazo zimezagaa katika mji wetu wa Zanzibar, zinaondoshwa na kuelekezwa katika maeneo yale ya ukuzaji wa vitega uchumi Nyamanzi.

Lengo ni kwamba ule mji upande wa kule uweze kukua na shughuli ziweze kupanuka na wananchi waweze kupata ajira zaidi na mambo mengine pia yaweze kuendelea vizuri zaidi. Mhe. Naibu Spika, pia naomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie mikakati ambayo ameipanga katika kuhakikisha hilo linatekelezwa.

Jengine ambalo nataka kupata maelekezo pia ni kuhusu suala zima la magendo ya mafuta. Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukijitahidi kupiga makelele sana hapa juu ya utaratibu mzima wa magendo ya mafuta ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Kwa kweli nilitegemea labda ningeweza kuona mikakati ambayo Mhe. Waziri ameipanga katika wizara yake, ili kuhakikisha kwamba tunakabiliana na tatizo hilo la magendo ya mafuta lakini kwa bahati mbaya sikubahatika kuona katika kitabu hichi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie kuweza kufahamu mikakati ambayo ameipanga kwa ajili ya kukabiliana na biashara hii haramu ya mafuta ambayo inaikosesha Zanzibar pato kubwa la serikali na hususan ukitilia maanani ni kipindi kirefu tumekuwa tunapiga kelele katika suala hili, lakini bado hatujaridhishwa na hatua ambazo zinachukuliwa katika kudhibiti magendo haya ya mafuta ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja kwenye waraka wetu huu ambapo ni marekebisho ya makadirio na mapato, kwenye hii karatasi ambayo tumepewa ukurasa wa 19 kwenye kifungu 0202 Idara ya Kodi za Ndani *TRA* katika *bullet* 112101 mapato ya wafanyakazi. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie uwiano baina ya makusanyo ya *pay as you earn* kwa mapato ya ndani, yaani kwa Zanzibar na wale wafanyakazi wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tofauti yake iko vipi, naomba kupata maelekezo katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba kupata ufahamu kidogo katika hicho kifungu cha Idara ya Kodi za Ndani kwenye *bullet* 115100 kuhusu Kodi za Forodha na *Custom Exercise* 115101 mpaka kumalizia 115106 na hapa kuna mapato ambayo hapa yameekwa ni makisio ya shilingi 93,900,136,000/=. Kwa hivyo, nikiangalia *table* ambayo ipo hapa na nikioanisha na makisio pamoja na mahesabu ambayo yalikuwemo kwenye kitabu chetu hichi kipya cha mwaka 2012/2013, naona kuna mahesabu ambayo hayaoani. Kutokana na hali hiyo, naomba kupata ufafanuzi je, kuna matatizo ya *typing error* au ndio uhalisia

hasa ulivyo kwamba kitabu hichi wakati kimepita mahesabu yake yanakuwa tofauti na kitabu hichi kipya ambacho kitakuwa kinaanza kutumika kwa sasa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja kwenye eneo la 0701 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kwa kweli mwaka jana tulipokuwa tunachangia hapa tulimuomba Mhe. Waziri atusaidie kuweza kuona kwamba ile *rotation* ya kuwabadilisha Wahasibu Wakuu wa serikali inaendelea lakini hatukupata maelekezo kwamba nini kinaendelea katika hilo.

Suala jengine nikiondoka hapo nikija chini kabisa katika fungu hilo la 0701, kuna salio la bajeti iliyopita ya shilingi 5,000,000,000/=. Mhe. Naibu Spika, naomba kupewa ufafanuzi pamoja na maelekezo kwamba hili salio la bajeti ambalo limebakia la shilingi 5,000,000,000/= ambalo hata katika taarifa ile ya bajeti kuu ya serikali lilikuwa limetamkwa linakuja vipi, wakati kuna mapungufu kwenye utekelezaji wa bajeti na mgao wa bajeti katika mwaka ambao umemaliza hivi sasa, naomba kupata maelekezo katika hilo. Vile vile katika kifungu 1301 Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma kuna makisio ambayo yamewekwa hapa ya Kodi za Serikali lakini maeneo ambayo yamepangwa kwa ajili ya hizo kodi ni mashamba ya mipira, malipo ya nyumba ya *Africa House* pamoja na malipo ya *Depot.*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa atusaidie maelekezo kwamba haya ni mapato basi ambayo yanastahili kukusanywa katika taasisi hii na kwenye nyanja hizi tu, kwa sababu naona kuna maeneo mengi ambayo yalipaswa kukusanywa mapato ya serikali, lakini mbona tumeainishiwa kidogo tu hapa na haya maeneo mengine hayahusiki basi naomba ufafanuzi zaidi katika hilo.

Tukiendelea mbele zaidi katika kifungu 2703 kuhusu Bodi ya Mapato Ofisi Kuu Zanzibar na hapa naomba kupata ufafanuzi, kwa sababu sijaridhishwa na makisio ambayo yapo hapa ya shilingi 74,619,468,000/=, kwamba haya ndio matarajio na makisio ya makusanyo katika bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, tukitilia maanani hapa kuna kitu ambacho kimenipa mashaka nikiangalia makisio ya kitabu kilichopita ambapo kulikuwa na makisio ya makusanyo ya shilingi 68,000,000,000/=. Lakini kwenye karatasi yetu hii tuliyopewa makisio ya makusanyo ni shilingi 69,000,000,000/= ukilinganisha makisio ya mwaka jana 2012/2013 na makisio ya mwaka 2013/2014 kuna tofauti hapa na bilioni 1.4. Sasa ningelipenda kupata ufafanuzi wa maelekezo hayo.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho kwamba tukiangalia hesabu ya ujumla ya

mapato ambayo yanatarajiwa kukusanywa na taasisi hii ya Wizara ya Fedha na maeneo yake mengine ni jumla ya shilingi 138,845,728,000/= na haya ni ya mwaka jana na mwaka huu ni shilingi 147,200,785,000/= tofauti yake ni shilini bilioni 8 na nukta kidogo tu. Kwa hivyo, tukiangalia kutokana na mikakati na mipango mizuri ya ukusanyaji wa mapato ndani ya serikali yetu kwa mwaka unaokuja na kiwango ambacho tumeekewa, kwa kweli hakijaniridhisha.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie ufafanuzi zaidi, ili tuweze kuona kwamba tunafanya makusanyo yetu vizuri, tunaisaidia serikali yetu pamoja na nchi yetu na tunaondokana na matatizo ambayo tunayo.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja hii kwa asilimia 85 na 15, nitamalizia shemegi yangu endapo atanipa majibu ambayo yataniridhisha na baada ya hayo ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa nafasi tunampa Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ajiandae Mhe. Saleh Nassor Juma na leo tutamalizia mchango wetu kwa Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha hapa nikasimama kwa neema zake, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe kunipa fursa hii na kama ungekataa basi nisingeweza kuchangia bajeti hii.

Vile vile nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada anazozichukua za kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pia nimpongeze kwa dhati kabisa jinsi alivyokuwa fundi wa kupanga maneno ya Kiswahili. Kwa kweli ni fundi mzuri tena ni mzungumzaji mzuri neema kubwa aliyoipata hiyo na katika mawaziri basi mmoja ya mawaziri muhimu sana katika nchi hii na ukiangalia wizara yake ni Wizara ya Fedha, yaani wizara baba au mama. Mhe. Naibu Spika, wizara hii ndio tunamalizia panapo uhai na majaaliwa, yaani wizara ambayo kila wizara inamgusa kwa namna moja au nyengine. Kwa hivyo, ninachokusudia kuzungumza hapa Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze kwa nia njema kabisa ya kuwatetea wananchi wa Zanzibar na kama sisi Wawakilishi tupo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na hivyo nitakayoyazungumza hapa ni kwa niaba ya wananchi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, hivi juzi tena kwa masikitiko nitakuwa sijafanya haki Wizara ya Afya kama sikuwatetea katika bajeti hii, Mhe. Waziri wa Fedha sijui tuseme umekuwa mchoyo au unawabana kwa sababu gani hawa Wizara ya Afya, kwani ilifika karibu siku tatu au nne *major operation* Hospitali ya Mnazi Mmoja haijafanyika, ni aibu ya hali ya juu, hospitali ambayo inategemewa kuitwa Hospitali ya Rufaa na sijui hii itakuwa ni ndoto ya usingizini tu au ifika kweli iwe Hospitali ya Rufaa. Mhe. Naibu Spika, ikiwa hospitali inashindwa na mtungi wa *oxygen* wa shilingi 65 tuna-*survive* vipi? *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumzwa hapa mimi nilifuatilia na kisingizio Wizara ya Fedha haijawapa fedha. Katika hali kama hii hatuwezi kufika Mhe. Waziri na tutawalaumu watendaji siku zote hapa, Waziri hivi, Naibu Waziri vile, Katibu Mkuu bila ya nyezo hawawezi kufanyakazi.

Sasa kuna sababu gani Mhe. Waziri wasipewe fedha zao kama tunavyowaombea na ikawa idara zake zote anachukua asilimia mia moja au ndio sadaka inaanza nyumbani na taa unawasha ndani ya nyumba kwanza, yaani asilimia mia moja idara zake zote inachukua fedha na wale wengine wanateseka wananchi wa nchi hii kwa kukosa matibabu katika hospitali ile. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa nitakuwa mkaidi na wala sina nia hiyo lakini mpaka nitakapopata maelezo, kwamba wanachokiomba Wizara ya Afya wapewe kwa mujibu walivyoomba kwa sababu ile wizara ni muhimu sana na wananchi imewagusa kwa kila njia. Kwa kweli leo aibu *oxygen* mtungi wa shilingi 65 au 70 *major operation* haijafanywa kutokana na kisingizio hiki.

Kwa mfano, kitabu juzi cha Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

> Kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kinaeleza hivi:-
>
> > “Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii: Mhe. Spika lengo kuu la mradi huu ni kuwa na miundombinu bora ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii nchini kupitia viwango vya juu vya utoaji mafunzo na nadharia, vitendo vya huduma vya hoteli na uongozi.
> >
> > Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa ujenzi wa ghorofa ya kwanza, ambapo nyumba 11 zikiwemo ofisi 10, ukumbi 1 wa mkutano wa ofisi pamoja na vyoo 7. Jengo hili

> limeshawekwa miundombinu yote ya maji na umeme na kukamilisha shughuli za uwekezaji na hivi sasa jengo hilo liko katika hatua ya mwisho ya uwekaji milango, utuaji rangi pamoja na *tiles.*
>
> Mhe. Spika, gharama za mradi huu ni shilingi 400,000,000/= ambazo hadi kufika Juni, 2013 jumla ya shilingi 400,000,000/= zimeingizwa kwa asilimia mia moja".

Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali inapotaka lake inaweza kufanya. Sasa leo wananchi wetu tunawaweka rehani maisha yao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hapa nitahitaji maelezo ya kina kuhusu wizara hii. Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, nizungumzie Benki yetu ya Zanzibar ambayo benki hii wengi imetulea na itakuwa si mwingi wa fadhila na ninawashukuru sana watendaji wake. *(Makofi).*

Lakini nataka kuwapa nasaha tu kwamba hebu watueleze wana siri gani na *ZSSF* kukodi majengo yao, leo wananchi wa Mwanakwerekwe wanavyoteseka pale huwezi kuamini na ule sio mjengo wa benki, isipokuwa ule ni mjengo wa maduka, yaani huku vibanda viwili na upande wengine ni vibanda viwili na wananchi wanateseka ndani na hata vipoza hewa hamna na mimi nimeshawaambia wenyewe *personally*. Kwa kweli itakuwa sijawafanyia wananchi haki kama sikuwazungumzia hapa kwamba lile jengo halikidhi na wananchi wanaumia ndani mule, yaani fedha zinawatesa wenyewe.

Jengine naomba niwaeleze ndugu zangu wa *PBZ* kupita kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba vikao vimekuwa vingi, basi ni vyema wavipunguze na kila ukenda unaambiwa kuna kikao na sijui vinaleta maendeleo gani, nadhani vikao vimekuwa vingi sana.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni kuhusiana na mikopo sijui mwananchi wa Zanzibar awe na sifa gani ili aweze kupata mkopo pale. Kwa kweli kwa muda mrefu wananchi wanateseka na benki yao inaitwa *PBZ,* vigezo havijulikani, kitu gani muda mrefu kwa mfano ukenda benki nyengine siku tatu au nne zikikamilika taratibu basi unapata na leo miezi mitatu au minne unaambiwa subiri *board* au kikao cha *management* ni muda mrefu.

Kwa hivyo, nadhani ni vyema inafika wakati mtu aelezwe tu kwamba kitu hichi kinawezekana au hakiwezekani na mtu atafute njia nyengine na mabenki yamekuwa mengi sasa hivi. Sio kwa sababu yangu mimi, wananchi

wanasikitika. Mimi sina mashaka nao watu hao, nawashukuru sana watu wa PBZ kwa jitihada zao wanazochukua.

Jengine kuhusu *dialing room*. Ninataka niwashauri waifanyie marekebisho, watakuja kula hasara kwa mujibu wa *rate* zinavyokwenda za dola hivi sasa kama hawakuangalia hilo. *Dialing Room* sasa hivi nawashauri waiangalie kwa makini kabisa ukilinganisha na mabenki mengine, hii ni benki yetu.

Baada ya hapo nije kwenye kitengo nyeti cha *ZRB* ukurasa wa 48, nasaha zangu hapa Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri kwanza wangetafutwa kwanza Mashakhe wawili au watatu, wakatoa nasaha namna gani ya kukusanya hizi pesa. Wafanyabiashara wetu wamekuwa wakiteseka na *ZRB*, tunataka watumie lugha iliyokuwa nzuri ya kufahamishana. Wananchi wa Zanzibar ni wasikivu na watulivu lakini ukitaka kutumia nguvu kwa kuhusiana na mapato utawaumiza tu.

Siku zote nasema Zanzibar tumerogwa, sijui nani katuroga. Leo mafuta Tanzania Bara rahisi kuliko hapa kwa Shs. 150/- kwa lita mpaka Sh. 120/-. Leo wenye vyombo vyao wanataka kutia mafuta Bara kufika hapa wanahojiwa. Sasa huu umekuwa ndio muungano kweli huu, Mhe. Waziri hapa nitahitaji maelezo. Ikiwa mafuta yako unanunua Bara ukija ukifika hapa unaambiwa ununue mafuta hapa, unamlazimisha mtu kula chakula chake. Tumeshindwa sisi kujipanga wacha wenzetu wa Tanganyika waendelee, sisi hatujawa tayari kuendelea. Shs.150/-. Sh. 120/-kwa lita ya mafuta ni mengi. Hatuwezi kwenda namna kama hii, huwezi kumlazimisha mtu leo amepika wali, kesha ukamwambia ale muhogo, wakati chakula chake mwenyewe ukampangie mtu. Mafuta Tanzania Bara yamekuwa rahisi kuliko hapa kwa ushahidi kamili.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 52 kuhusu Mfuko wa Barabara. Tumekuwa tukiweka wawekezaji wetu tuliokuwa tukiwahimiza waekeze lakini leo njia ya Jambiani kuna mahoteli karibu 20 au 15, tokea dunia ilipoanza barabara ile haijaangaliwa. Wawekezaji siye wanatwita kutuelezea hilo, tena ni wageni, hetu tuwaoneshe njia ya matumaini mazuri wale watu. Hapa ukimuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu jawabu analolitoa analijua Mwenyezi Mungu. Tena wawekezaji hao wanalipa kodi zote *ZRB*, ajira watu wanapata lakini barabara ya Jambiani haipitiki kuelekea Kibigija. Hapa atakapokuja Mhe. Waziri aliangalie kwa jicho la huruma. Wawekezaji sisi wanatwita kutulalamikia Mhe. Naibu Spika.

Jengine Mhe. Waziri umekuwa unafanya jitihada sana za kukusanya mapato. Mimi ni mfanyabiashara Mhe. Naibu Spika, nakuwa naleta magari, nashirikiana na mwenzangu lakini kwa mwendo tunaokwenda hivi sasa

tutashindwa kuleta magari hapa. Ingawa Mhe. Waziri wa Fedha jana aliinuka akasema serikali hii inathamini wananchi wake. Lakini kwa huu mwendo unaokwenda biashara itatushinda sisi wengine na itabidi tubaki Bara. Itabidi Zanzibar ikose mapato kuhusu ushuru. Usumbufu umekuwa mwingi na usumbufu wenyewe wengine kuruhusiwa na wengine kutokuruhusiwa. Leo magari ukitaka kuyapeleka Bara unaambiwa ukayapakie bandarini kwenye krini na hiyo krini yenyewe haipo na hata kama ingekuwepo haikidhi, ukiitia gari inafungwa kamba huku na huku, ukiitia kwenye meli inachunika, ukimuuzia mtu hatokubali.

Mhe. Naibu Spika, hii ndio biashara yetu kubwa wengine tunayoitegemea ni biashara ya magari. Tulipunguziwa ushuru kwa makusudi hapa ili angalau tupate biashara. Bora ushushe kule kule Bara gari unaipata iko *fresh* kabisa. Wengine wanakuja wanatumia kwa njia zao nyengine, vitendea kazi hakuna na mambo mengi mengineyo. Leo hotuba hizi nyengine za kudanganya katika kitabu hiki. Unaambiwa kuna kifaa kimeletwa bandarini, bandari yenyewe iko wapi, ikishafunga meli moja tu bandari haipo.

Mhe. Naibu Spika, tunadanganyana humu mchana hadharanasi, hatujawa tayari, unaposhindwa mwambie mtu hili miye limenishinda si aibu, aibu kuiba. Leo tunaambiwa imejengwa bandari, vitabu chungu mzima vyengine leo wananchi wanaumia humu. Mhe. Waziri nasaha zangu mimi unapokwenda upepo ndio ninapokwenda. Mimi nitashusha gari zangu Bara na nita-*declare* kule kule, lakini mapato yataumia hapa kwa kisingizio cha mji tu, huo mji mpya uko wapi hapa? Miye siujui huo mji wenyewe au Mji Mkongwe? makaro mabovu, ukenda nikikuonesha kuna mashimo yamewekewa alama ya majiti mtu asije akatumbukia. Ah! Mheshimiwa nisikutajie jimbo lako la Mji Mkongwe japo kuwa lipo hilo jiti. Kuna Msikiti sehemu ya Manispaa ya Mji Mkongwe pale kuna karo leo miezi mingapi limewekewa jiti ili mtu asije akatumbukia ni aibu. Sasa naambiwa mipango miji, mji huo uko wapi, hebu tueleze huo mji mpya uko wapi hapa? Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Baada ya maelezo hayo mimi nilikuwa sina mchango mkubwa, kubwa mimi na Wizara ya Afya tu, nitahitaji maelezo ya kina kabisa kuhusu Wizara ya Afya kwa nini pesa zao hawapewi asilimia, ikawa idara yake Wizara ya Fedha ina asilimia kubwa inapata. Kwa hayo machache nitahitaji maelezo Mhe. Naibu Spika, ili kuiunga bajeti hii mkono.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa mkichangia mzungumze na Spika huku juu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima tukakutana tena katika Baraza hili baada ya kishindo kikubwa cha jana.

Mhe. Naibu Spika, watu wanaweza kudhani wameshinda kupitisha bajeti lakini wananchi wamejua wepi wanaosimamia maslahi yao katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fura ya mimi kuichangia wizara hii nzito ambayo katika bajeti yake Mhe. Waziri kaiita mwenyewe kwamba ni moyo wa serikali. Naamini kuwa ni moyo wa serikali. Mtihani wake leo katika mchango wangu huu ni kwamba tuone huo moyo huu una dalili wa kuupa uhai mwili au moyo wenyewe unaumwa uko taabani unahitaji by passes nyingi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya uchache wa muda nitakwenda moja kwa moja katika yale niliyokusudia kuyachangia. Kwanza Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamesema hapa kwamba hakuna nchi inayoweza kujiita ni nchi huru, inayojitawala, ikasimamia maslahi ya watu wake ikiwa haina uwezo wa udhibiti wa masuala yake ya fedha, uchumi na sarafu. Kwa hivyo, kwanza nianze moja kwa moja niwaombe wananchi wa Zanzibar, wasikilize maneno mengi wanayoambiwa. Lakini wawe makini katika kufanya maamuzi kwamba bila ya Zanzibar kupata mamlaka yake kamili, hakuna litakalokuwa katika maendeleo ya nchi hii. Katika mamlaka hayo kamili moja wapo ni kusimamia mambo ya nje wenyewe Zanzibar, pili kusimamiwe wenyewe uraia na uhamiaji lakini linalohusika na wizara hii ni kusimamia sarafu na Benki Kuu yake wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kazungumza hapa Mhe. Asaa Othman Said kwamba walipokwenda kuzungumza na *Governor* anawambia Benki Kuu haisimamii chumi mbili, inasimamia uchumi mmoja tu wa nchi moja. Mimi ninavyojua Jamhuri ya Muungano na ndivyo inavyosema Katiba yetu kwamba huu ni muungano wa nchi mbili, wala Zanzibar haikujifuta na Inshallah haitojifuta mpaka kiama tukijaaliwa.

Tunapoambiwa kwamba hakuna chumi mbili najiuliza mimi wanakusudia nini au ndio ile hadithi kwamba tumeliwa dungu msokoni tulizokula tuziteme na mchezoni hatumo. Kwa sababu Zanzibar haikuuza uhuru wake kwa Tanganyika, imekabidhi sehemu ya mamlaka yake na sehemu ya mamlaka ya Tanganyika kuunda Jamhuri ya Muungano. Sasa vyombo kama hivi vinapofika pahala vikawa na jeuri kama hivi, sio kama vinasimamia uchumi mmoja tu, hiyo ni dharau ya mwisho kwa Wazanzibari na Wazanzibari nakuombeni tukomeshe jeuri hii na dharau hii kupitia mbadiliko ya Katiba kurejesha mamlaka kamili ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nimepata swali moja anisaidie Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja kufanya majumuisho. Tunazungumzia katika suala la Katiba suala la sarafu, lakini hapo hapo Jumuia ya Afrika Mashariki inazungumzia kuna sarafu ya pamoja ya Afrika Mashariki. Mhe. Naibu Spika, gazeti hili la *The East African* la tarehe 27 Julai hadi tarehe 2 Agosti, linaelezea hapa ukurasa wa mbele unasema kwamba tunakaribia kuelekea katika Jumuia halisi iliyosimama hapa. Suala la sarafu ya pamoja Afrika ya Mashariki sasa linaanza kuonekana linakaribia baada ya wanaojadilika kufikia makubaliano juu ya itifaki ya msingi katika suala hili.

Suala langu nafasi ya Zanzibar katika kuelekea kuwa sarafu ya pamoja ikiwa itakuwepo ya Afrika Mashariki? Kuna hatari kubwa sana kuja kuingizwa katika sarafu ya pamoja kwa kupitia mgongo wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu mnapokuwa na sarafu ya pamoja na eneo kubwa kama hili lilitokezea lolote litakalopelekea kuadhibiwa kwa nchi mwanachana tutakuja kuadhibiwa kwa pamoja. Mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, sasa hivi katika Umoja wa Ulaya, kuna nchi zimevurunda uchumi wao na kuathiri sarafu ya *Euro*, leo nchi ya Ugiriki inachukuliwa hatua kwa sababu imefanya udanganyifu katika kutoa ripoti juu ya uchumi wake wakati ule wanaelekea katika kuwa na sarafu ya pamoja ya *Euro*.

Sasa najiuliza tunapokuja kupeleka kwa mgongo wa pamoja wa Jamhuri ya Muungano ambapo kumejaa ufisadi. Huku kwetu upo, tumeona hapa katika bajeti hizi za wizara lakini kule umezidi wakaja wakaadhibiwa wao na sisi tutakuwa katika mkumbo mmoja. Nataka Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo akija anisaidie. Viongozi wa serikali wanasimamia vipi maslahi ya Wazanzibari katika masuala haya, hilo moja Mhe. Naibu Spika.

La pili Mhe. Naibu Spika, nilimuuliza swali Mhe. Waziri siku aliyotuwasilishia bajeti kuu, katika majumuisho akawa hakunijibu, na mimi nikashindwa kumsimamia kwa sababu bajeti kuu haina vifungu. Bajeti ya Wizara yake hii ina vifungu naomba leo anijibu. Takwimu alizotuletea katika bajeti kuu na alizotuletea leo katika hotuba yake hii, zinaonesha kwamba mapato tutakayopata kutokana na ushirikiano katika masuala ya misaada ni bilioni 40, kama misaada ya kibajeti dhidi yetu lakini mimi nilimwambia kama nikitumia hotuba ya Waziri Mgimwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano alipokuwa akiwasilisha bajeti ya muungano, inaonesha kwa mwaka huu wa fedha za misaada ya kibajeti ni trilioni 1,136.1 bilioni. Kama tutafanya asilimia 4.5 ya fedha hiyo Zanzibar ilikuwa tupate bilioni 52.34. Vipi leo vitabu vya Zanzibar vinatuonesha tutapata bilioni 40. Nani anamdanganya katika hili? Nani anamdhulumu nani katika muungano huu

tunaoambiwa ni mzuri sana katika dunia. Lakini si hilo tu hawa pia wanakwenda wakitafuta misaada na mikopo ya miradi ya maendelea kwa ajili ya Jamhuri ya Muungao. Katika fungu hilo katika bajeti ya Waziri Mgimwa akasema kuna trilioni 2,191. Ukifanya Mhe. Naibu Spika, kama Zanzibar ipo ya asilimia 4.5 ya fedha hiyo basi tunapaswa kupata 98.62 bilioni.

Halafu kuna mifuko ya kisekta ambayo inajumuisha maeneo mengi yaliyokuwa siyo ya muungano lakini inapokwenda kuombwa inaombwa kwa jina la muungano, kuna bilioni 500 kama Zanzibar ilikuwa ipewe asilimia 4.5 imepaswa tupewe 22.5 bilioni. Kwa ujumla mafungu hayo matatu Mhe. Naibu Spika, kama Zanzibar ingekuwa asilimia 4.5 ilikuwa tupate shilingi 163.4 bilioni sio bilioni 40. Kwa nini viongozi wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanashindwa kusimamia masuala haya ya haki za Zanzibar.

Katika hili nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, katika hotuba yake ya Kamati ambayo ameisifu na mimi naisifu. Imeandika na imejengewa hoja kitaalamu, nampongeza sana Mhe. Salmin Awadh Salmin na namwambia Mhe. Rais tunapomwambia kama kuna Mawaziri wengine wamechoka anazo nondo kama hizi azitumie. Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwamba kalitaja naomba maelezo leo.

Lakini pia kuna fedha nyengine nyingi ambazo zinapatikana, karibuni Tanzania ilisaini na Benki ya Dunia katika mkutano wa nchi za Afrika na Benki ya Dunia, mkopo wa dola milioni 196.5 hii hapa Mhe. Naibu Spika, imeripotiwa ndani ya mitandao, 196.5 milioni kwa ajili ya kuimarisha sekta ya gesi na mafuta ambayo mpaka sasa hivi ninavyozungumza haijaondolewa katika mambo ya muungano. Sisi Zanzibar tumepata kiasi gani katika kuendeleza sekta hii katika fedha hii ambayo imetolewa mkopo na Benki ya dunia. Naomba Mhe. Naibu Spika, nipate maelezo.

Mhe. Naibu Spika, mambo ni mengi na muda ni mchache, nimeyazungumza hayo kwa sababu yanagusa Wazanzibari. Lakini vile vile nilitaka nisaidiwe kuna taasisi za kimuungano zinakusanya fedha nyingi kama *TCRA*, *TCAA*, kuna Benki ya Posta, *TTCL*, tulikuwa kuna hisa zetu Zanzibar, mapato ya Zanzibar yako wapi katika taasisi hizi au ndio Zanzibar imegeuzwa shamba la bibi, Watanganyika kuja kuvuna sisi huku tubaki kuangamia tu kwa maslahi yao. Naomba maelezo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba maelezo ni hili ambalo amelizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Moja katika raha ya kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha kila Idara yake kwenye fedha za kawaida wamepata asilimia mia moja kila idara. Lakini kuna huduma za msingi za wananchi, tumeichambua hapa fedha zilizokuwa zikiingizwa, elimu hapa na maeneo

mengi. Lakini kwao Wizara ya Fedha kila idara kwenye fedha za matumizi ya kawaida ni asilimia 100. Nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha hichi ndio kipa umbele cha serikali inayojali wananchi wa Zanzibar?

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hichi ukurasa wa 25 tumeambiwa Idara ya Bajet kuna shilingi bilioni 2,520 zilihaulishwa kwenda katika kifungu cha safari za nje za viongozi wakuu. Mimi nilikuwa naomba mara nyingi huwa naliuliza hilo, hebu leo Waziri wa Fedha akija kufanya majumuisho atusaidie hilo, fungu la matumizi ya safari za nje na za ndani za viongozi wetu watatu wakuu hawa Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hebu tuambiwe kwa mwaka mzima wa fedha zinagharimu kiasi gani wananchi wa Zanzibar. Tuje tuambiwe kwa pamoja halafu nije niambiwe mchanganuo wa mmoja mmoja katika viongozi hawa watatu katika viongozi wakuu wa Zanzibar, tutajiwe.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba maelezo tulipokuwa tukichangia bajeti ya mawasiliano tulihoji kuhusu fedha za mamlaka ya usafiri baharini *ZMA*. Jana katika ule mburuzo miliotuburuza hapa, hatukufika pahala pa kuhoji vifungu katika maeneo mengine. Lakini katika maelezo ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu alisema fedha zilikuwa zinazotoka kwenye kampuni ya *Filtex* ambayo ni wakala wa *ZMA* Dubai, zilikuwa zinakuja kwa utataribu wa kawaida wa kifedha na zikiingia Hazina labda mamlaka haikuundwa.

Naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo atakapokuja aje anitajie Benki ya Dubai iliyotumika kusafirisha fedha hizo na Benki ya Zanzibar ipi iliyopokea fedha hizo kwa niaba ya Zanzibar. Naomba hilo sana na kama hilo sikujibiwa nitakuja kuikwamisha bajeti yake tukijaaliwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuunga mkono hoja za wenzangu nyengine zote, Mhe. Mohamedraza amezungumza suala la tozo la kodi ya simu la shilingi elfu moja na vipi athari yake kwa Zanzibar. Naomba maelezo kuhusu maeneo mengine mbali mbali ambayo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitaka maelezo. Kwanza kuhusu pencheni, kufanyiwa uhakiki ili kujua madudu yanayoendelea katika sehemu hizi. Baadhi wa Wawakilishi humu ndani waliwahi kutoa mpaka ushahidi wa jinsi fedha zinavyotafunwa kwa viinua mgongo hewa kwa pencheni hewa, mishahara hewa, naomba kupata maelezo.

Naunga mkono hoja vile vile ya kusema wahasibu imefika pahala waondolewe wamekuwa wakibaki katika sehemu moja kwa muda mrefu. Na wakaguzi wa ndani kupewa Mkuu wao vile vile. Naunga mkono hoja ya mashirika na taasisi zinazojitegemea kwa bajeti zake angalau ziletwe hata

kama kwa taarifa katika Baraza hili ziambatanishwe na bajeti Wizara husika hata kama hatuzipitishi sisi, zinapitishwa na bodi yao lakini tuzijue hapa ni kiasi gani.

Pia Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ambayo niliitoa mimi ina ning'inia tangu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya kuundwa Kamati Teule kwenda kuchunguza suala la mradi wa *e-Government*. Mhe. Waziri katika kitabu chake katupa maelezo ukurasa wa 70 mpaka 74, lakini sula la msingi halikujibiwa ambalo mimi na wewe ukiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria tuliyadai na barua hii ina saini yako Mhe. Naibu Spika, ukiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ya Utawala, kutaka mnyumbuliko wa matumizi, sio kuja kupewa hadithi hizi ambazo tulizokuwa tumetiliwa katika kitabu cha bajeti, mnyambuliko wa matumizi moja moja, tunataka hili. Iinaonekana hili limewashinda tumeshachoka kuliuliza sasa tunataka iundwe Kamati Teule ikachunguze ije ilete ripoti Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar .

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa maeneo mawili kwa ufupi sana. Kwanza Mhe. Naibu Spika, suala la deni la taifa. Hili katika kitabu hichi sikuliona lakini katika hotuba kuu ya bajeti ilitajwa katika ukurasa wa 16 hotuba kuu ya bajeti kwamba deni la taifa limeongezeka kutoka bilioni 209 hadi kufikia bilioni 252.3. Nataka kujua kwamba serikali ina mpango gani wa kulishughulikia deni hili. Bahati mbaya miradi mingi inayoombewa mikopo sasa inakwama, tena ni mabilioni ya fedha za wananchi maskini wa Zanzibar, kuna mradi wa *e-Government*, kuna mradi wa jengo la abiria la Uwanja wa Ndege, tumelizungumza jana, tumepigishana kelele humu ndani mpaka tumetoka, kuna mradi wa *ZUSP* ambao kila siku ni maneno tu hakuna kinachokuwa. Mhe. Rais mlimfikisha pahala akenda akatangaza kila kipembe cha nchi hii kwamba mji wetu utang'ara. Hakuna chochote mpaka leo, miradi mingi, sina muda wa kuielezea lakini nataka kuambiwa kuhusu deni la taifa.

Pia niiombe na Kamati ya *PAC*, washirikiane na *CAG* kwenye kuhakiki deni la taifa la Zanzibar. Tumewahi kuona kwa upande wa Bara Mhe. Naibu Spika, kiasi gani deni la taifa lilivyotumika watu kufanyia ufisadi, kwa sababu inaonekana kama vile hakuingiliwi. Nataka maelezo katika hilo na naiomba Kamati inayohusika ifanye uhakiki kwa kushirikiana na mkaguzi wa hesabu za serikali.

Mhe. Naibu Spika, niseme la mwisho kabisa nataka Mhe. Waziri wa Fedha akija kama yeye ndiye mwenye dhamana wa mali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, aje anipe maelezo kuhusu suala la *Zantel*. *Zantel* ilipoundwa SMZ ilikuwa na asilimia 18, Kampuni ya *MICO* ilikuwa na silimia 23.5 ya hisa,

Kampuni *HIT Johusiza* ilikuwa na asilimia 23.5 ya hisa na *Etisalaat* ilikuwa na silimia 25 ya hisa.

Mhe. Naibu Spika, ilipoanza kampuni hii tunakumbuka vishindo ilivyotiwa na upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ikahangaika sana lakini hatimaye ikaweza kusimama na ikawa inajiendesha vizuri. Nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar wa awamu ya tano Dokta Salmin Amour na aliyekuwa Waziri wake wa Mawasiliano Mhe. Amani Abeid Amani Karume kwa kazi waliyoifanya mpaka kampuni hii ikasimama Zanzibar, licha ya upinzani mkubwa kutoka Tanganyika. Wazanzibari wamehenyeka mpaka kampuni hii ikasimama. Leo asilimia 65 ya mapato ya *Zanteli* yanatoka katika wateja wake waliokuwepo Zanzibar na asilimia 35 inatoka kwa weteja wengine.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka maelezo kwamba niliwahi kuzungumza hapa kwamba kuna mkakati wa hujuma dhidi ya Zanzibar katika suala la *Zantel*. Wamelizungumza wengi hapa imefika pahala kutangazwa *tender* ya kuitaka kuiuza Kampuni ya *Zantel*, wenye hisa wananchi wa Zanzibar kupitia Wawakilishi wao hawana taarifa humu ndani. Matokeo yake Mhe. Naibu Spika, kutangazwa kule kwa *tender* kumefanya wale wanaotaka kuinunua kwenda ndani kujiridhisha kutafuta taarifa matokeo *Zantel* imekuwa imejianika wenyewe, iko uchi kabisa kila kitu kama kampuni ya biashara kinajulikana na washindani wake wanaotaka kuinunua.

Mhe. Naibu Spika, nimesikitika zaidi kwamba kulikuwa na uongozi mbovu kati kati hapa katika *Zantel* uliopelekea hali hii. Juzi tumekutana mimi na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Mhe. Marina Joel Thomas tumekutana na uongozi wa Zantel yule *CEO* anaitwa Bwana Pratap alikuja kutaka kutuona. Anatwambia katika miaka mitano iliyopita *Zantel* imepata hasara ya dola milioni 150. Lakini cha kuchekesha baada ya kuondoka tumeletewa taarifa kwamba hii ni siri msije mkaizungumza, kuna siri katika fedha za wananchi wa Zanzibar, kama siri kubwa za kampuni mmezianika nyinyi wenyewe kwa kutangaza *tender* kila mtu akaingia ndani akazigundua mpaka siri za ndani za *Zantel* zimekaaje wakati wamewaalika wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, huyu bwana Pratap tusidanganyane, kaletwa kwa lengo maalum na aliyemleta ni *Etisalaat*, kama ni *Chief Executive Officer (CEO)* mpya kuja kuimaliza, kuitia kabari, kuifilisi *Zantel* ili ipate kuuzwa iondoke Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, *Zantel* ni kampuni ya Wazanzibari hata jina lake limeanzia na ‘Zan’ ili kutoa utambulisho kwa Wazanzibari. Wamefisidi kampuni hii, ilifika pahala kulikuwa na ma-*bonus* makubwa makubwa mwaka 2005/2006 wakuu wa *Zantel* wamelipana *bonus* kufika dola 70,000 kwa mtu. Mwaka 2007 wamelipwa *bonus* zimekithiri, (dola 200,000) laki mbili.

Mhe. Naibu Spika, dola 70,000 ni mia moja, thalathini na tatu milioni za Tanzania (133,000,000) dola laki mbili (200,000) ni mia tatu ishirini milioni za Tanzania (320,000,000) watu wamelipana *bonus,* huku huduma mbovu. Na huduma kwa nini zimekuwa mbovu? kwa sababu *focus* yao wameondosha Zanzibar bila ya kujipanga, wamekwenda kuhamia Bara. Matokeo yake huku kwenye kupata mapato wamekuvuruga, huduma ni mbovu, wameondosha *focus* yao hapa makampuni mengine ya Bara yameingia hapa, wameongeza wateja. Leo kuna watu wana laini zaidi ya moja kwa sababu *Zantel* inaonekana haina huduma za uhakika. Matokeo yake mapato yaliyokuwa asilimia 80 ya *Zantel* yanayotoka Zanzibar yameshuka mpaka yamafikia asilimia 65 kwa sababu watu wametafuta *line* nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kinachonisikitisha zaidi katika hili sisi ni Wajumbe katika bodi ya *Zantel*, wanasikitika sana, mmoja katika wajuzi wetu wakubwa ndugu Khamis Mussa Omar. Ndio mmoja katika wajumbe wa bodi, hapo nyuma alikuwepo ndugu Abdalla Hussein Komba naambiwa sasa hivi kaingia Dkt. Juma Malik, Katibu Mkuu wa Mawasiliano. Hao wanafanya nini katika kulinda maslahi ya Wazanzibari katika hili. Wamo katika Bodi kulinda maslahi ya Wazanzibari? au na wao wenyewe wanashiriki ili kuiangamiza *Zantel*? Maana tunajiuliza wanatulindia vipi maslahi yetu haya.

Mhe. Naibu Spika, nataja maelezo ya kina kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha juu ya hili aje atwambie. Mimi nina ushauri kwamba ikiwa *Etisalaat* imewashinda na leo wanataka kuiuza, basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafute njia ya kuiokoa kampuni yake hii. Hii ni kampuni ya Wazanzibari, ni utambulisho na ni fahari ya Zanzibar. Mimi naamini leo zikitangazwa hisa kuuzwa, Wazanzibari wapo tayari kununua hisa, wananchi wa Zanzibar wauziwe hisa na duniani yamefanyika hayo. Wauziwe hisa watapata faida na serikali itapata kunusuru lakini hii kampuni ibakie Zanzibar. Hii inalipa katika kodi bilioni 21 kwa mwaka kwa *ZRB*. Leo kuna mkakati wa kuhamisha kodi zake zikalipiwe Bara ati kwa sababu ya kutaka kulipana fidia baina ya makampuni mbali mbali ya simu katika kupigiana simu. Mhe. Naibu Spika, hii ni hujuma dhidi ya Zanzibar, ni hujuma dhidi ya Wazanzibari inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kusema kwamba nimetaja maeneo mengi ambayo nataka maelezo na kwa sababu hiyo nisije nikaambiwa sikutangaza, natangaza kabisa, nitatumia kanuni ya 98(6)(c) kuzuia shilingi mia katika fungu la Wizara hii mpaka nipate maelezo ya kina juu ya mambo niliyoyatolea maelezo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyokuwepo mbele yako.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa *ZRB* kwenye Mamlaka ya Kodi ya Mapato Zanzibar kwa niaba yangu kwanza mimi sina tabia ya kusifu na kupongeza. Lakini Waswahili wanasema lisilobudi hutendwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa jimbo langu la Wawi nachukua fursa hii kuipongeza Bodi hii ya Mapato na shughuli zao wanazozifanya katika kutukusanyia mapato katika vyanzo mbali mbali vya mapato yetu. Kwa hali hiyo napenda nichukue fursa hii kumpongeza Kamishna wa *ZRB* kwa kuweza kusimamia vyema mapato yetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, dhana ya kodi ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa lolote, unapokuwa makini katika kusimamia mapato basi unakuwa makini vile vile katika kuleta maendeleo katika nchi. Kwa mnasaba huo napenda sana vile vile nimpongeze huyu Mhe. Waziri kwa kuwa makini sana katika kusimamia watendaji wake katika suala zima la kusimamia mapato yetu ili yasipenye kiholela.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Kamishna wa *ZRB* mimi hata ukinambia nikuoneshe hapo juu simjui, lakini ni kijana mmoja anayeonekana makini sana katika kufanya kazi zake na kutaka kuwaletea maslahi Wazanzibari kupitia kodi zao. Huyu kijana amefanya kazi nzuri mwaka 2012, hapa katika kuona kwamba Zanzibar mapato yake yanaingia katika mfuko mkuu wa serikali na katika kuona kwamba anakuwa makini katika kuwasimamia aliweza kutoa *stop order* kwa hili Shirika la *Precision* ili ku-*save* zaidi ya bilioni 2 za Tanzania. Sasa la kusikitisha pamoja na umakini na umahiri wa Waziri wetu wamekuja watu juu juu hivi wadogo wadogo, kwa kutumia ki-*note* cha mkono tu waka-*beat stop order* iliyotolewa na kijana wetu Kamishna hapo jambo ambalo ni baya sana inasikitisha Mheshimiwa. Mimi nataka Waziri akija hapa anipe maelezo na niridhike kwa nini Mtendaji Mkuu *ZRB* akatoa stop order akaja Mkurugenzi mwengine kwa kutumia maandishi ya mkono tu aka-*beat* ile *stop order*. Hakum-*beat* yule Kamishna wa *ZRB*, kam-*beat* Rais wetu kwa sababu yule jamaa ameteuliwa na Rais pale *ZRB*. Sasa Waziri aje anieleze amemchukulia hatua gani yule kijana aliyefanya mambo haya, sitaki niseme ya kijinga kwa sababu kanuni zetu haziruhusu kusema lugha chafu lakini kufanya mambo yaliyokuwa hayana maana kama vile.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa useme na Spika huku mbele.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nakuangalia sana. Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kwamba hawa vijana wetu wanaoteuliwa teuliwa vijana wenye taaluma wakishateuliwa pale na Rais hujiona kama hii nchi ni yao bwana, hii nchi si yao. Hii nchi ni yetu tumefanya kazi kubwa sisi kuleta uhuru wa nchi hii wawe makini sana wanapopata hizi nafasi pale.

Mheshimiwa inasikitisha kwamba huyu kijana pamoja na kosa hilo hivi karibuni tu alikuwa anataka kuwaondosha *ZAT* pale, ambayo wenyewe *ZAT* wameajiri zaidi ya watu 200 wazalendo wanatoa ajira leo anataka kuwaondosha, ninashukuru kwamba labda serikali imeingilia kati *ZAT* inaendelea na Mungu ajaalie iendelee kusudi waweze kutuendeshea vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la kodi ya simu ya shilingi elfu moja hii. Kodi hii Mhe. Mohammedraza pale Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Uzini alisema kwamba Zanzibar tumekuwa kama mbirimbi, kwa sababu haukodiwi, mtu anakuja kujichumia tu na kuondoka au zianguke zioze, huo ndio Mbirimbi ulivyo. Sasa hivi huo Mbirimbi bwana Zanzibar ni nchi hatuwezi kuachia kodi hii iendelee, ati wanasema wataipeleka kwenye mambo ya maji Bara huko wametaja hapa, naomba uniruhusu ninukuu kidogo anasema kwamba kodi hii katika gazeti la Uhuru la Ijumaa ya tarehe 12/7/2013, amesema kwamba kwa mujibu wa serikali mapato hayo yanayotokana na tozo hiyo yataharakisha maendeleo katika sekta ya maji, wakala wa umeme na mambo ya maji vijijini ambapo sisi hatuna hapa, kuna na mfuko wa barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara za vijijini, zote hizi ni za Tanganyika. Katika hili mimi nashauri kwamba kodi hii imalizie Chumbe, ikija ikiingia Unguja patavuka kivumbi kabisa kabisa katika hili lazima tuwe wazi, kama serikali itatumia mabavu kutudhibiti mimi nitaandamana na wananchi katika hili. Mimi nitakuwa mbele kuona kwamka kodi hii haiingii hapa kwa sababu haina maslahi ya nchi.

Sasa naomba katika hili la mambo haya vijana waliokuwa wanafanya mambo ovyo ovyo naona tabu hata kusema lakini wanafanya mambo ambayo hayana mantiki na mapato ya nchi. Napenda sana nimpongeze Balozi Seif Ali Idd, Mhe. Waziri wa Fedha kwa zile *statement* zenu mlizozitoa jana, mimi nadhani hawa vijana wanaokosa nidhamu hawa mtawadhibiti haraka au mtawafanyia marekebisho hii ninawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, niende katika mfuko wa barabara. Mhe Naibu. Spika, mfuko wa barabara huu ni muhimu sana na mimi dua zangu zinapanda sana, naona kama Uspika unakutembelea Mungu akipenda. Mhe. Naibu Spika, katika hili nadhani mtandao wa barabara ni muhimu sana, kwa hivyo mfuko huu wa barabara ni mfuko muhimu sana, sio tu kwa kufanya ukarabati zile

barabara ambazo zimesinyaa lakini ni mfuko muhimu hata kuanzisha zile barabara zilizosahauliwa kwa miaka mingi. Kwa hivyo mfuko huu unahitaji uwe na fedha za kutosha kwa sababu ndio unaoweka *network* baina ya kijiji na kijiji, baina ya mji na mji, baina ya mtaa na mtaa. Mheshimiwa ili tuweze kuwasiliana vizuri lazima tuwe na barabara nzuri sana ambazo zinafanyiwa ukarabati na mfuko huu.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kusikitisha kwamba mfuko huu vyanzo vyake vya mapato ni kidogo sana, unategemea tozo la kwenye shilingi elfu moja, shilingi mia kwenye mafuta. Kwa kweli hauna vyanzo vingi vya mapato. Sasa ninachoshauri Mhe. Naibu Spika, namshauri Waziri wa Fedha kama kutahitajika sheria itakayotanua wigo wa mapato kwa huu mfuko basi atuletee Barazani kusudi tuipitishe haraka ili huu mfuko uweze kupata nguvu zaidi, kwa sababu ni muhimu sana na isitoshe mfuko huu una haja ya kupata fedha kwa sababu haya makampuni wanaojenga mabarabara yetu hata wakiondoka njia wameshaziharibu sana hizi barabara tulizokwishazijenga hasa zilizojengwa na awamu ya sita ya Mhe. Amani Abeid Karume, amefanya kazi kubwa kutujengea barabara.

Sasa katika hili mimi nashauri kama ikiwa itawezekana Waziri wa Fedha atuletee sheria ya kuanzisha mfuko unaoitwa *enviromental habilitation fund* huu wa ku-*rehabilitated* mazingira. Mfuko huu uwe chini ya Mfuko wa Barabara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika Kitengo cha Mazingira kwa sababu hizi barabara wanaziharibu kila *contractor* akija hapa akijenga barabara akatwe asilimia 10%. Hii asilimia 10% iingie katika hii *enviromental habilitation fund* kusudi mfuko upate nguvu na hizi nyengine ziende kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, mazingira waweze kuziba ziba yale mashimo katika viwanda vyako vile vya kutengeneza kokoto kama ulivyotueleza kwenye bajeti Mhe. Waziri, kule viwandani kwako mashimo ni mengi, katika viwanda vyako mashimo ni mengi. Sasa mfuko huu Mhe. Waziri utakusaidia sana Mhe. Waziri ambaye ni mtoto wangu wewe katika kurekebisha mazingira haya.

Mhe. Naibu Spika, niende sasa katika suala la Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kama pana pahala pa kusifiwa hasa basi ni Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hawa watu wamefanya kazi nzuri na katika hili napenda nimpongeze mwanangu pale Waziri kwa kuweza kuiondosha *ICU* kwa sababu *PBZ* ilikuwa *ICU* ikipumua kwa mashine. Sasa huyu kijana bwana makini sana Mhe. Omar ukimuangalia unamuona ni mtu wa kawaida tu na mwana siasa wa kawaiada kama mimi, lakini kwa wasifu wake wa ndani huyu kijana ana vipaji vitatu vikubwa. Naomba haraka haraka nivitaje.

Huyu kijana ana ubongo wa hekma, huyu kijana ana ulimi wa fasaha na huyu kijana ana moyo unaowaza kuhifadhi siri za nchi hii kama kaburi linavyohifadhi maiti. Kwa kweli vipaji vyake makini sana ameisaidia sana *PBZ*, huyu kijana ili kuona kwamba inafufuka. Nitakuwa mchache wa shukurani Mhe. Naibu Spika, kama sikumpongeza Mkurugenzi *Managing Director* wa *PBZ*, yule kijana mmoja makini sana. Ana heshima, mpole na mtendaji. Yule kijana ninampongeza sana bila ya kumsahau Katibu Mkuu pamoja na benchi lake la ufundi, Katibu Mkuu Fedha Khamis Mussa Omar na kwa kwenda benchi lake la ufundi wataalamu pale wamefanya kazi nzuri sana katika hili ninawapongeza sana.

Aidha Mhe. Naibu Spika, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuwapongeza hawa mameneja wa matawi hasa hapo Malindi, Chake Chake na kadhalika. Hawa mameneja hawa wanafanya kazi nzuri na *keep it up*, mnafanya kazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni kwamba *PBZ* sasa hivi kunakuwa na changamoto wanazopambana nazo ni kwamba katika kipindi cha mishahara mrundikano unakuwa mkubwa sana pale. Mimi ninachoshauri na ninachoomba waanzishe *ATM machine* katika vijiji mbali mbali vikiwemo vya Vitongoji Umangani pale, waweke kwa sababu kuna wafanyabiashara wengi pale. Hilo moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ikiwa kuanzisha *ATM Machine* kila pahala ni tatizo basi waanzishe *mobile service* wapiti-pite humo ili wakipita na magari yale waweze kufanya *mobile service*, *than* niondoke hapo niende kwenye Mamlaka ya Vitege Uchumi.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka nakwenda kwenye Mamlaka ya Vitega Uchumi. Kwanza hii ni mamlaka inayoshawishi wawekezaji, hii mamlaka inahitaji kazi kubwa lakini inasikitisha sana mamlaka hii haiko makini kwa sababu uwekezaji unatakiwa unufaishe wawekezaji na sisi wananchi. La kusikitisha Mhe. Naibu Spika, ukenda mahotelini hasa huku Kaskazini ndio hatari, maana yake yale mahoteli hata mfagiaji, haya Mtumbatu na Mpemba wa Vitongoji hawezi kufyagia.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nataka nimsifu mwekezaji wa *Visitors Inn* kule Jambiani, yule kijana kwa kweli ni mzalendo na amefanya kazi nzuri na hata *cashier* ni Mpemba wa Wawi pale kajitahidi sana, ndio nikasema wawekezaji msisikilize maneno, kuna kijana yule kutoka Dubai ambaye ni Mpemba wa kwangu pale jimboni kwangu anataka kuekeza katika mambo kadhaa, ana *package* kubwa hapa, kijana mmoja aachiwe na yeye aweze kunufaika Wazanzibari hawa ndio wazalendo. Unamuona yule kijana pale Jambiani

wote waliopo ni wa-Pemba, ni Mtumbatu ni mnani na nani. Hivi ndio tunavyotaka Mhe. Naibu Spika.

Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, dakika zilizobakia ni chache lakini nitatumia uzoefu wangu wa ualimu kumalizia. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumze kdogo kidogo ili Mhe. Waziri anifahamu na Mhe. Waziri alipokuwa akitoa utangulizi wake amesema kwamba Wizara hii ni moyo wa serikali na mimi nasema ni moyo wa serikali. Lakini ninachokijua hivi sasa ni kwamba maradhi ya moyo yameenea kwa wingi katika nchi yetu na sababu kubwa ya kuenea kwa maradhi hayo ni kula kulikokuwa hakuna kipimo. Kwa hivyo ninamuomba ale kidogo kidogo ili asije akapata maradhi hayo ya moyo ikabidi tena atumie fedha za serikali kumpeleka India matibabuni.

Mhe. Naibu Spika, karibuni tulipitisha misaada ambayo ilifanya marekebisho ya kodi mbali mbali. Hivi sasa kumekuwa na malalamiko makubwa sana hasa katika kisiwa cha Pemba kwa wale ambao wanatuletea michanga kwa ajili ya ujenzi wa majumba yetu. Wanasema kwamba umekuwa ni ghali sana mchanga kuupata lakini wenye magari wanakuwa wanalalamika kwamba sisi Baraza la Wawakikilishi ndio tuliopitisha sheria mbali mbali za marekebisho ya kodi. Ningemuuliza Waziri tuje katika hii kodi ya mchanga ni kiasi gani hivi sasa inatozwa kwa wale wanaokwenda kuchota mchanga ili kupata kujua ni kiasi gani tunahitaji tulipe katika ununuzi wa mchanga kwa gari moja.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya *ZIPA* katika sheria ambazo pia tulizipitisha pia tuliigusa na ninachokijua ni kwamba wenzetu hawa walikuwa wanapata asilimia 2 ya ile *exemption* ambayo wanatoza wale wawekezaji. Lakini kwa sheria hii ina maana hii asilimia 2 wao wataikosa na kwa ujumla hizo Idara nyengine zinafanya kazi baada ya *ZIPA* kukamilisha, watu wa *TRA* mpaka mwekezaji aje apitishwe na *ZIPA*, watu wa *TRA* na wao ni hivyo hivyo. Lakini inavyoonesha watu hawa au Idara hii kama imewekwa nyuma na ruzuku wanayopewa ni ile ile kila mwaka utakuta ruzuku yao ni shilingi milioni 200, milioni 250, milioni 300 haibadiliki. Sasa kweli itaweza kuleta maendeleo hayo ambayo tunayoyakusudia ikiwa wao tuliowapa kipa umbele cha kuwaleta wawekezaji na wengine wanaoboresha uchumi katikia nchi hii.

Ninafikiri ningemuomba Waziri hilo akaliona kwamba hivi sasa kitengo hiki kina umuhimu mkubwa katika nchi yetu. Kwa hivyo ruzuku wanayopewa basi waongezewe isiwe kila mwaka inabakia ile ile ili utendaji wao wa kazi uongezeke.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika mitaji hii ya uhakiki mali na mitaji ya umma. Ninachokijua au kwa hotuba hii tumeona kwamba kuna gawio ambalo linatolewa kutoka mashirika ya *PBZ*, *ZSTC*, Bima na bandari na kwa ujumla nilivyofahamu mimi baada ya kusoma kitabu hiki nimeona kwamba mashirika haya yanachangia kwa ujumla milioni 400. Sasa hii ningeomba Waziri akanifafanulia. Je, katika hii milioni 400 kwa sababu haya mashirika uwezo wao ni tofauti, wanachangia shilingi milioni 400 kila mmoja; yaani milioni 100 mashirika manne au kila mmoja anachangia kutokana na ule mtaji wake alionao.

Lakini katika hilo pia Mhe. Naibu Spika, je tunaendelea na mpango huu huu wa mashirika kwa sababu ukiangalia bajeti iliyopita ni vile vile milioni mia nne katika gawio lao kupeleka serikalini. Utaratibu huu utaendelea hadi mwisho huko tunakokwenda mbele au tutaangalia sasa ki-*percentage* kwamba Wizara au Shirika, kwa mfano *PBZ* wamezalisha kiasi fulani, kwa maana hiyo sasa tutachukua *percent* fulani na sio kile kiwango kilichowekwa tu kwamba hiki kitabakia hivi hivi, wakipanda na serikali izidi kupata wakiporomoka nayo serikali ijue kwamba na wao wameporomoka. Kwa hivyo uwezo wao utakuwa ni huu, utaratibu huu utabadilika au ni hivi hivi tu.

Mhe. Naibu Spika, niende kidogo katika ujenzi wa barabara. Baada ya kupata mafunzo nimefahamu kwamba mfuko wa barabara dhumuni lake kubwa ni matengenezo na sio ujenzi. Lakini ninachokijua ni kwamba hivi sasa barabara ya Amani au tunayoita *Mkapa Road* inajengwa haitengenezwi. Sasa je, katika hili hatuoni kama tumekwenda kinyume na taratibu zile ambazo tumeziweka za huu mfuko wa kutengeneza barabara na sio kujenga barabara. Kwa maana hiyo kutakuwa na barabara nyingi baada ya kuzitumia fedha nyingi ambazo zitakuwa muda mchache hazipitiki. Sasa labda ningelimuomba Waziri akanifafanulia, je hizi fedha tutakuwa tumezitendea haki kuzipeleka katika ujenzi na sio matengenezo kama tuliyoyakusudia mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, labda niende Chwaka. Tukiangalia Skuli ya Chwaka tunaona kwamba wao katika utaratibu wao wanatoa ufadhili fulani kwa zile skuli ziliopo katika jimbo lile au ziko katika maeneo yale. Wao chuo hiki kinapata ruzuku kutoka serikalini, sasa na wao wanazalisha wenyewe kutokana na ada mbali mbali za masomo pale chuoni. Sasa hii fedha wanayoitumia kwa ajili ya kutoa misaada ya maendeleo ya baadhi ya skuli zilioko katika nchi zinatoka katika fungu gani? Fungu la mfuko wao ambao wanazalisha wenyewe au katika lile fungu ambalo linatoka la ruzuku kutoka serikalini. Je, hii kulikuwa na mkataba maalum uliosema kwamba kama unataka kujenga chuo ufanye hivi au ni ufadhili tu. Labda kama ni hivyo wataendelea kufadhili na sehemu nyengine au ni sehemu hii ya Chwaka tu.

Mhe. Naibu Spika, ninafikiri nimesema haraka haraka sana na wakati umekaribia naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa ninakushukuru na niwashukuru wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia kwa ushirikiano wenu mzuri na tunategemea kesho tumalize hoja hii na huku juu tumebaki na wachangiaji wawili tu. Kwa hivyo ninawaarifu wale wachangiaji wajitahidi waje mapema. Mmoja Mhe. Marina na wa pili Mhe. Ali Mzee Ali.

Baada wa hao nitamwita Waziri kufanya majumuisho na baadae tuingie kwenye vifungu. Tunaomba wale wote waliotoa hoja wafike mapema na sasa hivi kuna wajumbe wengi wana kawaida ya kusikiliza hoja ndani ya gari, hiyo hatuikubali tuthamini nguvu za wananchi tuje hapa tuwawakilishi kama walivyotuagiza.

Baada ya hayo ninahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 5 siku ya Jumatatu saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 8.54 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 05/08/2013 saa 3.00 asubuhi)